

## BUNGE LA TANZANIA

---

### MAJADILIANO YA BUNGE

---

### MKUTANO WA KUMI NA SITA

**Kikao cha Nane – Tarehe 12 Septemba, 2019**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

#### DUA

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mkutano wetu wa Kumi na Sita na Kikao cha leo ni Kikao cha Nane, Katibu.

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:**

#### HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

**SPIKA:** Hati za Kuwasilisha Mezani, naomba nimwite Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Namuona Naibu Waziri, Mheshimiwa Elias Kwandikwa.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu zilizokaguliwa za Mfuko wa Barabara kwa Mwaka 2015/2016 (*The Annual Report and Audited Report of Roads Fund Board for the year 2015/2016*).

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Sasa naomba nimuite Mwanasheria Mkoo wa Serikali, Mheshimiwa Prof. Kilangi tafadhalii.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:**

Maelezo ya Mwanasheria Mkoo wa Serikali kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 6) wa Mwaka 2019 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 6), Bill, 2019*].

**SPIKA:** Ahsante sana. Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, anakuja Mwenyekiti mwenyewe, Mheshimiwa Andrew Chenge. (*Makofii*)

**MHE. ANDREW J. CHENGE – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGЕ YA SHERIA NDOGO:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 6) wa Mwaka 2019 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 6), Bill, 2019*].

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati. Msemaji Mkoo wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni Kuhusu Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Cecilia Pareoso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO (K.n.y MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU WIZARA YA KATIBA NA SHERIA):**

Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 6) wa Mwaka 2019 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 6), Bill, 2019*].

**SPIKA:** Ahsante sana. Katibu.

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:**

**MASWALI KWA WAZIRI MKUU**

**SPIKA:** Maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Waziri Mkuu, karibu. (*Makofi*)

Ahsante sana. Muuliza swali wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Mlalo, Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi. Mheshimiwa Shangazi tafadhali.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi hii.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Serikali ya Awamu ya Tano imehamasisha sana shughuli za kilimo na wananchi wamehamasika sana, lakini hivi karibuni limetokea tatizo kubwa sana la ufungaji wa mazao kwa mtindo wa lumbesa lakini pia kuwepo na vifungashio ambavyo havina viwango stahiki. Jambo la kusikitisha sana ni kwamba Mamlaka za Serikali, hasa Wakala wa Vipimo na Mizani, pia Serikali katika ngazi za Halmashauri, Wilaya na Mikoa zimeshindwa kabisa kudhibiti tatizo hili la ufungaji wa mazao kwa mtindo wa lumbesa. Je, Serikali ipo tayari kuanzisha operesheni maalum nchi nzima kudhibiti tatizo hili ambalo kwa kweli linawanyong'onyeza wakulima na kuwaletea lindi la umaskini? (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri Mkuu tafadhali.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Shangazi, Mbunge wa Mlalo kule Lushoto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Serikali imeendelea kusisitiza wakulima wetu nchini wanapolima mazao yao waweze kunufaika kutokana na masoko yaliyo sahihi. Tunaanza kuona baadhi ya wanunuzi kutofuata sheria,

kanuni na taratibu za manunuzi ya mazao hayo pindi wanapokwenda kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, nimefanya ziara Wilaya ya Karatu eneo maarufu linalozalisha mazao la *Lake Eyasi*, eneo la Eyasi kule chini. Moja kati ya malalamiko ambayo wakulima waliyatoa ni kama ambavyo Mheshimiwa Shangazi ameeleza, lakini Serikali imeweka utaratibu wa mazao yote yanayolimwa na kuingia kwenye masoko, lazima masoko hayo yatumie vipimo halisi ili liweze kulipa bei stahiki na mkulima aweze kunufaika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tunaposema vipimo stahiki maana yake kuna vipimo ambavyo tunavitumia, inaweza kuwa ni kipimo cha ndoo ambazo tunajua kuna ndoo za lita tano, kumi, ishirini, na ni rahisi pia kukadiria na bei ambayo inawekwa na wakulima inakuwa ndiyo bei sahihi. Pia kuna vifungashio kama vile magunia ya kilo hamsini, kilo mia, nayo pia ni sehemu ya vipimo halisi lakini muhimu zaidi ni kutumia mizani ambayo haina utata.

Mheshimiwa Spika, sasa imetokea wanunuzi kuwalazimisha wakulima baada ya kile kipimo halisi kuongeza tena nundu inayojulikana kwa jina la lumbesa kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge ameeleza, hii haikubaliki. Tumetoa maelekezo sahihi kwa Wakuu wa Mikoa wote, Wakuu wa Wilaya wote, Wakurugenzi na Maafisa Kilimo na Maafisa Ushirika wanaosimamia masoko kwenye ngazi hizo za wakulima wawe wasimamizi wa biashara inayofanywa na wanunuzi kwa mkulima pindi anapouza mazao yake ili kujiridhisha kwamba vipimo vyote vinatumika na siyo kuongeza nundu zaidi ya kipimo ambacho kinatakiwa, kwa sababu kufanya hivyo tunamnyonya mkulima na mkulima anapata hasara kwenye mazao hayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo utayari wa Serikali upo na tumeshatoa maelekezo kwa Wakuu wa Wilaya. Kwa hiyo nirudie tena kutoa wito kwa Maafisa Kilimo, Ushirika, Wakuu Wa Wilaya, Wakuu wa Mikoa kwenye maeneo yao

wasimamie biashara hii na kuendesha operesheni kwenye maeneo yote ya masoko ili kujiridhisha kwamba mazao yetu yananunuliwa kwa vipimo kama ambavyo vimekubalika. Huo ndiyo msisitizo wa Serikali na tutaendelea kusisitiza wakati wote. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana, tunaendelea. Mheshimiwa Mariam Nasoro Kisangi, uliza swali lako.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kunipa nafasi nami niweze kuuliza swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, katika miezi ya karibuni katika Mikoa mbalimbali ya nchi yetu kumekuwa na changamoto kubwa ya kupanda kwa gharama za maji bila kuzingatia uasilia, kuletewa bili zisizo sahihi, kukatiwa maji bila utaratibu na kukosa maji kwa muda mrefu kisha unaletewa bili kubwa. Kero hiyo imejitokeza katika Mikoa mbalimbali katika nchi yetu ikiwemo Mikoa ya Dar es Salaam, Manyara, Dodoma, Tanga, Mwanza na Mikoa mingine minge na hasa katika maeneo ya Mijini.

Je, Serikali inatoa kauli gani kwa wananchi wake waliokumbwa na kero hiyo?

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu majibu kwa swali hilo tafadhali.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Kisangi, Mbunge wa Mkoa wa Dar es Salaam, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, alichosema Mheshimiwa Mbunge, yako maeneo yanajitokeza kwamba mamlaka tulizopita mamlaka hiyo ya kusimamia maji kwenye maeneo yao, tunazo mamlaka ambazo tunazianzisha sasa za RUWA za vijijini na kwenye ngazi za Wilaya, lakini zipo mamlaka ambazo zimechukua maeneo makubwa kwenye ngazi za

Mikoa, pia tuna Kamati za Maji ambazo zinasimamia miradi hii kwenye maeneo ya vijiji na maeneo mengine yote.

Mheshimiwa Spika, kumejitokeza wimbi la mabadiliko ya bei. Ni kweli upo utaratibu ndani ya Serikali kwamba mamlaka hizo zinapoona zinahitaji kuboresha huduma zinaweza kufanya mapitio ya bei zao. Lakini kinachotokea sasa ni kwamba zipo mamlaka zinapita zaidi ya kiasi.

Mheshimiwa Spika, nimefanya ziara Mkoani Simiyu na hapa karibuni nilikuwa kwenye Wilaya ya Maswa, moja kati ya malalamiko niliyoyapokea kwa wananchi pale ni kupanda kwa bei kutoka shilingi 5,000 wanayoilipa kwa mwezi mpaka shilingi 28,000. Sasa bei hizi hazina uhalisia, hakuna sababu ya mamlaka kutoza fedha yote hiyo na kuwafanya wananchi wakose maji.

Mheshimiwa Spika, Serikali ndiyo inatekeleza hii miradi na inatoa fedha kwa lengo la kuwapa huduma wananchi ili wapate huduma ya maji. Mamlaka tumewapa jukumu la kusimamia mradi huo na kuhakikisha kwamba angalau wanaweza kufanya marekebisho, matengenezo pale ambapo kunatokea uharibifu. Kwa hiyo, gharama haziwezi kuwa kubwa kiasi hicho na wala wao hawapaswi kutoza wananchi ili kurudisha gharama za mradi kwa sababu Serikali hajadai gharama ya kuendesha mradi huo kwa wananchi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa bahati nzuri jana nilikuwa na Waziri wa Maji nikimwambia hili la kwamba lazima afuatilie Mamlaka ya *EWURA* ambayo ina mamlaka ya kukaa na hizo mamlaka zetu za maji kufanya mapitio ya bei. Bei zinazotakiwa kuwekwa ni zile ambazo mwananchi wa kule kijijini anaweza kuzimudu lakini siyo kwa kupandisha bei kutoka shilingi 5,000 mpaka shilingi 28,000, jambo ambalo halina uhalisia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wote na Watanzania kwa ujumla, tutaendelea kusimamia Mamlaka

zote za Maji, lakini Serikali itaendelea kutoa huduma za maji, nataka tujiridhishe kila Mtanzania anapata maji kwenye maeneo yake kwa usimamizi wa mamlaka hizi, lakini hatutaruhusu na hatutakubali kuona Mtanzania anatozwa ghamama kubwa za maji kiasi hicho. Huku tukiwa tunatoa wito kwamba lazima tuchangie maji ili tuweze kuendesha miradi hii pale ambapo tunatakiwa kununua *diesel*, tunatakiwa tununue tepu ya kufungulia maji au bomba linapopasuka, lazima mamlaka zile ziweze kufanya ukarabati huo, lakini siyo kwa kutoza fedha kiasi hicho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, masharti ambayo yapo mnapotaka kuongeza bei ni kwamba mamlaka hizo zinapodhamiria jambo hilo ni lazima kwanza zitoe taarifa *EWURA*, mbili kwenye vikao hivyo lazima Kamati za Maji zihusike, Kamati ambazo zinaundwa na wananchi wenyewe, tatu ni lazima wahusise wadau, wadau ni wale watumia maji. Kwa hiyo, wote wakikubaliana sasa kwa viwango ambavyo wananchi wake wanaweza kuvimudu ndipo mnaweza kupandisha. Lakini msipandishe wenyewe na mkawaumiza wananchi na miradi yenye imetekelezwa na Serikali, Serikali inayotaka wananchi wapate maji halafu mnataka kuwakwaza wananchi wasipate maji waanze kuilalamikia Serikali yao. Hatutakubaliana na hili na kwa hiyo mamlaka ziwe makini, Wizara ya Maji iendelee na utaratibu na maagizo ambayo nimewapa jana.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunisikiliza. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana, tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu hii ni kero kwelikweli hii, mtu alikuwa analipa bili ya Sh.10,000 leo analetewa bili ya Sh.80,000, nyumba ileile watu walewale, wanaigana nchi nzima wamepandisha hasa; tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Mbunge wa Babati Vijijini, Mheshimiwa Jitu Vrajlal Soni, uliza swali lako.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali kwa Waziri Mkuu siku ya leo.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwanza niipongeze Serikali kwa jitihada kubwa na ya dhati kabisa ya kusaidia na kuhakikisha kwamba uzalishaji wa mazao mbalimbali nchini unakua, wakulima wameweza kuzalisha tena kwa viwango vyatuu na mazao sasa tumeona kukua kwa uzalishaji, sasa changamoto kubwa imekuwa jambo la masoko. Niipongeze pia Serikali kwa kuweka mifumo mbalimbali kuhakikisha kwamba mazao ya wakulima yanapata bei sahihi...

**SPIKA:** Sasa twende kwenye swali.

**MHE. JITU V. SONI:** Naomba kuuliza je, kwa hivi karibuni kumetokea mkanganyiko wa kauli na nyaraka mbalimbali zinazotoka kutoka Taasisi mbalimbali za Serikali kwa mfano *TMX*, Ushirika, *AMCOS* na pia Bodi ya Mazao Mchanganyiko kuhusu mfumo wa ununuzi wa mazao hayo. Mkanganyiko huo sasa umefanya maeneo mengi mifumo hii ishindwe kufanya kazi vizuri na wakulima sasa waweze kukosa bei stahiki wanayoweza kupata. Tunaomba kujua kauli ya Serikali ni nini kuhusu mkanganyiko huu ambao umejitokeza ili maeneo yote kwa kila Mkoa mifumo hii sasa iweze kukaa vizuri na wakulima waweze kufaidi matunda...

**SPIKA:** Unajua Mheshimiwa Jitu hujauliza swali mpaka sasa hivi?

**MHE. JITU V. SONI:** Kuna mkanganyiko mkubwa uliojitokeza...

**SPIKA:** Yaani jaribu kuokoa muda kwa kueleza huo mkanganyiko ni mkanganyiko gani ili uweze kupata majibu.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu mifumo ya kununua, kauli tofauti baina ya Taasisi mbalimbali za Kiserikali kwa mfano *TMX* na Ushirika kulazimisha kununua

mazao kwa kupitia mfumo huo badala ya mfumo uliokuwepo, kwa hiyo kuna maeneo ambapo hii mifumo...

**SPIKA:** Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, swali linalofuata.

Mheshimiwa Jitu Soni utanisamehe, hata Wabunge wenzako hawajaelewa unachotaka kuuliza, utajipanga siku nyingine. Ndiyo Mheshimiwa Msongozi.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuuliza swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Serikali imeweka mkazo mkubwa katika kuboresha mazingira ya uwekezaji nchini Tanzania, licha ya jithada hizo kuna baadhi ya Maafisa wanakwamisha wawekezaji. Je, Serikali inatoa kauli gani kwa Watendaji wa aina hii?

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Unaweza ukajaribu kutoa hata kamfano kidogo Mheshimiwa Jacqueline, maana yupo Waziri wa Uwekezaji naye ajifunze ni ukwamishaji gani unaotokea?

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Wawekezaji wanapokuja nchini unakuta labda kwa mfano anakwenda katika Mkoa wa Mwanza anataka aweke kiwanda cha usindikaji wa samaki lakini unakuta kwenye, labda Sekta ya Ardhi au kwenye Halmashauri zetu katika sekta mbalimbali wanakuwa wanaweka vikwazo mbalimbali labda kutengeneza mazingira labda ya rushwa na mambo kadha wa kadha. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante. Sasa umeelewa Mheshimiwa, Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri Mkuu tafadhali.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Msongozi, Mbunge kutoka Mkoa wa Ruvuma, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu kwa sasa tumeweka utaratibu mzuri sana wa uwekezaji na tunaendelea kuhamasisha uwekezaji nchini wa ndani na nje ya nchi. Natambua kwamba tulipoanza kutoa wito wa uwekezaji kwa yejote mwenye nia ya kuwekeza hapa nchini tulianza katika mapito mbalimbali, watendaji, wengine walikuwa hawajajua *philosophy* ya Serikali, lakini pia maeneo muhimu ya uwekezaji bado ilikuwa hayajachanganuliwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Tano imeweka utaratibu mzuri sana, kwanza kwa kuunda Wizara ya Uwekezaji ambayo sasa itashikilia Sera ya Uwekezaji kwa ujumla, pia Serikali ina chombo kinachoshughulikia uwekezaji, Taasisi ya Uwekezaji Tanzania (*TIC*) ambayo sasa tumerahisisha mambo yote ya uwekezaji yako hapo ndani, anayetaka ardhi anapata huko ndani, anayetaka huduma za *TRA* anakuta huko ndani, usajili wa kampuni anakuta huko. Sekta zote zinazogusa uwekezaji sasa zinapatikana pale *TIC* kwa maana tumeanzisha *One Stop Center* ambayo kila mwekezaji anapokuja shughuli zote zinaishia hapo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia tumeleta mamlaka kwenye ngazi za Mikoa na Halmashauri kupokea Wawekezaji wenye nia ya kuwekeza kwenye ngazi hizo na Mikoa sasa itawezesha kuhakikisha kwamba mwekezaji huyo anapata huduma ya uwekezaji na atapata maelekezo sahihi. Yako mambo yanawezeshwa hukohuko kwenye ngazi ya Halmashauri au ngazi ya Mkoa lakini mengine lazima yaende *TIC* na mengine lazima yaende Wizarani kukutana na Waziri kwa ajili ya Sera ya ujumla.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kwa utaratibu huu kama bado kuna mtendaji anakwamisha uwekezaji huyu atakuwa hana nia njema na nchi yetu. Na popote ambako wananchi, Waheshimiwa Wabunge unaona kuna Mtendaji wa Serikali

tumempa jukumu la kusimamia shughuli za Serikali ikiwemo na uwekezaji, uwekezajia ambao sasa kila siku tunatoa wito watu wawekeze, tena wawekezaji wa ndani na wa nje ya nchi na anakwamisha *process* hiyo hatua kali dhidi yake zitachukuliwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, bado Serikali inatoa wito wa uwekezaji. Tumerahisisha uwekezaji kwa sababu pia tumekuwa na vikao na makundi mbalimbali ya wafanyabiashara, wawekezaji. Mheshimiwa Rais amekutana na wafanyabiashara wengi, wawekezaji wengi na sisi watendaji huku chini tumekutana na makundi hayo mbalimbali tukapata kero zinazowagusa hao wafanyabiashara.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tumeandaa mfumo tumetengeneza ile *blueprint* kile kitabu ambacho kinaonesha mabadiliko ya mifumo mbalimbali ya uwekezaji ambayo yanarahisisha uwekezaji hapa nchini kuwa uwekezaji rahisi zaidi. Ndiyo kwa sababu sasa unaona idadi ya wawekezaji nchini inaongezeka na tunaendelea kupokea kero za wawekezaji ili tuendelee kuboresha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niendelee kutoa wito kwa wawekezaji wote wasihofu kuja nchini tuna ardhi, tunazo maliasili lakini tuna rasilimali za kuendeshea kilimo uwekezaji huo kama ni viwanda au tukitaka kuchakata madini, tunayo. Muhimu zaidi ni kufuata sheria, kanuni na utaratibu wa ndani ya nchi ili uweze kuwekeza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niseme tu kwamba tumesikia, tumepata ujumbe wako ndani ya Serikali tutaendelea kusimamia vizuri kwa watendaji ambao hawaelewi bado *philosophy* ya Serikali na malengo ya nchi kwa ajili ya kuleta uwekezaji ulio sahihi na bora. Mazingira ya uwekezaji kwa sasa tumerahisisha na tutaendelea kurahisisha zaidi.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunashukuru kwa majibu hayo mazuri sana. Tukumbushe tu kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu mlikuwa mmetuahidi kwamba Bunge hili tungeletewa sheria inayohusiana na masuala ya *blueprint*. Kwa kuwa Bunge hili haijaja tunatumaini kwa vyovyyote vile basi Bunge Iijalo Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji msiingie mitini tena. Bunge Iijalo mtuletee ili iendane na ahadi ya ambazo Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Rais wamekuwa wakizitoa. (*Makofii*)

Twende Visiwani sasa, Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu katika ziara anazofanya Tanzania na tumeshuhudia nyingi katika ziara zake changamoto nyingi za wapiga kura wetu akizitatua hapo kwa hapo bila kulala. Pongezi sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu ukumbuke tu bado Visiwani hujafika ikiwemo Tanzania nayo Zanzibar imo, Unguja na Pemba na naamini huna muda mrefu utafika.

Mheshimiwa Spika, kati ya mambo ya Muungano ni suala elimu ya juu, lipo Kikatiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Suala hili tumeshuhudia hivi majuzi Waziri wa Elimu Mheshimiwa Ndlichako akisindikiza wanafunzi karibu 100 kwenda China. Kwanza naomba ku-*declare interest* ni mjumbe wa Kamati hii na kauli za ndani katika Kamati hii sikupata jawabu na hatimaye mmelileta hapa leo wananchi waliskie na walione.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jaku swali sasa.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Spika, swali, huko nyuma kulikuwa kuna utaratibu wa kugawa nafasi hizi

ambapo kwa kisheria juu ya udogo wake Zanzibar. Je, ni lini Mheshimiwa Waziri utaagiza tena utaratibu huo urudi ili Wazanzibar katika nafasi hizi za *scholarship* wawemo?

**SPIKA:** Kwani kwa utatifi wako Mheshimiwa Jaku katika 100 hakuwepo hata mmoja au ilikuwaje?

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Spika, bila shaka niliwaambia katika Kamati na jibu halikupatikana ikiwa kigugumizi kitupu, wanakonyezana hivi na hivi tu.

**SPIKA:** Umesema!

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Spika, kwa ufupi jawabu halikupatikana, hamna maana yake. Kwa hiyo nillichoklomba ule utaratibu wa zamani na hili suala liko Kikatiba ya Muungano wa Elimu ya Juu na zamani kuilikuwa utaratibu wa ...

**SPIKA:** Maana yake swalii hili lingekuwa na maana kwanza kama tungkuwa na hakika, yaani ungekuwa umefanya utafiti wa hakika kwamba katika hao 100, wazanzibar ni wangapi, kwa hiyo, nafazi zake chache kuliko zinavyostahili. Sasa kwa kuwa haina uhakika...

**JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Spika, aaa, hapana hapana.

**SPIKA:** Mtamfanya Waziri Mkuu ajibu swalii ambalo halina hakika.

**JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Spika, uhakika hamna, mimi sijawahi kulewa wala kuvuta bangi, hamna hata mjumbe mmoja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati, au Makamu wa Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma. Tupeni kwa harakaharaka ninyi utafiti wenu ndani ya Kamati mliona uwiano ukoje. Kama Mwenyekiti hayupo Makamu upo,

Mheshimiwa Nkamia. Maana yake anasema mlikuwa nalo kwenye kamati.

**MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA ZA JAMII:** Mheshimiwa Spika, hili jambo analolisema Mheshimiwa Jaku, siyo jambo la kukurupuka, linahitaji utafiti wa kina na kuwa na uhakika na kile anachokizungumza. Nikuombe utuachie turudi kwenye kamati ili alete hiyo hoja yake tufanyie utafiti. Ahsante.

**SPIKA:** Nashukuru sana, ni vizuri kutafiti, haya mambo yanayohusu muungano na nini ni vizuri kutafiti, kuja na kitu ambacho tayari, vinginevyo tutakuwa tunamtaka Waziri Mkuu ajibu vitu ambavyo havina...

Mheshimiwa Senator Richard Mganga Ndassa.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana kwa nafasi hii ya kumuuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Waziri Mkuu najua unajua kwamba kwenye msimu huu unaoendelea wa pamba, zao hili limekumbwa na kadhia mbalimbali. Ningependa kujua changamoto hizi, ya kwanza, tani elfu 35 zilizochukuliwa na wanunuzi na wakulima wakakopwa, tani 52 elfu ambazo ziko maghalani kupitia *AMCOS*, ambazo pia wakulima wamekopwa hawajalipwa, tani elfu 70 zinazokisiwa, ambazo ziko majumbani bado hazijapelekwa kwenye soko.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu tungependa kujua, nini kauli ya Serikali au tamko la Serikali kuhusu wakulima wa zao la pamba ambao pamba yao iko majumbani lakini wamekopwa mpaka sasa hivi hawajalipwa? Nini kauli ya Serikali? (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana, majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri Mkuu tafadhalii.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika naomba kujibu swali la Mheshimiwa *Senator Ndassa* kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala la pamba Serikali tumelifanyia kazi kweli kweli na kwa bahati sasa pamba inalimwa kwenye mikoa zaidi ya 11 nchini na uzalishaji tunafurahi sana kwamba umeongezeka kutoka tani 220,000 mwaka uliopita na msimu huu tumekwenda mpaka tani 300,000, tunategemea kupata tani zaidi ya 350,000.

Mheshimiwa Spika, lakini Serikali imeendelea kusikia malalamiko ya baadhi ya wakulima kwamba pamba hainunuliwi ni kweli, na sisi tumepita, mimi mwenyewe nimepita, Mawaziri wa Kilimo, Waziri mwenyewe, Manaibu wake wamepita maeneo yote kuona hali hiyo lakini na kuzungumza pia na wananchi kwenye maeneo hayo. Tumekuwa na vikao vya wadau, wadau wanaohusika ni wakulima, wanunuzi, wafanyabiashara na kwa maana ya wanunuzi, watu wa mabenki pamoja na viongozi wa Serikali wa maeneo hayo ili kuona njia sahihi ya kuondoa pamba yote mikononi mwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, nafurahi kusema kwamba, utaratibu ambao tumeuweka wiki tatu zilizopita umeanza kuleta matunda kwamba sasa ununuzi wa pamba tumeshafikia asilimia kama 80 hivi, kwa sababu tumeshanunua tani, mpaka juzi, tani ambazo tumeshanunua ni tani 235,000. Kwa hiyo, pamba ambayo bado iko ni kidogo na kwa hiyo tunaamini kwamba pamba hii yote tutaichukua.

Mheshimiwa Spika, utaratibu tuliuweka kuwashakikisha wakulima kwamba pamba hii tutaichukua, ni kwamba baada ya kuchanganua pamba iliyobaki kwa wakulima tumeigawa kwa wanunuzi maalum ambao wana uhakika wa kuinunua pamba hiyo kwa *kilograms* zao na tumeshafika mpaka *kilograms* zote mpaka laki tatu, kila mmoja ana mgao huo na Benki Kuu kuitia mabenki, wanunuzi wale wanapewa fedha za kwenda kuchukua pamba yote mikononi mwa wakulima na zoezi la kuwapa fedha hizo linaendelea na wanunuzi wanakwenda sasa kuchukua pamba.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tuna uhakika katika kipindi kifupi kijacho pamba yote itatoka mikononi mwa wakulima na itabaki mikononi mwa wanunuzi ili utaratibu wa kwenda kufanya mauzo uendelee. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa bahati nzuri sana juzi tulikuwa na kikao cha pamoja kati ya Benki Kuu, Mabenki na Wawakilishi wa wanunuzi na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge ambao pia walipata fursa ya kuingia pale kwenda kusikia mpango mkakati wa kumaliza pamba yote kule kwa wananchi. Kwa hiyo, niendelee kuwahakikishia wanunuzi wa pamba kuititia Waheshimiwa Wabunge ambao mnatoka kwenye mikoa ile yote kwamba, pamba yote itachukuliwa kwa sababu mpango wa fedha kuwapatia wanunuzi, wanunuzi wakachukue pamba unaendelea na pia tumewashirikisha Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa kwa kuwaambia wilaya yako inanunuliwa na fulani na mnunuzi huyo atachukua kilo kadhaa kwenye eneo hilo na tumeshampa fedha, kwa hiyo, kazi pale ni kushirikiana naye kwenda kuichukua pamba yote ili iweze kuondoka mikononi mwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka niwahakikishie kuititia Mheshimiwa Mbunge aliyeuliza swali Mheshimiwa Ndassa ambaye pia ni mwakilishi wa wakulima wa pamba kule Kwimba, kwamba pamba yote ambayo tumeizalisha hii, tutaitoa sasa wakati huu tunafikiria kwamba hali ya hewa inaweza kubadilika wakati wowote ili isiweze kunyeshewa na mvua, tuwahakikishie kwamba pamba yote imetoka mikononi mwa wakulima. Ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu ahsante sana, Mheshimiwa Mbunge wa Monduli, Mheshimiwa Julius Kalanga Laizer, uliza swali lako tafadhalii!

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimia Spika, nakushukuru. Mwaka huu maeneo mengi ya nchi yetu yamekabiliwa na upungufu wa mvua ambayo imepelekea maeneo mengi

kukosa chakula cha uhakika na hivyo kusababisha bei ya chakula kupanda kwa kiasi kikubwa sana. Hapa tunapozungumza maeneo mengi mahindi yanauzwa kuanzia shilingi elfu 80 mpaka laki moja.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, je, nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba chakula cha bei nafuu kutoka *NFRA* kinapelekwa katika maeneo haya yaliyokumbwa na ukame ili wananchi waweze kumudu chakula? (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu tafadhali.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Kalanga, Mbunge wa Monduli kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa chakula nchini kwa maana usalama wa chakula nchini kufuatia msimu uliopita wa uvunaji wa mazoa ya chakula uko vizuri, lakini tunatambua kwamba yako maeneo kadhaa hali ya hewa haikuwa nzuri na uzalishaji wake haukuwa mzuri sana. Kwa hiyo, maeneo hayo yanaweza kuathirika kwa kuwa na bei zisizotabirika wakati wote na kusababisha wananchi kutojua hasa bei ya mahindi, chakula hicho, lakini pia ni wapi tunaweza kupata chakula hicho.

Mheshimiwa Spika, lakini nataka niwahakikishie kwamba uzalishaji wa chakula ambaa umefanywa, ambaa Wizara ya Kilimo imeweeka utaratibu wa kuhakikisha kwamba maeneo yote yanapata chakula, *NFRA* imepewa jukumu la kuhakikisha kwamba usalama wa chakula nchini unaimarishwa kwa kuwa na chakula cha akiba kwenye maghala ili kiweze kutolewa na kuuzwa kwenye maeneo ambayo hayana chakula kwa sasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini pili, kwa kuwa chakula kiko nchini na tunao wafanyabiashara ndani ya nchi, hiyo ni fusa muhimu kwao ya kupata chakula kukipeleka maeneo

ambayo hayana chakula. Mheshimiwa Kalanga amezungumzia bei nafuu, bei nafuu sasa ni tumeruhusi wanunuzi mbalimbali kuingia kununua. Wanapokuwa wanunuzi wengi kunakuwa na ushindani wa ununuzi, ingawa pia bei inakuwa iko juu lakini sisi kwa sababu tuna *NFRA* ambayo inashughulikia usalama wa chakula, basi chakula huwa kinapatikana. Kwa hiyo, muhimu zaidi tupate taarifa, wapi kuna upungufu wa chakula, halafu tuone, tuweze kupeleka chakula ambacho tunaweza kununua kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Spika, lakini muhimu zaidi ni ule msisitizo wa kila mmoja afanye kazi na tumeanza kuona matunda kwamba chakula sasa uzalishaji ni mkubwa mpaka tunakua na ziada hapa nchini na chakula kingine tunauza pia hata nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Iakini mbili, ni hilo ambalo tumelisema la kwamba wanunuzi sasa wapite maeneo hayo waweze kuchukua mahindi kutoka eneo moja kupeleka eneo la pili ili wananchi wa maeneo hayo waweze kupata huduma.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kupitia Mheshimiwa Kalanga *NFRA* inaweza ikipata taarifa na Wizara ya Kilimo inasikia hapa ni rahisi sasa kuweza kushughulikia maeneo hayo yanayokosa chakula. Kwa hiyo, kwa taarifa ambayo tumeipata sasa naamini tutaishughulikia ili kuona namna nzuri ya kufikisha chakula ambacho tunaweza kukinunua kwa bei nafuu. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mbunge wa Jimbo la Temeke Mheshimiwa Abdallah Ally Mtolea, tafadhali uliza swali lako!

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nimuulize swali Mheshimiwa Waziri Mkuu. Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli imekuwa ikitoa fursa nydingi kwa ajili ya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu kupitia

10% za halmashauri lakini kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, Vijana, Kazi na Ajira. Anapotamkwa kijana anamaanishwa mtanzania mwenye umri kati ya miaka 18 hadi 35 tu. Hii siyo changamoto kwa wanawake kwa sababu kama amepindukia miaka 35 na ni kijana anaweza kuipata fursa hiyo kupitia mlango mwingine wa kundi la wanawake, lakini kwa wanaume anakuwa ameishia hapo.

Mheshimiwa Spika, katika maisha yetu ya kawaida wanaume wenyewe umri kati ya miaka 35 kwenda 40 ndiyo wenyewe mahitaji makubwa wa hizi fursa ambazo zinatolewa na Serikali. Nilitaka kujua kama Serikali inalionia hili na kama ina mpango wowote wa kupanua ukomo wa umri kutoka miaka 35 kwenda angalau miaka 40 ili wanaume wengi na wenyewe waweze kunufaika na fursa hizi? (*Makof*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Mtalea lengo si ni vijana, kwa hiyo unataka kusema umri wa vijana sasa uwe miaka 40! Hoja yako ni nini?

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Spika, hoja yangu ni kwamba kwenye maisha ya kitanzania watu ambao wako kati ya umri wa miaka 18 – 35 unapotaka kuwaingiza kwenye fursa hizi za mikopo unachukua kundi dogo sana la watu labda wenyewe miaka 33 – 35 tu. Hao wengine wanakuwa wako vyuoni, wako shulenii nabado hawaajaanza maisha, wanaoanza maisha kwenye maisha yetu haya hasa kwa wanaume ni kati ya miaka hiyo 35 kuja 40 hapa ndiyo kuna kundi kubwa la watu wenyewe mahitaji kwa wanaume. (*Makof*)

**SPIKA:** Kwa hiyo utaitaje, maana sheria hii imesema vijana, swalii lako lina base wapi?

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Spika, swalii langu saa kwa sababu hiyo sheria inayotumika ni ile ya kimataifa ya kundi la vijana, sisi tunapokwenda kwenye fursa twende na uhalsia.

**SPIKA:** Ni sheria tumetunga hapa hapa Bungeni na wewe ukiwepo. (*Kicheko*)

Ni sera ya kimataifa.....

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Ni kweli lakinini tunapokwenda kwenye sera ya kimataifa kwa sababu fursa ni suala la kisera, tuangalia uhalisia watu gani tunawalenga na tunataka kuwasaidia. Ndiyo kundi hilo la miaka 35 kwenda 40.

**SPIKA:** Bahati mbaya huna swali Mheshimiwa, leo imekuwa bahati mbaya sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu tunakushukuru sana nusu saa imeisha, ahsante sana. (*Makof*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. (*Makof*)

**SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, ahsante sana. Wauliza maswali wa leo wamepata nafasi isipokuwa Mheshimiwa Issa Mangungu siku nyingine na wewe utapata nafasi hamna shida. Waheshimiwa katika kuuliza maswali ni vizuri tukajipanga kwa Waziri Mkuu. Maswali yanayotakiwa hapa ni maswali ya kisera, ukimuuiliza swali Waziri Mkuu la kupinga sheria ambayo tumetunga sisi wenyewe sasa unataka ye ye ajibu nini. Sheria inasema vijana na vijana ndiyo hao na hilo kundi la vijana ni vijana wengi kweli, wengi kweli.

Mnajua ile *population graph* ya Tanzania ilivyo, ilivyo pana huku chini, pana sana. Hii ni vijana kuanzia wanaomaliza darasa la saba, darasa la saba wanamaliza wakiwa na miaka mingapi, kumi na nne, kumi na tano hata kama amechelewa ana miaka 20. Mpaka afike 35 bado ana miaka 15 ya kuweza kuwa *supported*, hilo ni kundi kubwa sana la wanaomaliza *form four* ni kundi kubwa mno. Useme sasa waongeze mpaka wa miaka 40 cjui ngapi, kwa nini wameweka 45 wasiongezeke, kwa nini wa miaka 50 nao wasiongezeke, utafika mahali utajikuta hata lengo lako halieleweki.

Pia, hili jambo japo tulitunga sheria unatakiwa kuliangalia Mheshimiwa Mtolea. Kwa mfano, Dodoma hapa

Manispaa hii katika makusanya ndiyo ya kwanza, inakusanya karibu bilioni sabini na, mapato ya ndani, bilioni sabini. 10% ni bilioni saba, bilioni saba unagawagawa hivi, unagawagawa hivi. Wakati mwingine mtu unawaza hizi bilioni saba zingewekezwa kwenye kitu fulani, isingekuwa ni *more profitable* kuliko kusambaza sambaza hivi tunavyofanya. (*Makofi*)

Hata nyie Temeke mnakusanya fedha nyingi sana ambazo wakati mwingine mngeweza kuziwekeza kwenye kitu fulani ikiwa na matokeo makubwa zaidi kuliko hii tunayofanya, ni mawazo tu.

Mheshimiwa Jaku pia, swali lako linahusu tukio na tunatakiwa tumuulize Mheshimiwa Waziri Mkuu maswali yanayohusu sera. Matukio yanaweza kuwa sera endapo matukio yamejirudia rudia mara tatu, mara nne, mara tano. Lakini likiwa ni tukio kama hilo la watoto kwenda China na bahati nzuri wewe ni mjumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii ambako mnakutana na Mheshimiwa Waziri mara kwa mara mngeweza kuulizana. Ukija kumuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhusu tukio la namna hiyo hana takwimu, hana *data*, hana nini ni ngumu sana kuweza kulijibu swali la aina hiyo. Kwa hiyo, natumaini huko mbele Waheshimiwa tutajitahidi kujikita zaidi katika mambo yanayohusu sera kwa ujumla wake na utekelezaji wa sera.

Katibu!

#### **NDG. STEPHEN KAGAIGAI-KATIBU WA BUNGE:-**

#### **MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Maswali ya kawaida, Mbunge wa kwanza kuuliza atakuwa Mheshimiwa Mbunge wa Bumbwini Mheshimiwa Mohammed Amour Mohammed, Uliza swali lako Mheshimiwa tafadhali.

Na. 99

**Kuzisaidia Taasisi Zinazoshughulikia Watu  
Wenye Ulemavu**

**MHE. MOHAMMED AMOUR MOHAMMED** aliuliza:-

Idadi ya watu wenye ulemavu inakaribia asilimia kumi (10%) ya watanzania na idadi hiyo inatarajiwa kuongezeka kwa sababu mbalimbali.

Je, Serikali imejipanga vipi katika kuzisaidia na kuwezesha taasisi zinazoshughulikia watu wenye ulemavu nchini?

**SPIKA:** Ahsante, swali hilo linaelekezwa kwenye Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu majibu tafadhali, nani anajibu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE,  
KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, anajibu Mheshimiwa Naibu Waziri Mheshimiwa Ikupa kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**SPIKA:** Ok, ok ahsante Mheshimiwa Ikupa, tafadhali majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (WENYE  
ULEMAVU):** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Muhammed Amour Muhammed, Mbunge wa Bumbwini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sera ya Taifa ya Maendeleo na Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu ya mwaka 2004 na Sheria Na.9 ya mwaka 2010 ya Watu Wenye Ulemavu, Serikali inayo majukumu yafuatayo katika kuhakikisha taasisi inayoshughulikia watu wenye ulemavu zinatoa huduma stahiki. Kwanza ni kuzijengea uwezo taasisi

zinazoshughulikia watu wenyewe ulemavu kwa kuzipa mafunzo ya namna ya kuwahudumia watu wenyewe ulemavu.

Mheshimiwa Spika, Taasisi hizo ni vyama vyaya watu wenyewe ulemavu ikiwemo Chama cha Watu Wenye Ulemavu wa Viungo, Chama cha Viziwi Tanzania, Chama cha Wasiona Tanzania, Chama cha Wenye Vichwa Vikubwa na Mgongo Wazi, Chama cha Viziwi Wasiona, Chama cha Watu Wenye Ugonjwa wa Akili, Chama cha Walioumia Uti wa Mgongo na Chama cha Watu Wenye Ulemavu wa Akili pamoja na Chama cha Watu Wenye Ulemavu wa Ngozi.

Mheshimiwa Spika, pia tunatoa miongozo kwa jamii na sekta zote kuhusu Sera, Sheria, Kanuni na Mikataba ya Kimataifa inayohusu watu wenyewe ulemavu katika kuleta haki na usawa wao. Kuzitambua na kuzitembea na kuzipa ushauri wa kitaalam taasisi nillizozitaja hapo juu namna ya kuwahudumia watu wenyewe ulemavu kulingana na aina ya ulemavu na mahitaji yao. Vile vile kuziwezesha taasisi mbalimbali za watu wenyewe ulemavu, upatikanaji wa nyenzo za kujimudu kwa ajili ya kuwahudumia watu wenyewe ulemavu pale inapolazimu kufanya hivyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Muhammed, muuliza swali nimekuona.

**MHE. MUHAMMED AMOUR MUHAMMED:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Serikali ambayo kwa kiasi fulani yanatoa mwangaza kidogo na yanaonesha matumaini katika maelezo sijui kwenye utendaji itakuwaje. Pia nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kulitamka jina langu kama vile ambavyo linatakiwa litamkwe, hakulikosea hiyo ndio asili ya jina Muhammed Amour Muhammed.

Mheshimiwa Spika, pamoja na yote hayo nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa tunategemea idadi ya watu wenyewe ulemavu kuongezeka nchi. Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka *ratio* ya uwazi kabisa katika kutoa ajira Serikalini kwa watu wenyewe ulemavu?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, watu wenye ulemavu nao ni watu kama wengine, wanasafiri wanaenda kwenye viwanja vyta michezo kama *football* na kadhalika tunawaona mara nyingine wanapata tabu bandarini pale, saa nyingine *airport* na mara nyingine kwenye vituo cha mabasi. Je, Serikali imejipangaje katika kuweka miundombinu wezeshi kwa watu wenye uleamavu katika maeneo kama yale? (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Ikupa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Muhammed Amour Muhammed, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Mbunge vile ambavyo anaafuatilia masuala haya ya watu wenye ulemavu. Ameulizia kuhusiana na *ratio* ni kwa jinsi gani Serikali ina weka *ratio* ya ajira kwa watu wenye ulemavu. Bunge letu Tukufu lilitunga Sheria Na.9 ya mwaka 2010, ndani sheria imeelezwa wazi kwamba watu wenye ulemavu ni kwa jinsi gani wanatakiwa kuajariwa. Mwajiri yoyote mwenye watu kuanzia 20 na kuendelea, basi 3% inatakiwa kuwa ni watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, kwa hili lipo wazi na niendelee kuwasihii na kuhawamasisha waajiri kwamba waweze kuitekeleza sheria hii kwa sababu sheria hii ya watu wenye ulemavu ni sawa na sheria zingine na pia inapobidi sheria itachukua mkondo wake wa yule ambaye atakuwa hatekelezi.

Mheshimiwa Spika, vile vile ameuliza ni kwa jinsi gani Serikali inahakikisha kwamba usafiri kwa watu wenye ulemavu unakuwa ni rafiki. Mimi mwenye nimefanya ziara katika maeneo kadhaa ikiwemo *airport*, lakini pia tumeendelea kusitiza na kuweka mkazo kuhakikisha kwamba miundombinu inakuwa rafiki. Katika *airport* kwa hapa nchini

tunahakikisha kwamba kunakuwa na *wheelchair* lakini kunakuwa na zile *ambulift* kwa ajili ya kubeba watu wenye ulemavu pamoja na wazee.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo pia kwenye maeneo ya usafiri wa umma ikiwemo huu usafiri wa kawaida hiyo ni changamoto ambayo nikiri wazi tunaendelea kuifanya kazi kwa kuendelea kuelekeza wamiliki wa vyombo hivi kuhakikisha kwamba miundombinu inakuwa ni rafiki kwa watu wenye ulemavu.

**SPIKA:** Jamani mkishamwona Mheshimiwa Amina Mollel amesimama, Mheshimiwa Ally Saleh amesimama. Mheshimiwa Ally Saleh swali la nyongeza, tafadhali.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri amezungumzia habari ya huduma stahiki na sasa hivi *mobility* ni huduma stahiki kwa watu wenye ulemavu. Swali langu linakuja kwamba, je, haoni ni wazo nzuri sasa kwamba Serikali itoe agizo kwamba katika *parking lots* katika *public spaces* kunakuwa na uhakika wa nafasi ya kuwekwa maalum kwa watu wenye ulemavu ambao aidha wanaendeshwa au wanaendesha wenyewe?

**SPIKA:** Nafasi za *parking*, Mheshimiwa Stella Ikupa majibu tafadhali, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza Mheshimiwa Ally Saleh kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, huu ni ushauri mzuri ambao tunapokea, lakini pia kama serikali tayari tumekwishaanza kufanya hivyo, hata tukienda kwenye *airport* mpya ambayo tumeijenga pale Dar es Salaam tumeona kabisa kuna *parking* maalum kwa ajili ya watu wenye ulemavu. Pia hata kama ukienda maeneo mengine hili limekuwa likifanyika, lakini tunapokea kama ushauri ili tuendelee kuhamasisha maeneo

mengine kuwa na *parking* maalum kwa ajili ya watu wenye ulemavu. Vile vile kwa Watanzania wote ambao wanansikia waweze kulitekeleza hili kuhakikisha kwamba *parking* za watu wenye ulemavu zinakuwepo. Kwa kweli inakuwa ni usumbufu mtu mwenye mwenye ulemavu akifika akikuta magari yamejaa anaanza kuhangaika na hasa akiwa anaendesha ye ye mwenyewe. Ahsante.

**SPIKA:** Swalii mwisho Mheshimiwa Amina Mollel, kwa kifupi.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pia nashukuru kwa majibu mazuri kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri. Hata hivyo, ningependa kufahamu tu kwamba, ni lini sasa Serikali itaanza kutoa ruzuku hasa kwa kutenga bajeti maalum kwa ajili ya Vyama vya Watu Wenye Ulemavu badala ya vyama hivyo kutegemea wafadhili. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Amina Mollel, pacha wangu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimewahi kujibu mara kadhaa ndani ya Bunge lako Tukufu, kama Serikali tukiwa tunaahidi Mfuko wa Watu Wenye Ulemavu utakapotengewa fedha ndipo ambapo hivi Vyama vya Watu Wenye Ulemavu vitawezeku patiwa ruzuku. Pia niliarifu Bunge lako Tukufu kwamba katika bajeti ya mwaka huu, fedha zimeweza kuwekwa kwenye Mfuko wa Watu Wenye Ulemavu na hivyo basi tunasubiri uzinduzi ufanyike, baada ya hapa ruzuku hizi za Vyama vya Watu Wenye Ulemavu zitaendelea kutolea.

Mheshimiwa Spika, pia nitoe wito kwa Vyama vya Watu Wenye Ulemavu kuwa wabunifu, kama ambavyo Mheshimiwa Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph

Magufuli ambapo ameendelea kusitiza jinsi gani ya vyama ama maeneo mbalimbali kuweza kujitegemea. Kwa hiyo pia niombe ubunifu kwa viongozi wa Vyama vya Watu Wenyewe Ulemavu ili kuwa na miradi na si kutegemea Serikali peke yake.

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge masuala haya yanayohusu wale mavu, tunapaswa wote tuwape kipaumbele cha hali ya juu, kwa sababu na sisi wenyewe tunaweza tukawa wale mavu wakati wowote. Haya ni mambo ya Mwenyezi Mungu tu. Tuna Wabunge waliwahi kuingia hapa wakiwa wazima, lakini leo ni wale mavu. Juzi tulipokuwa Zanzibar tulikuwa na Mbunge mmoja wa Kenya tunamfahamu vizuri, juzi nimekutana naye kwenye *wheelchair*na ni mlema *permanently*sasa hivi lakini ameingia Bungeni akiwa mzima kabisa. Kwa hiyo haya mambo tusiyaone kama yana watu fulani yanayohusu na wengine hatuhusiki, hapana, yanatuhusu wote kabisa kabisa. Tunaelekeea Ofisi ya Rais, TAMISEMI swalii la Mheshimiwa Joel Mwaka Makanyaga, Mbunge wa Chilonwa.

Na.100

#### **Miundombinu ya Barabara – Jimbo la Chilonwa**

**MHE. JOEL M. MWAKANYAGA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuitengeza barabara inayounganisha kijiji cha Bwawani kilichopo Kata ya Manchali na Kijiji cha Ikowa kilichopo Kata ya Ikowa ili iweze kupitika katika kipindi chote cha mwaka?

**SPIKA:** Majibu ya swalii hilo la watu wa Chilonwa, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH S. KANDEGE)** alijibu:-

Mheshmiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joel Mwaka Makanyaga, Mbunge wa Chilonwa, kama ifuatavyo:-

Mheshmiwa Spika, Serikali kupitia Wakala wa Barabara za Vijiji na Mijini (*TARURA*) Wilaya ya Chamwino imekuwa ikifanya matengenezo ya mara kwa mara ili kuwezesha barabara hiyo kupitika nyakati zote. Katika mwaka wa fedha 2017/2018, Serikali ilifanyia matengezo barabra ya Chinangali II – Ikowa yenye urefu wa kilomita tatu kwa gharama ya shilingi milioni 14.15.

Mheshimiwa Spika, ili kuifikia barabara ya Chinangali II – Ikowa ni lazima kutengeneza kwanza barabara ya Mwegamile – Makoja - Ikowa na katika mwaka wa fedha 2019/2020, Serikali imetenga kiasi cha shilingi milioni 114 kwa ajili ya kufanya matengenezo barabara ya Mwegamile –Makoja – Ikowa. Aidha, tathmini iliyofanywa na Wakala wa Barabara za Vijiji na Mijini (*TARURA*) imebainisha kuwa jumla ya shilingi milioni 668.2 zinahitajika kufanya matengenezo makubwa ambayo ndiyo itakuwa suluhisho la kudumu kwenye barabara ya Ikowa - Kiegea kwa maana ya Bwawani yenye urefu wa kilomita 12.3.

Mheshimwia Spika, katika mwaka wa fedha 2018/2019, Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino imetengewa bajeti ya shilingi bilioni 1.4 kwa ajili ya matengenezo ya barabara na ilipokea kiasi cha shilingi bilioni 1.2 ikiwa ni asilimia 82 ya bajeti. Baadhi ya barabara zilizotengenezwa ni barabara ya lami ya Chamwino Mjini, Haneti – Kwahemu-Gwandi na Zajilwa. Chinangali II – Chilowa na barabara ya Dabalo – Segela. Aidha, kwa mwaka fedha 2019/2020 Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino imetengewa kiasi cha shilingi bilioni 1.366 kwa jili ya matengenezo ya barabara.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na jitihada za kutafuta fedha kuiwezesha *TARURA* kuimarisha mtandao wa barabara wa Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino ikiwa ni pamoa na barabara inayounganisha Kijiji cha Bwawani – Ikowa.

**SPIKA:** Mheshimwa Joel Mwaka Makanyaga, Mbunge wa Chilonwa, swali la nyongeza tafadhali.

**MHE. JOEL M. MWAKANYAGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu yanayotia moyo kwa wananchi wa Jimbo la Chilonwa. Pia nishukuru kwa ujumla wake jibu limekuwa la jumla mno kwa halmashauri lakini kwa jumla mno kwa Jimbo la Chilonwa, kwamba barabara nyangi zimetengezwa mwaka jana na nyangi zimepangwa kutengenzwa mwaka huu. Sasa ombi langu kwa Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa mwaka huu wa fedha 2019/2020 ambapo zimetengwa bilioni 1.366, naiomba Serikali ifanye kila linalowezekana kuhahikisha kwamba barabara hii ya kutoka bwawani kuja lkowa angalau inatengenezwa na angalau iwe inatengenezwa kwa zile sehemu korofii ili iweze kuitika kipindi kizima cha mwaka. Ahsante sana.

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS,TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH S. KANDEGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Makanyaga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimetoea majibu ya msingi kwamba uhitaji kwa ajili ya kukamilisha barabara hii ni shilingi milioni 668.2, ni kiasi kingi cha fedha na katika bajeti ambayo wametengewa ni bilioni 1.366 maana yake ukisema unamega kiasi chote barabara zingine ambazo nazo zina uhitaji maalum zitakosa kutengenezwa. Naomba Mheshimiwa Mbunge avute subra kama ambayo nimejibu kwamba Serikali inajitahidi kutafuta kiasi kingine cha fedha ili tuweze kutengeneza barabara hiyo iweze kuitika katika vipindi vyote. Katika mikoa ambayo sisi kama Taifa kipaumbele kwa barabara ni pamoja na Dodoma, ndio maana hata bajeti yake imetengwa nyangi ukiliganisha na mikoa mingine.

**SPIKA:** Tunaendelea na Wizara Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, swali linaulizwa na Mheshimiwa Allan Joseph Kiula, Mbunge wa Ilamba Mashariki. Mheshimiwa Kiula uliza swali lako tafadhali.

Na.101

**Hitaji la Barabara ya Lami inayounganishwa Mikoa ya Simiyu na Singida**

**MHE. ALLAN J. KIULA** aliuliza:-

Sera ya Serikali ya Awamu ya Tano ni kuunganisha kwa barabara za lami:-

Je, ni lini Serikali itajenga barabara ya lami inayounganisha Mikoa ya Simiyu na Singida kupitia Daraja la Sibiti lillopo Wilaya ya Mkalama?

**SPIKA:** Majibu kwa swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Elias Kwandikwa, tafadhali

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MWASILIANO**  
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Allan Joseph Kiula, Mbunge wa Jimbo la Iramba Mashariki kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mikoa ya Simiyu na Singida inaunganishwa na barabara yakutokea Bariadi kupitia Maswa – Lalago-Ng’hoboko- Mwanhuzi- Sibiti – Mkalama- Gumanga – Nduguti - Iguguno Shamba hadi Singida Mjini yenyе urefu wa kilomita 341 na inaunganishwa pia na barabara ya kutoka Bariadi kupitia – Mwandoya – Ng’hoboko – Mwanhuzi – Sibiti – Mkalama – Gumanga – Nduguti – Iguguno Shamba – Singida Mjini yenyе urefu wa kilomita 338 na barabara hizi

zinahudumiwa na Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*) Mikoa ya Singida na Simiyu.

Mheshimiwa Spika, Ujenzi wa Daraja la Mto Sibiti lenye urefu wa mita 82 umekamika na ujenzi wa barabara unganishi zenyé jumla ya urefu wa kilomita 25 umekamilika kwa kiwango cha changarawe na ambapo taratibu za manunuzi za kuzijenga kwa kiwango cha lami zinaendelea. Barabara ya Sibiti – Mkalama – Gumanga – Nduguti hadi Iguguno kilomita 106 ipo upande wa Mkoa wa Singida na sehemu ya barabara hii kuanzia Sibiti hadi Mkalama kilomita 27 inaendelea kufanyiwa usanifu wa awali kupitia Mradi wa Serengeti *Southern Bypass* sehemu iliyobaki ya barabara hii ni barabara ya kiwango cha changarawe na hupitika majira yote ya mwaka.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mkoa wa Simiyu barabara ya kuaznia Sibiti- Mwanhuzi-Ng'oboko kupitia Lalago- Maswa hadi Bariadi, sehemu ya kuanzia Bariadi - Maswa kilomita 49.5 inaendelea kujengwa kwa kiwango cha lami na sehemu ya kuanzia Maswa – Lalago – Ng'oboko – Mwanhuzi – Sibiti kilomita 146.83 inaendelea kufanyiwa usanifu wa awali kupitia mradi wa Serengeti *Southern Bypass* Kisesa hadi Bariadi ni bararaba ya changarawe na inapitika vizuri majira yote ya mwaka.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutambua umuhimu wa barabara hii inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kufanya usanifu wa kina kwa sehemu zilizobaki ziweze kujengwa kwa kiwango cha lami.

**SPIKA:** Mheshimiwa Allan Kiula swali la nyongeza, tafadhalii.

**MHE. ALLAN J. KIULA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza niipongeze Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi kubwa ya kukamilisha Daraja la Sibiti. Ninayo maswali mawili ya nyongeza. Swali la pili, kwa sababu sasa Daraja hilo Sibiti limekamika na magari

makubwa yanapita juu yakiwemo ma-semi trailer na makampuni mbalimbali ya mabasi yanayoonesha nia ya kupita huko ikiwemo Simiyu, Turu basi. Je, Serikali ipo tayari kuimarisha madaraja madogo madogo yanayokadiriwa kufikia nane ambayo yapo haratin kuvunjika kutokana na uzito wa magari yanayopita kwenye daraja hilo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; barabara hiyo kwa sababu tumeelezwa kwamba itajengwa, Serikali ina kauli ipi kwa wananchi ambao wamewekewa alama ya X kwenye Vijiji vya Chemchem, Ibaga, Gumanga, Kisuluiga, Nduguti, Ishenga, Kinyangiri na Iguguno? Wangependa kupata kauli kuhusu hatima yao ya maeneo ambayo walikuwa wanayamiliki.

**SPIKA:** Majibu, hatima ya wananchi hao, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kiula, kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Kiula namna anavyopigania maeneo ya Mkalama na Mkalama inafanya uzalishaji mkubwa sana wa mazao ikiwemo vitunguu na mahindi. Mheshimiwa Kiula mwenyewe ni mkulima kwa hiyo anafahamu mahitaji muhimu ya barabara katika maeneo yake. Niseme tu kweli barabara hii kutoka Iguguno Shamba kwenda Sibiti kilomita 103, iko kwenye utaratibu mzuri wa kuiboresha sana na Mheshimiwa Kiula atakubalina nami kwamba yale madaraja makubwa tumeshaanza kuyafanyia ujenzi na kuna miradi ya ujenzi inaendelea.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nimhakikishie tu Mheshimiwa Kiula kwamba, yale makalavati madogo madogo ambayo sehemu nyingi yanaonesha kuwa yana usumbufu tunaendelea kuyashughulikia ili yakae vizuri ikiwa ni pamoja na kuondoa zile kona, kwa sababu sasa hivi baada ya kukamilika Daraja la Sibiti magari makubwa

nafahamu kwamba yanapita katika barabara hii kwenda kwenye mikoa hiyo ya Simiyu pamoja na Mwanza. Kwa hiyo tunaendelea kufanya marekebisho makubwa ili kusiwe na usumbufu, lakini pia kuepusha ajali ambazo zinaweza kutohana na barabara jinsi ilivyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wananchi waliowekewa alama ya X niwahahakikishie wananchi hawa, kwanza niwapongeze na kuwashukuru kwa kutoa ushirikiano kwa kuwa na utayari wa kupisha eneo la mradi wa barabara hii muhimu na wananchi hawa wanafahamu kwamba barabara ni kwa ajili ya maendeleo yao. Kwa hiyo, niwahakikishie tu kwamba tumeweke alama za X ili kuwatahadharisha wananchi wasifanye maendelezo makubwa katika maeneo haya. Baada ya kumaliza usanifu wa awali na upembuzi yakinifu, tutajua gharama za kuwafidla wananchi hawa. Niwahakikishie wananchi hawa kwamba tutawafidia ili kupisha mradi ili tuweze kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami.

**SPIKA:** Nilimwona Mheshimiwa Mtaturu.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Spika, ndiyo.

**SPIKA:** Endelea Mheshimiwa Mtaturu.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona.

Matatizo ambayo ameyaeleza Mheshimiwa Kiula yamefanana na Wilaya ya Ikungi ambayo ndiyo Jimbo la Singida Mashariki lilipo. Wakati nauliza swali hili naomba niwahakikishie wananchi wa Jimbo la Singida Mashariki, niko imara kuwawakilisha katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nilitaka niseme tu, kwa kuwa barabara au miundombinu ya barabra ndiyo inayosaidia kukuza uchumi wa wananchi; na kwa kuwa barabara ya Njiapanda – Makiungu – Kwamtoro mpaka kule Handeni ni

barabara ambayo imekuwa ikifanyiwa upembuzi muda mrefu: Ni lini sasa Serikali itaanza kujengwa na kuweza kusaidia kukuza uchumi wa wananchi wa Wilaya ya Ikungi na Mkoa wa Singida? (*Makofii*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Elias Kwandikwa.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Mtaturu na nimhakikishie tu kwamba tutampa ushirikiano wa hali ya juu katika kutekeleza majukumu yake ya kibunge katika eneo lake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba, barabara anayoitaja Mheshimiwa Mbunge kutoka Njiapanda kuptilia Makiungu kwenda kwa Mtoro, itatoka Chemba kwenda mpaka Handeni, kilometra 461; ni kweli kwamba usanifu umeshakamili na kwa kadri tutakavyopata fedha tutaanza kujenga barabara hii. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi kwamba mradi huu mkubwa wa Kilometra 461 utawanufaisha sana wananchi wa eneo lake na kwa kweli tumejipanga kama Serikali kuona kwamba tunawahudumia vizuri wananchi katika eneo lake. nnAhsante. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tuendelee na swali la Maliasili na Utalii, swali linaulizwa na Mheshimiwa Oscar Rwegasira Mukasa, Mbunge wa Biharamulo Magharibi. Mheshimiwa Mukasa, uliza swali lako tafadhalii.

Na. 102

**Tembo Wanaoharibu Mazao ya Wananchi Kijiji  
cha Kabukome-Biharamulo**

**MHE. ALEX R. GASHAZA (k.n.y. MHE. OSCAR R. MUKASA)** aliuliza:-

Mwanzoni mwa mwaka 2016 wananchi wa Kijiji cha Kabukome Kata ya Nyarubungo Wilaya ya Biharamulo walivamiwa na tembo na kupoteza asilimia kubwa ya mazao yao:-

Je, ni lini wananchi hao watapata fidia ya mazao yao?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Oscar Rwegasira Mukasa, Mbunge wa Biharamulo Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kufuatia kuongezeka kwa juhudzi za uhifadhi nchini na kupungua kwa ujangili, wanyamapori hususan tembo wamekuwa wakitoka ndani ya hifadhi na kupita maeneo ambayo ni shoroba au maeneo ya vijiji yanayopakana na maeneo ya hifadhi, ikiwemo baadhi ya vijiji vinavyopakana na yaliyokuwa mapori ya akiba ya Biharamulo na Burigi, kwa sasa ni Hifadhi ya Taifa ya Burigi - Chato katika Wilaya ya Biharamulo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto hiyo, Wilaya imekuwa ikichukua hatua kadhaa ili kunusuru maisha na mali za wananchi ambazo ni pamoja na kushughulikia matukio ya uvamizi wa wanyama kama tembo kwa haraka ikiwezekana pindi yanapojitokeza na kutoa elimu ya uhifadhi kuhusu namna ya kujilinda, lakini pia wananchi kuepuka kulima kwenye shoroba na mapito ya wanyamaporii.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imekuwa ikitoa fedha kama pole kwa wananchi wanaoathirika na matukio ya wanyamaporii wakali na waharibifu ikiwa ni pamoja na kifuta jasho na kifuta machozi, siyo fidia kwa mujibu wa

Kanuni ya Kifuta Jasho na Kifuta Machozi ya Mwaka 2011. Aidha, Kanuni husika zinafanyiwa marekebisho ambapo kwa sasa maoni ya wadau ndani na nje yamekusanywa, hatua inayofuata ni kuwasilisha kanuni hizo kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii na baada ya hapo zitasainiwa na Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, kumbukumbu zinaonyesha kuwa katika kipindi cha mwaka 2016/2019, Wizara yangu hajapokea maombi yoyote kutoka Kijiji cha Kabukome, Kata ya Nyarubongo, Wilaya ya Biharamulo. Hivyo ninashauri Mheshimiwa Mbunge kuitia Halmashauri ya Wilaya kuwasilisha maombi husika ili yafanyiwe kazi kwa mujibu wa Kanuni za Kifuta Jasho na Kifuta Machozi za Mwaka 2011. Wananchi watakaokidhi vigezo watalipwa kifuta jasho mara baada ya taratibu kumalikika.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Alex Gashaza, uliza swalii nyongeza tafadhali. (*Kicheko*)

**MHE. ALEX R. GASHAZA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swalii la kwanza. Kwa kuwa matukio haya yamekuwa yanajitokeza mara kwa mara hususan katika Kijiji hicho cha Kabukome; na kwa kuwa Serikali imetoa maelekezo kwa Halmashauri kwamba wananchi hawa waweze kuwasilisha madai yao ili waweze kulipwa kifuta jasho: Je, Naibu Waziri pengine baada ya Bunge hili kufika katika eneo hilo ili kuweza kushauriana pia na wananchi wa eneo hilo kuona ni namna gani ya kuweza kuzuia tukio hili lisiweze kuwa endelevu?

Mheshimiwa Spika, swalii la pili. Kwa kuwa Kijiji hiki cha Kabukome kinavyoathirika inafanana sana na baadhi ya viji katika Jimbo la Ngara vinayopakana na Hifadhi ya Taifa ya Burigi - Chato, Kijiji cha Gwakalemela Kata ya Kasulu na Kijiji cha Rusumo Kata ya Rusumo kwa sababu matukio haya yamekuwa yakijitokeza mara kwa mara, anaweza

akafika pia katika maeneo hayo kwa ajili ya kushauriana na wananchi wanaoishi katika maeneo hayo namna gani ya kuweza kuendelea kudhibiti uvamizi wa wanyama hawa hasa tembo? (*Makofii*)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kumpongeza Mheshimiwa Alex Gashaza kwa kuwa mshiriki mzuri katika uhifadhi, amekuwa pia akitusaidia sana kurejesha mahusiano kati yetu na wananchi katika maeneo yanayozunguka pori la Burigi - Chato. Pia namshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Oscar Mukasa kwa sababu amekuwa akifuatilia sana haki za wananchi wake katika eneo hili ambalo wamepata mgogoro wa wanyama.

Mheshimiwa Spika, taratibu za kulipa fidia ndiyo zinazosumbua kwenye maeneo mengi. Inatakiwa mwananchi anapopata tatizo la kuliwa kwa mazao yake au kushambuliwa na wanyama, ndani ya siku tatu, kama ni shamba awe ametoa taarifa kwenye Serikali ya Kijiji; na Afisa wa Kilimo amekagua na kuwasilisha kwa Afisa Wanyamapori wa Wilaya. Afisa Wanyamapori au Afisa wa Kilimo wa Wilaya ndiye anayeleta taarifa hizi kwenye Wizara yetu nasi tunashughulikia.

Mheshimiwa Spika, kama ni shambliong la mauaji, Afisa wa Kijiji anatoa taarifa Polisi na Polisi na Daktari wanafanya *postmortem* na baadaye taarifa hizi zinafika kwenye Wizara yetu nasi tunaweza kulipa. Hata hivyo, sehemu nyingi taarifa hizi zinachelewa kufika, zinafanyika baada ya tukio kupita muda mrefu, kwa hiyo, wanapokwenda watu wa kufanya tathmini, wanakuta shamba lilishapata uoto mwengine wa asili.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba sisi Wizara yetu iko tayari

kutoa kifuta jasho na kifuta machozi mara tu tukio hili linaporipotiwa ndani ya muda.

Mheshimiwa Spika, swali la pili la Mheshimiwa Mbunge, anaomba mimi Waziri nipate nafasi kwenda Jimboni kuweza kushirikiana kutoa elimu katika vijiji vya Benako, Kalemela na Kasulo, naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba niko tayari na nitafanya hivyo baada ya Bunge hili. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante tuneandelea. Mheshimiwa Sannda nimekuona, swali la nyongeza tafadhalii. (*Makofi*)

**MHE. EDWIN M. SANNDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Wananchi wa vijiji vya Chemchemi, Tampori, lyoli kule Kata ya Kingale pamoja na Muluwa Kata ya Serya wamekuwa wakipata athari kubwa sana kutokana na wanyama waharibifu hawa tembo, almaarufu kule Zanzibar, Unguja ya Kusini kama ndovu.

Mheshimiwa Spika, tunaishukuru sana Serikali, wameanza kufanya malipo ya vifuta jasho na vifuta machozi kuanzia mwaka 2016 kwa baadhi ya vijiji, lakini athari hizi zimeanza 2012, taratibu zote zilifuatwa na pia madai yakawasilishwa Wizarani.

Sasa Je, kuna mpango gani wa kufanya malipo ya maeneo yaliyoachwa tangu mwaka 2012 kwa watu wote na kwa maeneo yote ambayo yalipata athari?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Costantine Kanyasu, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sannda, Mbunge wa Kondo Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba athari za wanyama zimeendelea kuwepo na kwa sasa hivi

zimeendelea kusumbua nchi nzima. Labda tu nitumie nafasi hii kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge kwamba kabla ya miezi michache iliyopita, ilikuwa ni jukumu la TAWA peke yake kuitia kikosi cha *KDU* kwenda *ku-respond* na matukio ya wanyama waharibifu yanapotokea, lakini Wizara imefanya marekebisho kama ilivyo kwenye maelekezo na hivi sasa popote ambapo tuna Hifadhi ya Taifa au tuna pori la akiba iwe ni TANAPA au TAWA au ni *TFS* katika eneo hilo, wanawajibika *ku-respond* na wanyama waharibifu wanapotokea kwenye maeneo ya vijiji. Kwa hiyo, maelekezo haya tumeshayatoa kwenye Taasisi zetu zote hizi.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tulianza kulipa mwaka 2016 na hii ilisababishwa na kutokuwepo kwa kumbukumbu za kutosha huko nyuma. Mwaka 2018 peke yake Wizara yangu imelipa shilingi billioni 1.6 kama kifuta jasho na fidia. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tatizo la kutokulipa huko nyuma pamoja na kumbukumbu ilikuwa pia ni tatizo la fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, mwaka huu peke yake mpaka leo tuna madai ya wananchi yanayofikia takriban shilingi billioni 3.2 lakini mfuko wetu hauwezi kuzidi shilingi billioni 1.6. Kwa hiyo, pale ambapo kumbukumbu zitaonyesha kwamba kuna wananchi bado wanadai, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Wizara yangu itafanya mpango wa kulipa.

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Fedha na Mipango, swali linalizwa na Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub. Mheshimiwa Jaku tafadhali uliza swali lako.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Swali hili ni la muda mrefu, limekuja karibu mara nne au mara tano. Naomba lipate jibu na nitahitaji msaada wako kwa Watanzania kuhusu swali hili.

Na. 103

**Wateja wa Benki ya *FBME***

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB** aliuliza:-

(a) Je, ni lini Benki ya *FBME* italipa wateja amana zao zilizokuwepo kwenye Benki hiyo?

(b) Je, Benki iko katika hali gani sasa?

(c) Je, Benki Kuu ya Tanzania ina dhamana gani katika kulinda Mabenki?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, Dkt. Ashatu Kijaji, ukizingatia maoni ya Mheshimiwa Jaku.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango na kwa kuzingatia maombi ya Mheshimiwa Jaku, naomba kujibu swali lake lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Benki ya *FBME Limited* ilifutiwa leseni ya kufanya biashara hapa Tanzania na Benki Kuu ya Tanzania mnamo tarehe 8 Mei, 2017 kutokana na tuhuma za kujihusisha na biashara ya kutakatisha fedha huko nchini Marekani. Aidha, Benki Kuu iliteua Bodi ya Bima ya Amana kuwa Mfilisi wa Benki hiyo. Katika kitimiza wajibu wake wa msingi, Bodi ya Bima ya Amana ilianza zoezi la kulipa fidia kwa mujibu wa Sheria kwa waliokuwa na amana katika benki hiyo kuanzia mwezi Novema, 2017 na bado zoezi hilo linaendelea.

Hadi kufikia tarehe 9 Septemba, 2019 jumla ya kiasi cha shilingi milioni 2,404.2 kimelipwa kwa wateja 3,426 kama fidia ya Bima ya Amana. Kiasi hicho ni sawa na asilimia 55.9 ya kiasi chote kilichotarajiwa kulipwa kama fidia ya Bima ya

amana kwa wateja wote 6,628 waliopo Tanzania pamoja na wateja waliopo nje ya nchi (*Tanzania International Banking Depositors*). Aidha, jumla ya shilingi milioni 2,401.2 zimelipwa ikiwa ni asilimia 83.3 ya lengo la kulipa jumla ya shilingi milioni 2,882.6 kwa wateja waliopo Tanzania tu.

Mheshimiwa Spika, wateja waliokuwa na amana zaidi ya shilingi milioni 1.5 watalipwa kiasi kilichobakia kwa mujibu wa sheria na taratibu za ufilisi. Kiasi kitakacholipwa kwa wenge amana zaidi ya shilingi milioni 1.5 kitategemea fedha zitakazopatikana kutokana na mauzo ya mali za benki pamoja ukusanyaji wa madeni kutoka kwa wadeni wa benki hiyo.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa sasa Benki ya *FBME Limited* ipo katika hatua za ufilisi na hivyo haiendeshi shughuli zozote za kibenki hapa nchini.

(c) Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006 imeipa Benki Kuu ya Tanzania mamlaka ya kutoa leseni, kutunga Kanuni, kusimamia benki zote zinazochukua amana za wateja na kuchukua hatua za kisheria dhidi ya benki zinazoendesha biashara bila kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na miongozo iliyopo.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, Benki Kuu imepewa mamlaka ya kusimamia na kudhibiti benki na taasisi za fedha ili kuhakikisha kuwa amana za wateja zinakuwa salama pia kuna usalama, utulivu na uthabiti wa Sekta ya Fedha na uchumi kwa ujumla. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Jaku, majibu muafaka?

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Spika, haya ndio majibu ya muda mrefu, lakini anavyoanguka ndivyo anavyochinjwa. Nami nitakuja hivyo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Waziri, kwanza nakupongeza na mionganoni mwa Manaibu Waziri wanaopigiwa simu wewe

na Atashasta Nditiye mnapokea kwa wakati tofauti na Mawaziri wengine, hilo hongereni sana. (*Makofi*)

Mheshiniwa Naibu Waziri, swali hili limeulizwa karibu mara tano humu ndani nikiwemo mimi mwenyewe tarehe 6 Septemba, 2018 na leo ni tarehe 12 Septemba, 2019, ni mwaka mmoja na siku kidogo. Kama mwaka mmoja hivi tulifanyiwa semina hapa Ukumbi wa Msekwa, walikuja *Ma-deputy governor* karibu watano, Wakurugenzi na Watendaji na niliuliza swali hili, wakasema hizi fedha ziko *Dutch Bank* zitaletwa muda siyo mrefu. Sasa swali langu ni: Je, tokea muda huo zinaletwa kwa balskeli ama kwa mguu? Maana ni muda mrefu hazjifikia. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, hivi juzi hawa jamaa walishinda kesi yao huko Uingereza: Je, ni kweli na kwamba waliambiwa waliofungua kesi hiyo walipe gharama za kesi? Ni kweli wameshinda kesi? Kama wameshinda, ni hatua gani zinazofuata? Wengine tukumbuke Mheshimiwa Naibu Waziri, cheo ni dhamana...

**SPIKA:** Maswali yasiwe mengi, nataka maswali mawili tu Mheshimiwa Jaku.

Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali mawili katika mlolongo huo tafadhali, Mheshimiwa Dkt. Ashatu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza, amekuwa mfuatiliaji mzuri sana tangu benki hii ilipofutiwa usajili wake hapa nchini akifuatilia amana za wateja ili waweze kulipwa. Kwa dhamira njema na nia njema ya Serikali yetu, ndiyo kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi kwamba kwa shilingi milioni 1.5 wateja ambao walikuwa na amana hiyo ndani ya benki, yatari tumeshalipa zaidi ya asilimia 83 ya wateja wote. Asilimia 17 iliyobaki ni wateja ambao hawajajitokeza wao wenyewe kuja kuchukua amana zao.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba dhamira ya Serikali yetu ni njema na

ndio maana tumeanza kulipa hawa wateja wote ambao walikuwa na fedha zao ambazo hazizidi shilingi milioni 1.5 kama sheria inavyotuelekeza.

Mheshimiwa Spika, kwenye swali lake la kwanza naomba niyajibu yote mawili kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza fedha hizi hazitakuja kwa baiskeli, wala kwa gari, wala kwa meli, ila ni taratibu za kisheria zitakapokalimika. Nachukua fursa hii kumpongeza sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wakili Mkuu wa Serikali pamoja na Benki Kuu ya Tanzania, wanafanya kazi kubwa kuhakikisha amana za wateja wetu wote ambao wako ndani ya Tanzania na nje ya Tanzania zinabaki kuwa salama na wanazipata pale ambapo tumemaliza majadiliano na Benki Kuu ya Cyprus.

Mheshimiwa Spika, tayari mwezi wa Tisa baada ya Mahakama za nchini Cyprus kurejea na kuanza kufanyakazi yao, kesi zote zilizokuwa zimefunguliwa, tumekubaliana zitafutwa na tayari sasa fedha hizo zitafika ndani ya nchi yetu na watu wetu wote wataweza kulipwa fedha zao.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, majibu ya nyongeza tafadhali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, naomba tu nitoe majibu ya nyongeza kwa swali la nyongeza alilouliza Mheshimiwa Mbunge na hasa kuhusu ile kesi ya Uingereza.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba wamiliki wa iliyokuwa Benki ya *FBME* walifungua kesi Uingereza. Lakini lengo la kesi ile ilikuwa ni ku-*challenge* mwenendo wa mchunguzi aliyekuwa anachunguza masuala ya *FBME* kule Uingereza, ni kweli kwamba Mahakama kule imetoa hukumu yake lakini kwa namna yoyote hukumu au matokeo ya kesi ile haiathiri suala zima la *liquidation* ya ile benki huku. Kwa maneno mengine, hukumu ile haina athari yoyote wala haigusi jambo

lolote katika mchakato unaoendelea kwa upande wa Tanzania na Cyprus.

Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Nilikuona Mheshimiwa Shally Raymond, swalil nyongeza.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa benki hii ilikuwa na matawi Dar es Salaam, Mwanza na Arusha, na kwa kuwa benki hii ilikuwa na wafanyakazi zaidi ya 100 na familia hizo na wafanyakazi hao mpaka sasa hawajui hatma yao, familia hizo zinateseka kulipa ada, kulisha ndugu na kadhalika.

Je, ni lini sasa wafanyakazi hao watafahamishwa hatima yao kwa sababu pia hawawezi hata kwenda kuomba kazi mahali pengine popote? (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya swalil hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji tafadhali.

**NAIBU WAZIRI W AFEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimesema kwenye majibu ya msingi na majibu ya nyongeza ambayo nimemjibu Mheshimiwa Jaku Hashim, baada ya kuwa tumemaliza majadiliano na Benki Kuu ya Cyprus na kuingia sasa kwenye mchakato wa kuhakikisha kila mwenye haki yake anapata haki yake ni imani yangu na wafanyakazi hao wa iliyokuwa Benki ya *FBME Limited* watapata haki yao, nimesema wazi mwezi wa Septemba, baada ya Mahakama za nchini Cyprus kurejea kazini basi yote hayo yatajulikana na kila mmoja atapaa haki yake na kwa wafanyakazi kwa sababu walajirriwa na Benki hii ambayo ilikuwa na Makao Mkuu hapa nchini, basi sheria zetu za kazi na ajira zitatumika ili kila mtumishi aweze kupata haki yake. (*Makofi*)

**SPIKA:** Tunaendelea na Wizara ya Viwanda na Biashara. Swali la Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini, uliza swali lako tafadhalii.

Na. 104

**Eneo la EPZA Mtwara**

**MHE. HAWA A. GHASIA** aliuliza:-

Je, ni nini mpango wa Serikali katika kuendeleza eneo EPZA Mkoani Mtwara.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini, kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, eneo la *Special Economic Zone* Mtwara (*SEZ*) lipo katika eneo la Msanga Mkuu. Eneo hilo litaendelezwa kwa ajili ya bidhaa zinazotokana na mafuta na gesi ambapo litajengwa *Petrochemical Complex* pamoja na kiwanda cha kuzalisha mbolea. Mkoa wa Mtwara kupitia Baraza la Ushauri la Mkoa Mtwara (*RCC*) umeingia mkataba na kampuni ya *Helm AG* na *Proman A.G* kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda cha mbolea.

Mheshimiwa Spika, eneo la Mtwara *SEZ* linahusisha kuanzishwa kwa viwanda vitano vya kuzalisha *methanol*, kiwanda cha kuzalisha *ammonia* kutengeneza *petrochemical*, mbolea na *urea* na *melamine*. Mradi huo ambaao umepangwa kutekelezwa katika awamu tatu utagharimu Dola za Kimarekani Bilioni Tano ambapo awamu ya kwanza itagharimu dola za Kimarekani Bilioni Moja. Utekelezaji wa mradi wa kutengeneza mbolea unatarajiwa kuanza mara muafaka wa bei ya gesi asilia kati ya Serikali

na Mwekezaji utakapofikiwa. Juhudi za kuhitimisha majadiliano zinafanyika.

Mheshimiwa Spika, uendelezaji wa eneo hili unaendelea na kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 Serikali ilitoa shilingi bilioni 3.95 kwa ajili ya kuendeleza miundombinu ya maji na usanifu wa barabara za kuingia eneo la mradi. Kazi hizi zimeletekelezwa na *TARURA* pamoja na Mamlaka ya Maji Mtwara (*MTUWASA*). Hadi sasa kazi ya kujenga miundombinu ya maji imekamilika, na kazi ya ujenzi wa barabara na jengo la utawala zinaendelea na matarajio ni kukamilika mwezi Desemba 2019.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hawa Ghasia nimekuona, swalii nyongeza tafadhali.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake ambayo ameyatoa. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza eneo ambalo amelizungumzia zaidi siyo eneo la Msanga Mkuu, ni eneo la Mtwara Mjini. Kwa upande wa Msanga Mkuu hakuna kazi yoyote ambayo mpaka sasa hivi imefanyika ambayo inaweza kubeba ujenzi wa viwanda ambavyo amezungumzia. Je, ni lini majadiliano ya bei ya gesi asilia yatakamilika ili hivyo viwanda vianze kujengwa?

Mheshimiwa Spika, swalii la pili, inapotokea kwamba mchakato wa majadiliano unachukua muda mrefu sana kama ambavyo *Hel'm* na *TPDC* wamechukua tangu mwaka 2011 mpaka leo 2019 majadiliano hayajakamilika. Nini nafasi ya Wizara ya Viwanda na Biashara kuwasaidia wawekezaji ili waweze kutoka katika huyo mkwamo ambao wameupata. (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo muhimu, majadiliano miaka nane.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:**  
Mheshimiwa Spika, ahsante.

Mheshimiwa Spika, kwanza ninashukuru kwa niaba ya Wizara kwa pongezi alizotupa kwa majibu, pili niseme tu kwamba Serikali imekuwa ikienendeza juhudhi ya kukamilisha mazungumzo hayo, suala la gesi ni utajiri wa Tanzania ambao unapaswa kutumika kwa uangalifu mkubwa. Kwa hiyo, kabla ya kuingia mkataba, ni muhimu sana kwa Serikali kuangalia kwamba inampa mwekezaji gesi hiyo kwa bei ambayo kwanza itakuwa ni bei inayokubalika lakini vilevile kumhakikishia upatikanaji wa malighafi hiyo kwa wakati wote.

Mheshimiwa Spika, nikiendelea na swalilake la pili la kuchukua muda mrefu niseme tu kwamba Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Uwekezaji pamoja na Wizara ya Nishati na Madini tutahakikisha kwamba hilo zoezi la kukamilisha kwa bei inayotakiwa ili aweze kupewa mwekezaji linafanyika mapema iwezekanavyo. Kwa hiyo, nalichukua hili kama *commitment* ya kushirikiana na Wizara nilizozitaja kuhakikisha kwamba tunafanya kazi mapema ili nchi iweze kunufaika na gesi ambayo inapatikana Mtwara. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea na Wizara ya Kilimo, swalilake na Mheshimiwa Mbunge wa Kasulu Mjini, Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, tafadhalililiza swalilako.

Na. 105

**Uhaba wa Mbegu za Mahindi na Maharage Nchini**

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO** aliuliza:-

Nchi yetu kwa muda sasa imekumbwa na uhaba mkubwa wa mbegu hasa za mahindi na maharage ambayo ni mazao ya chakula, kwa taarifa zilizopo Wizara ya Kilimo 2018 nchi yetu inazalisha mbegu hizo kwa asilimia zisizozidi 35 tu:-

(a) Je, kuna mkakati gani wa kutatua tatizo hilo ili angalau nchi itosheleze kwa asilimia 70?

(b) Je, ni kwa nini shamba la mbegu la Bugaga lililopo Wilaya ya Kasulu lisiwe kitovu cha kuzalisha mbegu za mahindi na maharage?

(c) Je, ni kwa nini Serikali haiwekezi katika uzalishaji wa mbegu hizo.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo Mheshimiwa Hussein Bashe, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. HUSSEIN M. BASHE)**  
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko Mbunge wa Kasulu Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, upatikanaji na uzalishaji wa mbegu bora ikiwemo za mahindi ngano, maharage, mpunga, soya, alizeti, mtama, ufuta na mbegu za mazao ya bustani kwa msimu 2018/2019 ulifkia tani 49,000, kati ya hizo tani 38,000 sawa na asilimia 78 zilizalishwa nchini, tani 8,361 sawa na asilimia 17 ziliagizwa nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, mikakati ya Serikali ya kuongeza uzalishaji wa mbegu ni pamoja na kuwezesha Wakala wa Mbegu za Kilimo (*ASA*) kuongeza uzalishaji wa mbegu bora katika mashamba ya Mwele, Dabaga, Mbozi, Msimba, Bugaga na Arusha, kutumia Taasisi za Utafiti wa Kilimo kuzalisha mbegu mama, msingi na zilizodhibitiwa ubora na kukodisha maeneo kwa mashamba ya *ASA* kwa kampuni binafsi za mbegu ili kuongeza uzalishaji wa mbegu bora za mazao mbalimbali ikiwemo mahindi na maharage.

Mheshimiwa Spika, aidha, mkakati mwingine ni kuongeza eneo la umwagiliaji katika mashamba ya mbegu

ya Msimba, Arusha, Dabaga na mashamba ya vituo vyatufitit kutoka hekta 200 hadi 600, kushirikisha taasisi za umma kama Jeshi la Magereza na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kuzalisha mbegu bora pamoja na vikundi vyawakulima wadogo kuzalisha mbegu za daraja la kuazimiwa ubora.

Mheshimiwa Spika, shamba la mbegu la Bugaga liliopo katika Wilaya ya Kasulu lina ukubwa wa hekta 200. Shamba hilo linamilikiwa na ASA na kwa sasa linatumika kuzalisha mbegu bora za mahindi, maharage na alizeti. Aidha, shamba hilo linatumika kuzalisha miche bora ya mchikichi, miche ya matunda ya machungwa na maembe. Pia Serikali imeanza kuchimba kisima cha maji katika shamba hilo ili kuwezesha uzalishaji wa mbegu kwa kipindi chote cha mwaka. ASA imejenga kitalu nyumba cha kukuzia miche ya mchikichi pamoja na kuandaa bustani ya kukuzia miche hiyo ya mchikichi na miche ya matunda.

Mheshimiwa Spika, mkakati wa Serikali ni kuongeza uzalishaji wa mbegu ambapo Serikali katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 imetenga takribani shilingi bilioni 1.3 kwa ajili ya utafiti wa mbegu kupitia Taasisi ya Utafiti wa Mbegu – TARI na uzalishaji wa mbegu kupitia Wakala wa Mbegu za Kilimo – ASA kwa ajili ya kuzalisha mbegu kwa njia ya umwagiliaji ili kuongeza uzalishaji mara tatu hadi nne zaidi ya sasa.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuzisihi Halmashauri kutotumia maeneo yaliyotengwa kwa tafiti za Kilimo kwa shughuli zingine ikiwemo kujenga stendi za mabasi. Aidha, Wizara ya Kilimo itaamua kuyaachia maeneo haya kwa shughuli zingine baada ya kujiridhisha kwamba maeneo haya hayana tija kwa shughuli za kilimo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Spika, nimesikia maelezo ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ambayo kwa ujumla wake swali langu la msingi halijajibiwa. Swali

langu la msingi naulizia utoshelevu wa mbegu za mahindi na maharage kwa sababu ni mbegu ambao ni chakula. Je, kama nchi tunajitosheleza mbegu za mahindi na maharage kwa asilimia ngapi? Ndiyo msingi wa swali langu. Hii habari ya mtama, ufuta na ngano haikuwa msingi wa swali.

Mheshimiwa Spika, swali la pili nina hakika kuna uhaba mkubwa sana wa uzalishaji wa mbegu. Ni lini Wizara ya Kilimo sasa itakuja na mkakati unaoeleweka wa namna ya kukabiliana na tatizo hili na hasa ukizingatia kwamba Jeshi la Magereza na JKT kuna nguvukazi kubwa ambayo wanaweza kushirikiana na Wizara wakaja na mkakati wa kuondoa tatizo la mbegu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, tunataka majibu siyo maelezo tafadhalii. (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo muhimu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Bashe.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. HUSSEIN M. BASHE):** Mheshimiwa Spika, mahitaji (*potential demand*) ya nchi ni *metric tons* 120,000 kwa mwaka. Asilimia 70 ya mahitaji haya ni mbegu za mazao ya nafaka ikiwemo mahindi. Ni ukweli usiopingika kwamba kama nchi tunajitosheleza kwa asilimia 40 tu ya mahitaji yetu ya mbegu ndani ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, huu ndiyo ukweli na ndiyo *status* kwamba kama nchi tuna uwezo wa kuzalisha asilimia 40 ya tani 120,000 za mbegu ya mazao yote ndani ya nchi, kwa hiyo tuna upungufu wa asilimia 60 katika suala la uzalishaji kama nchi. Sasa hivi Wizara inafanya programu na siku ya Jumapili ya wiki hii taasisi zote zinazohusika na suala la uzalishaji wa mbegu za umma na binafsi tunafanya kikao Morogoro kwa ajili ya kutengeneza *master plan* ya miaka mitatu ili tuondokane na tatizo la *import* za mbegu na *gap* ili yopo katika suala la mbegu katika nchi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kuhusisha Taasisi za Umma kama JKT, Magereza katika *grand plan* ya miaka mitatu ya Wizara ya kufanya *seed production, research* na *seed multiplication* na *soil profiling*, JKT na Jeshi la Magereza ni sehemu ya mkakati wetu. Kwa hiyo, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko kwamba kama Wizara tunafahamu upungufu na kama Wizara tumeamua kimkakati uwekezaji wa *development partners* wote tutaupeleka kwenye *seed production, research* na *seed multiplication* kwa kutumia *irrigation* ili tuondokane na suala la uzalishaji wa mbegu wakati wa msimu wa mvua. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante. Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri. Swali hilo ilimetuchukulia muda. Baada ya swali la Mheshimiwa Nsanzugwanko, bado tuko Wizara hii ya kilimo, swali la Mheshimiwa Zaynabu Matitu Vullu.

Na. 106

**Hitaji la Soko la Kudumu la Zao la Nazi**

**MHE. ZAYNABU M. VULLU** aliuliza:-

Zao la nazi ni zao ambalo pia lina faida nyingi sana kuanzia mti, matawi, na nazi yenye:-

(a) Je, ni lini Serikali itatafuta soko la kudumu la zao hilo?

(b) Je, Serikali ina mpango wa kuhamasisha kilimo cha zao hilo kama ilivyokuwa zamani?

**NAIBU WAZIRI WAKILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA)** aliibuu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Zaynabu Matitu Vulu, Mbunge Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, soko la kudumu la zao la nazi lipo nchini kwa sababu kiasi cha nazi kinachozalishwa bado hakikidhi mahitaji ya soko la ndani la nchi kutokana na kuongezeka kwa matumizi ya zao hilo ikiwemo ulaji wa madafu na watumiaji wa nazi. Aidha, mafuta mwali yanayotokana na nazi yanaendelea kupata umaarufu kutokana na uhitaji wake kuwa mkubwa ndani na nje ya nchi ambayo lita moja inafikia hadi shilingi 40,000. Bidhaa kama fagio, mbao, ka mbao na samani zinazotokana na mti wa mnazi na uwezo wa zao hilo kutunza mazingira huongeza thamani ya zao la minazi.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha soko la zao la nazi nchini msimu wa mwaka 2018/2019 wakulima wapatao 74 katika Mikoa ya Lindi na Mtwara wamefundishwa namna ya kukamua mafuta mwali. Vilevile, kikundi cha wanachama 50 katika Wilaya ya Bagamoyo kimepewa mashine yenye uwezo wa kukamua lita 500 za mafuta ya mwali kwa mwaka. Aidha, Serikali inaendelea kuimarisha masoko ya mazao yote ya kilimo likiwemo zao la nazi kwa kuwaunganisha wakulima na wanunuzi kuititia vyama vyao ushirika, masoko ya moja kwa moja na viwanda vidogo vya kuongeza thamani ya zao la nazi.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutoa elimu kwa wazalishaji wa zao la nazi kuendelea kupanda mbegu bora zenye ukinzani dhidi ya magonjwa na zenye tija kubwa. Tanzania ni nchi ya 10 Duniani kwa uzalishji wa nazi ikiongozwa na nchi ya Indonesia na kwa Afrika ni nchi ya kwanza ambapo huzalisha wastani wa tani 530,000 za nazi kwa mwaka, ikifuatiwa na Ghana ambayo huzalisha wastani wa tani 366,183.

Mheshimiwa Spika, pia Serikali inaendelea kuhamasisha kilimo cha minazi nchini ambapo imeanzisha shamba lenye ukubwa wa hekta 54 katika kituo kidogo cha utafiti cha Mbezi Wilaya ya Bagamoyo ili kuzalisha miche bora ya minazi yenye ukinzani dhidi ya ugonjwa wa kunyong'onyea kwa minazi (*Coconut Lethal Disease*) na kuisambaza kwa wakulima kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Spika, Serikali inahamasisha kilimo cha minazi katika maeneo mapya ili kuongeza uzalishaji wa nazi nchini ambapo msimu wa 2018/2019 ilizalisha na kusambaza jumla ya mbegu ya miche 11,000 kwa wakulima katika Mikoa ya Rukwa na Mwanza. Aidha, Serikali inafanya mazungumzo ya Jumuiya ya Asia – *Pacific Coconut Community*) ambayo hutunza '*germplasm*' ya minazi kuwezesha upatikanaji wa mbegu bora za minazi zenye kuongeza tija na uzalishaji mkubwa kwa wakulima. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Vulu, swali la nyongeza.

**MHE. ZAYNABU M. VULU:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na nazi kuwa na mandhari nzuri inayovutia inapopandwa, lakini zao lake limekuwa likiporomoka bei mwaka hadi mwaka. Kwa mfano, mwaka jana bei ya jumla ya nazi illkuwa inauzwa shillingi 400 au zaidi lakini nazi hiyo hiyo mwaka huu inauzwa kwa shillingi 50. Swali la kwanza, je, Serikali ina mkakati gani wa kuweza kumsaidia mkulima kwa kuweza kudhibiti bei na kuweza kupata faida ukizingatia zao la nazi linavunwa mara nne kwa mwaka?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa nazi ina faida nyingi ikiwemo mafuta na nyingine Mheshimiwa Naibu Waziri amezielezea. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuweza kuwasaidia wakulima wa zao la nazi kuweza kuanzishiwa viwanda vidogovidogo ikiwemo ya mafuta, tui la nazi au vifuu kutengeneza mkaa mdogo mdogo ili kudhibiti mazingira ya nchi ili na wao wakulima wa zao hilo waweze kupata faida? (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Naibu Waziri Kilimo, Mheshimiwa Omary Mgumba, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA):** Mheshimiwa Spika, mkakati wa kwanza Serikali kwa ajili ya kuongeza bei pamoja na kutafuta soko kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi. Soko bado lipo kubwa ndani ya nchi na ndio maana tunalazimika wakati mwingine kuagiza tui la nazi kutoka nje ya nchi kuonyesha kwamba bado kuna

mahitaji makubwa ya nazi. Lakini tatizo kubwa linalokuja si bei, tatizo kubwa ni tija ndogo wanaipata wakulima kutokana na kipato kidogo wanachokipata kwenye kuchukua nazi.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano mzee Bakhresa yuko tayari kuwekeza na mashine zimeshaingia zina miaka minane lakini anashindwa kupata mali ghafi ya kutosha kuweza kuzalisha tui la nazi hapa nchini kwa muda wote wa mwaka. Kwa sababu kama ulivyosema ni kiasi kidogo kutokana na matatizo unayokumbuka.

Mheshimiwa Spiaka, swalı lake la pili kuhusu mkakati wa kuweza kuongeza thamani ni kweli tuna mkakati wa kwanza kama nilivyosema kwenye kuongeza tija na uzalishaji ili kuweza kuwavutia wafanyabiashara na wawekezaji wa ndani wan je kuja kuweka viwanda vidogo, vyta kati na vikubwa baada ya uhakaika wa upatikanaji wa malighafi.

Mheshimiwa Spika, mkakati wa kwanza ni kuendelea kuongeza shughuli za utafiti ili kuja na mbegu ya minazi ambayo itawenza kukinzana na mabadiliko ya tabia nchi na huu ugonjwa uliokuwepo ili wananchi hawa wakazalishie nazi nyingi zaidi.

Mheshimiwa Spika, mkakati wa pili ni kutoa elimu kwa wakulima kwa ajili ya kuchanganya mazao mbalimbali kwenye mashamba ya minazi kama miembe, michungwa na mazao mengine ili kupunguza gharama za uzalishaji na kuongeza kipato kwa wakulima hao.

Mheshimiwa Spika, pia tunaendelea kuwaelimisha wananchi waache kutegemea ile minazi ambayo iliyokuwa walirithi kutoka kwa mababu zao sasa hivi tunawahimiza kupanda mbegu mpya ili wawe na minazi mipyä ambayo italeta tija na uzalishaji mkubwa itaenda kuongeza kipato chao.

**SPIKA:** Asante Wizara ya Maji Mheshimiwa Mchungaji Innocent Bilakwate.

Na. 107

### **Mradi wa Maji wa Vijiji 57-Kyerwa**

**INNOCENT S. BILAKWATE** aliuliza:-

Usanifu na upembuzi wa kina wa mradi wa maji wa vijiji 57 Wilayani Kyerwa umekamilika muda mrefu. Je, ni lini utekelezaji wa mradi huo utaanza ili wananchi wa Kyerwa waweze kupata maji safi na salama?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo lililoshangiliwa sana Mheshimiwa Naibu Waziri maji.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako naomba nitoe pole kwa wananchi wa Mkoa wa Tanga kwa kuondokewa na kipenzi chetu aliyekuwa Mbunge Mheshimiwa Omary Nundu Mwenyezi Mungu ailaze mahala pema roho yake peponi.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate, Mbunge wa Jimbo la Kyerwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wialya ya Kyerwa ni mojawapo ya wilaya zinazounda Mkoa wa Kagera na kwa sasa hali ya upatikanaji wa huduma ya maji imefika asilimia 45.6 kutokana na asilimia ya upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama kuwa Serikali iliamua kubuni mradi mkubwa utakaoweza kuhudumia wananchi zaidi ya 232,000 walioko kwenye vijiji 57 kutoka kwenye chanzo kimoja ambacho ni Ziwa Rushwa kando na Mto Kagera. Kazi hii alipewa mtaalam mshauri *Don Consult* na aliweza kukamilisha kazi hiyo mwaka 2018.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya usanifu pamoja na makisio ua utekelezaji wa mradi huo ni shilingi bilioni 144.

Baada ya kupitia garama hizo, Serikali imeamua kupitia upya usanifu huo ili kujiridhisha na mfumo wa ujenzi uliopendekezwa na garama za ujenzi wa mradi huo. Serikali imeamua kuchukua hatua na uamuzi huo kutokana na uzoefu ulipatikana kuwa baadhi ya miradi mikubwa imekuwa na garama kubwa bila kuzingatia uhalisia wa teknolojia inayopendekezwa na pia uwezo wa uendeshaji wa jamii husika.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo wakati taratibu hizo zinaendelea, Serikali kwa upande wake inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kutekeleza mradi huo kwa kadri mapitio ya usanifu yatakavyoonesha na utatekelezwa kwa awamu. Kwa kuanza, mwaka wa fedha 2019/2020, Serikali imetenga shilingi billioni moja zitakazoanza kutekeleza mradi huo kwa awamu kwenye vijiji vya Mkiyonza, Nshunga, Milambi, Mkombozi, Rukurajjo, Nyabikurungo na Nyaruzumbura. Hivyo, Serikali inamuomba Mheshimiwa Mbunge kuwa mvumilivu wakati Serikali inaendelea kukamilisha mapitio ya usanifu kwa lengo la kuanza kutekeleza mradi huo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Innocent Bilakwate swali la nyongeza.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwanza niipongeze Serikali kwa juhudini ambazo zinaendelea kuwapatia wananchi wa Jimbo la Kyerwa maji na napongeza kwa ajili ya mradi wa Rutunguru, Kaisho na Isingiro ambao mkandarasi alisimamishwa lakini mradi huu umeanza, naipongeza Serikali.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza Mheshimiwa Waziri alipofika Kyerwa tulikaa na kukubaliana mradi huu utakapoanza uweze kwenda kwenye Kijiji cha Kagenyi ambacho tumejenga hospitali ya wilaya, lakini kwenye vijiji ambayo mmevieleza Kijiji cha Kagenyi hakipo. Ninaomba Mheshimiwa Waziri unihakikishie hospitali yetu ya wilaya ambayo iko kwenye Kijiji cha Kagenyi itapelekewa maji? (Makof)

Mheshimiwa Spika, swalii la pili kuna mradi unaoendelea kwenye Kata ya Mabera lakini kumekuwepo na ucheleweshwaji wa kulipwa mkandarasi na sasa hivi anadai zaidi ya milioni 150. Mheshimiwa Waziri ni lini mkandarasi huyo atalipwa ili mradi huu uweze kukamilika na wananchi wa Kata ya Mabera waweze kupata maji safi na salama? (*Makofii*)

**SPIKA:** Majibu ya swalii hilo muhimu Mheshimiwa Naibu Waziri Maji tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, kiukweli naomba nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Mbunge ni mionganini mwa Wabunge ambaao ni wachapakazi na ni wapiganaji hususan maendeleo ya wananchi wake. Kikubwa binafsi nimekwenda na Mheshimiwa Waziri amekwenda kuhusu suala la huu utekelezaji wa mradi huu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, sasa nachotaka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kutokana na jitihada kubwa ambazo amezifanya ujenzi wa hospitali ile kubwa sisi kama Wizara ya Maji hatutokuwa kikwazo, namhakikishia kijiji kile tutakipelekea huduma hii ya maji.

Mheshimiwa Spika, lakini kuhusu swalii lake la pili tuna mraii ambaao tunautekteleza katika Kata ya Mabira, mradi takribani milioni 586, upo asilimia 80 ambaao unatekelezwa na mkandarasi ambaye anaitwa Vumwe *Company Ltd* anadai takribani milioni 137. Nataka nimhakikishie ndani ya mwezi huu tutalipa fedha ile ili mradi ukamilike na wananchi waweze kupata huduma ya maji na mimi nipo tayari kwenda kuufungua kuambatana na Mheshimiwa Mbunge.

**SPIKA:** Mheshimiwa Steven Masele nilikuona uliza swalii lako tafadhali.

**MHE. STEPHEN J. MASELE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swalii la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa mradi wa KASHUWASA wa kutoa maji Ziwa Victoria kuleta katika Mji wa Shinyanga na Kahama. Katika mradi ule vijiji vyote vinavyopitia pembezoni mwa bomba hilo vilipaswa kuunganishwa na maji ya Ziwa Victoria. Sasa Mheshimiwa Naibu Waziri alipofanya ziara na Mheshimiwa Makamu wa Rais alituahidi kutupatia pesa katika vijiji vya Bugwandege, Kata ya Ibadakuli, vijiji vya Mwanubi Kata ya Kolandoto, Chibe katika Kijiji cha Mwakalala pamoja na Kijiji cha Ihapa ambapo tank kubwa la Kashuwasa limejengwa pale lakini wananchi wale hawajapatiwa maji.

Swali langu ni kwamba, sasa ni lini zile pesa alizoahidi zitakuja na ili wananchi wale waweze kupatiwa maji kama alivyoahidi? (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Maji tafadhalii.

#### **NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:**

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Mbunge Masele kwa kazi kubwa ambayo anaifanya. Kiukweli kama Serikali tunatambua Mkoa wa shinyanga ni moja ya maeneo yalikuwa na changamoto kubwa sana ya maji na Serikali ikawekeza fedha kwa ajili ya kuyatoa maji Ziwa Victoria na kuyapeleka katika Mji wa Shinyanga.

Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge ni kweli viro baadhi ya vijiji ambavyo havina maji na jukumu la kuwapatia maji ni jukumu letu sisi Wizara ya Maji. Ni muombe Mheshimiwa Mbunge tukutane sasa haraka na wataalam wetu ili tuangalie namna ya kuweza kutekeleza ahadi hiyo ambayo tuliahidi, ahsante sana.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kwa sababu ya muda swali la mwisho tutalipangia muda wakati mwingine.

Sasa twende kwenye matangazo, leo tuna mambo mengi kidogo. Kwanza ni watambue wageni walioko katika

Jukwaa la Spika, nikianza na wageni saba ambao nitaomba wasimame naye ni Askofu wa Dayosisi ya Mpwapwa Dkt. Jacob Chimeledya, Mkurugenzi wa Maendeleo ya Dayosisi Albert Galahenga, Mganga Mfawidhi wa St. Lukes Kituo cha Afya, Edwin Kiula, Meneja Habari Energia Limited Michael Endo, Karibuni sana. (*Makoff*)

Meneja Matukio David Marealle huyu ni wa Energia Limited, Mwenyekiti wa Vijana wa Dayosisi Paschal Chisonjela, na Katibu wa Vijana wa Dayosisi Sadoki Mjilima, ahsante. Naomba tena msimame wote saba pamoja na baba askofu. Waheshimiwa Wabunge wageni wetu hawa wakiongozwa na Baba Askofu wa Dayosisi ya Mpwapwa ambaye pia ni Askofu Mkuu Mstaafu wa Kanisa la Anglikana Tanzania nzima. Ni kwamba Dayosisi ya Mpwapwa imeandaa matembezi ya hisani kwa ajili ya kuchangisha fedha za ujenzi na upanuzi wa wodi na ununuzi wa vifaa kwa ajili ya kituo cha afya kule Mpwapwa Makao Makuu ya Dayosisi kinachoitwa St. Lukes.

Siku ya matembezi ni kesho kutwa tarehe 14 siku ya Jumamosi kuanzia saa kumi na mbili na nusu asubuhi kuanzia pale Jamhuri Stadium hadi Nyerere *Square*. Ruti sio ndefusana ikizingatia hasa ninyi Wabunge ili iwe ni ruti ambayo ni *user friendly*. Matembezi haya yatakayoongozwa na Wabunge wenye we wa Mpwapwa Mheshimiwa George Simbachawene Waziri na Mheshimiwa Seneta George Lubeleje yanawaalikeni Waheshimiwa Wabunge wote kuweza kwenda kushiriki na spika atakayapokea pale Nyerere *square*. (*Makofi*)

Wabunge wote mnaalikwa na mnaombwa kushiriki na wananchi wa Dodoma hapa mjini wanaombwa sana kushiriki katika matembezi haya kesho kutwa kuanzia saa kumi na mbili na nusu asubuhi. *T-shirt* za matembezi zinauzwa katika eneo letu la Bunge hapo nje kwa hiyo Mheshimiwa Baba Askofu amekuja hapa na timu yake kuwaombeni sana kesho kutwa asubuhi tujunge katika matembezi haya kuunga mkono jambo hili jema la ujenzi na upanuzi wa Kituo cha Afya cha St. Lukes. Baba Askofu karibu sana pamoja na timu

yako Waheshimiwa Wabunge tunaombwa tushiriki kesho kutwa. Ahsanteni sana na karibuni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, pia kwenye Jukwaa la Spika, nina wageni kutoka kule Kongwa yupo diwani wa Kata ya Iduo, yupo Diwani wa Kata ya Iduo ndugu Valentino Seng'unda, karibu Mheshimiwa Diwani. Mwenyekiti wa Kijiji cha Suguta Shabani Athuman, Mwenyekiti wa CCM Suguta Yona Chadibwa, Mjumbe Emma Nyoni, karibu sana Emma umekuja aaah! Leo? Ahsante sana. Mwenyekiti wa Kitongoji Suguta Amon Mbwembwe na Mwenyekiti wa Kitongoji mwingine Jailos Machaka, karibuni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na wageni wa Waheshimiwa Wabunge ambao tuna wageni wanne wa Mheshimiwa Stella Ikupa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughullkia masuala ya Watu Wenyewe Ulemavu, kutoka kampuni ya BF Suma wakiongozwa na ndugu Easter Elisante, karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni wawili wa Mheshimiwa Jumaa Aweso Naibu Waziri Maji na Umwagiliaji kutoka Pangani Mkoa wa Tanga ambao ni ndugu Kayanda Ibrahim na ndugu Shabani Shehe, karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni watatu wa Mheshimiwa Ally Ungando Mbunge wa Kibiti ambao ni wapiga kura wake kutoka huko ndugu Daniel Motera, Ally Ismail na Yusuph Kilonga, karibuni sana. (*Makofi*)

Mgeni wa Mheshimiwa Dastun Kitandula ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Yetu *Microfinance Bank*, Altemious Milinga, wageni 4 wa Mheshimiwa Zainab Mwamwindi ambao ni ndugu zao kutoka Mkoa wa Iringa wakiongozwa na Hamis Halifa, karibuni wanyalukolo. (*Makofi*)

Wageni 18 wa Mheshimiwa Dkt. Dalali Kafumu ambao ni Wenyevitii wa CCM kata na madiwani 2 kutoka Igunga Mkoa wa Tabora wakiongozwa na Mwenyekiti wao

Mheshimiwa Masaba Gwitogwa, karibuni sana. Ninyi mnakuja bila kupiga hodi ni namna gani, karibuni sana watu wa Igunga. (*Makofi*)

Wageni saba wa Mheshimiwa Juma Nkamia ambaao ni wakutubi kutoka Ndaki ya Maktaa ya Kitivo cha Sayansi ya Mawasiliano wakiongozwa na ndugu James Mambo, karibuni sana. Kiswahili bana kinakuwa kila siku sasa wanafika mahali kinakuwa kigumu hata kwa waswahili wenyewe sijui ndaki ndio kitu gani. (*Makofi*)

Wageni nane wa Mheshimiwa Mussa Hassan Mussa ambaao ni viongozi na Makada wa Chama cha Mapinduzi kutoka Amani- Zanzibar akiongozwa na Katibu wa Siasa na Uenezi Ndugu Maulid Khamis, karibuni sana wageni wetu kutoka Zanzibar karibu sana. Japo Mheshimiwa Mussa hayupo lakini tupo naye na anachapa kazi hapa Bungeni. (*Makofi*)

Wageni saba wa Mheshimiwa Angelina Malembeka ambaao ni ndugu zake kutoka Zanzibar na Dar es Salaam wakiongozwa na ndugu Ibrahim Mbuzi. (*Makofi*)

Wageni wawili wa Mheshimiwa Shally Raymond kutoka Jumuiya ya Mtakatifu Brigita Medeli ya Jijini Dodoma ndugu Anna Siriwa na ndugu Regina Siriwa, wale pale karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni 81 wa Mheshimiwa Joel Makanya ambaao ni wanafunzi 69 na walimu 12 kutoka Shule ya Sekondari ya Buigiri ya hapa Dodoma wakiongozwa na Mkuu wa Shule hiyo Mwalimu Dominick Sulumo, karibuni sana watoto wazuri. Waheshimiwa Wabunge Buigiri ni hapo njiani mnapopita kuelekea Gairo hapo katikati hapo, mmependeza kweli watoto, hongereni sana. (*Makofi*)

Mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Rashid Chuachua ambaye ni rafiki yake kutoka Kibaha Mkoa wa Pwani Mwalimu Said Ngani, karibu sana.

Mgeni wa Mheshimiwa Gibson Ole Meiseyeki ambaye ni jamaa yake kutoka Chuo Kikuu cha Teofilo Kisanji Jijini Mbeya ndugu Ezekiel Meliary, karibu sana. (*Makofi*)

Wageni 12 wa Mheshimiwa Suzana Mgonokulima ambao ni kutoka Manispaa ya Iringa waliongozwa na Mwenyekiti wao ndugu Debora Chacha, karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni wawili wa Mheshimiwa Martin Msuha kutoka jijini Dar es Salaam ndugu Ombeni Orok na ndugu Omary Sawa karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni wawili wa Mheshimiwa Saada Mkuya ambao ni ndugu zake kutoka Bergen Norway ndugu Ghania Salum na ndugu Wahida mohammed karibuni sana. (*Makofi*)

Mgeni wa Mheshimiwa Ally Keissy ambaye ni mtoto wake kutoka Jijini Dar es Salaam ndugu Rahma Radhia Kisuo, mtoto wa Mheshimiwa Keissy! Karibu sana mzee yupo hapa anachapa kazi. (*Makofi*)

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge walishangilia sana)*

Waheshimiwa Wabunge acheni jicho pembe. Wageni wa Mheshimiwa Koshuma ambao ni ndugu zake kutoka Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na baba mkwe wake ndugu Simon Msumba, ahsante sana. (*Makofi*)

- (a) save as provided for under subsection (2), take photos, pictures, videos or images of corpses, dead persons, victims of crimes or gruesome incidents; or
- (b) intentionally and without authority, use any form of communication to share pictures, videos or photos of corpses, dead persons, victims of crimes or gruesome incidents.

(2) The provision of subsection (1) shall not apply to taking of photos, pictures, videos or images of corpses, dead persons, victims of crimes or gruesome incidents for the purposes of-

- (a) criminal investigations;
- (b) burial ceremonies, in the case of corpses and dead persons; or
- (c) any other purposes as may be permitted by the police officer or other authorised officer.

(3) A person who contravenes the provisions of this section commits an offence and on conviction is liable to a fine of not less than one million shillings or to imprisonment for a term of not less than one year or to both."

- R:** In Clause 68 by deleting the proposed paragraph (e) and substituting for it the following:
- (e) notwithstanding any other written law to the contrary, be the highest authority in matters relating to labour mobility in the Service."
- S:** In Clause 72 by-
- (a)deleting the word "Ministry" appearing in paragraph (a) and substituting for it the word "Division"; and
  - (b)deleting the word "Ministry" appearing in paragraph (b) and substituting for it the word "Director".
- T:** In Clause 74 by deleting the proposed definition of the term "Ministry" appearing in paragraph (c) and substituting for it the following:
- "Director" means the Director responsible for social security within the Ministry for the time being responsible for social security matters; and
- "Division" means the division responsible for social security within the Ministry for the time being responsible for social security matters;".
- U:** In Clause 76 by deleting the word "Ministry" appearing in the proposed section 4 and substituting for it the word "Division".
- V:** In Clause 77 by deleting the word "Ministry" wherever it appears in the proposed section 5 and substituting for it the word "Division".
- W:** In Clause 87 by deleting the words "Representative from the Ministry" appearing in paragraph (b) and substituting for them the words "word "Director".
- X:** In Clause 88 by deleting the word "Minster" and substituting for it the word "Minister".
- Y:** By deleting Clause 89 and substituting for it the following:
- |                                 |  |
|---------------------------------|--|
| "Amendmen<br>t of section<br>40 | <b>89.</b> The principal Act is amended in section 40 by deleting the words "The Bank may direct the Authority to" appearing in subsection (2)" and substituting for them with the words "The Director may." |
|---------------------------------|--|

**Z:** By deleting Clause 90 and substituting for it the following:

"Amendmen  
t of section  
41

- 90.** The principal Act is amended in section 41, by-
- (a) deleting the words "the Authority may, with the approval of the Board" appearing in subsection (1) and substituting them the words "the Minister may"; and
  - (b) deleting the word "Authority" wherever it appears in subsections (2) and (4) and substituting for it the word "Minister"."

**AA:** In Clause 92, by-

- (a) adding immediately after paragraph (a) the following:
  - "(b) deleting the words "within thirty days of receipt of the written application made under subsection (1)" appearing in subsection (1);
- (b) renaming paragraph (b) as paragraph (c);
- (c) adding immediately after paragraph (c) as renamed the following:
  - "(d) adding immediately after subsection (3) the following:
    - "(4) Every scheme shall establish an internal mechanism for handling members complaints before they are referred to the Division for review."".

**BB:** In Clause 97 by-

- (a) deleting the word "and" appearing in the heading to the proposed Part X;
- (b) deleting the word "Ministry" appearing in the proposed sections 61(b)(ii) and substituting for it the word "Division";
- (c) deleting Clause 63; and
- (d) deleting the proposed section 67 and substituting for it the following:

"Provision  
regarding  
employees

**67.-**(1) Employees or staff of the Authority who are necessary for the purposes of the Ministry, government institutions or departments shall, subject to laws and procedures governing public service, be transferred to public offices on such terms and conditions not less favourable than those applicable to them before the transfer.

(2) Every employee or staff of the Authority whose service is not transferred to a public office shall be paid terminal benefits in accordance with the applicable laws and regulations governing the terms and conditions of his service immediately before the termination.

(3) An employee or staff who is deemed to be employed or transferred to a public office shall continue to be a member of a statutory, voluntary pension or any other superannuation scheme in accordance with the laws and regulations governing the scheme."

**CC** In Clause 100 by adding a word "or" at the end of subsection (2)(a)(i).

:

Dodoma,  
....., 2019

**ALK**  
*AG*

**SPIKA:** Hoja imetolewa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali na imeungwa mkono. Tunakushukuru sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Prof. Adelardus Kilangi. Sasa baada ya mtoe hoja, namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria Ndogo ambao ndio walichambua Muswada huu wa Serikali, Mheshimiwa Mtemi Andrew Chenge, tafadhali. (*Makofii*)

**MHE. ANDREW J. CHENGE – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO:** Mheshimiwa Spika, tarehe 4 Septemba, 2019 wakati wa kikao cha pili cha Mkutano wa Kumi na Sita wa Bunge, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali (Na. 6) wa Mwaka 2019 (*the Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.6) Bill 2019*) ulisomwa Mara ya Kwanza Bungeni, baada ya hapo, Mheshimia Spika aliagiza masharti ya kanuni ya 84 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo ya Januari 2016 na kupeleka Muswada huo kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo.

Mheshimiwa Spika, naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa Kamati iliujadili Muswada huo kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni za Kudumu za Bunge hususan Sehemu ya Nane inayohusu masharti ya jumla kuhusiana na kutungwa sheria.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 86 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 6) ya Mwaka 2019 (*the Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.6) Bill, 2019*).

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza masharti ya Kanuni ya 84 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilikutana na Serikali katika ukumbi Na. 9 ulioko jengo la Utawala katika Ofisi za Bunge hapa Jijini Dodoma mnamo tarehe 5 Septemba, 2019 ili kupokea maelezo ya Serikali kuhusu Muswada husika. Katika kikao hicho, mtoe hoja Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali alijulisha Kamati kuwa

Muswada huu unakusudia kufanya marekebisho katika sheria tisa ili kuondoa upungufu ambao umebainika wakati wa utekelezaji wa sheria hizo kwa lengo la kuongeza ufanisi kwa taasisi zinazosimamia utekelezaji wa sheria hizo.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya Serikali yalionesha kuwa Muswada wa Sheria wa Marekebisho Mbalimbali unapendekeza kufanya marekebisho katika sheria tisa kama ilivyoainishwa kwenye Muswada ulio mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupokea maelezo hayo, Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya 84 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge na kutuma mialiko na kutoa matangazo ya kuwaalika wadau mbalimbali wafike mbele ya Kamati kwa lengo la kuisaidia Kamati katika uchambuzi wa Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, kwa mialiko hiyo, Asasi ya Kiraia ya Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania (*Tanzania Women Lawyers Association - TAWLA*) ilifika mbele ya Kamati na kutoa maoni yao. Napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru kwa dhati wadau hao kwa ushirikiano wao na Bunge lako Tukufu ambao kwa nyakati tofauti waliwasilisha maoni yao kuisaidia Kamati kuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumzia masuala ya awali katika utangulizi wa taarifa hii, napenda kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu maoni ya kamati ambayo yametokana na maelezo ya Serikali pamoja na uchambuzi wa Kamati katika sehemu na ibara mbalimbali za Muswada na ambayo kwa sehemu kubwa yamezingatiwa na Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchambuzi wa Muswada Kamati ilipitia na kufanya uchambuzi wa ibara zote 100 za Muswada na vifungu vyote vya sheria vinavyopendekezwa kurekeblishwa. Wakati wa majadiliano na Serikali, Kamati ilipendekeza marekebisho katika baadhi ya sehemu za Muswada (*parts*) ambayo kwa ujumla yamekubaliwa na

Serikali kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali la marekebisho ya Serikali ambalo litagawiwa kwa Waheshimiwa Wabunge. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia masharti ya kanuni ya 84 fasili ya (3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilimshauri ipasavyo mtoa hoja. Naomba kutoa taarifa kuwa ushauri huo kama nilivyosema, utawasilishwa katika jedwali la marekebisho.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini jumla ya ibara tisa na imetoa mapendekezo ya kiuandishi ambayo ni maeneo tisa ambayo yalikuwa na dosari mbalimbali. Ibara hizo ni Ibara ya 6, 8, 12, 13, 18, 26, 30, 66 na 88 na imetoa mapendekezo yake ambayo yote yamekubaliwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya marekebisho ya msingi pamoja na kubaini dosari za kiuandishi, pia Kamati ilibaini baadhi ya Ibara za Muswada kuwa na dosari zinazohitaji marekebisho ya msingi ili kuwezesha sheria hizi kuleta mantiki iliyokusudiwa na kurahisisha utekelezaji wake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kamati inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Huduma za Maji Sura ya 414 kama ifuatavyo:-

(i) Kufuta Kifungu kipyaa cha 6(2) kinachoanzishwa na Ibara ya 6 ya Muswada, ambacho kinatoa nafasi kwa mkosaji kufikishwa Mahakamani wakati kosa lake limeshafifilishwa (*compounded*). Lengo la mapendekezo haya ni kuweka wajibu kwa Mamlaka kutompeleka mkosaji Mahakamani pale ambapo kosa lake limeshafifilishwa. Aidha, msingi wa mapendekezo haya unazingatia ukweli kwamba, dhana ya kufililisha *to compound* makosa ni makubaliano kati ya mtuhumiwa na chombo chenye mamlaka, ambapo mtuhumiwa anakiri kwa maandishi kufanya kosa au makosa husika na kukubali kulipa kiasi cha fedha alichotakiwa kulipa kwa makubaliano ya kutofikishwa Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Vivuko, (Sura ya 173) kama ifuatavyo:-

(i) Kurekebisha kwa kuongeza adhabu inayopendekezwa katika Ibara ya 18 inayofuta na kuandika upya kifungu kipyga cha 12 (3) kinachoweka adhabu ya faini isiyopungua shilingi elfu hamsini na isiyozidi shilingi laki tano au kifungo kisichozidi miezi sita. Msingi wa mapendekezo ya Kamati ni kuzingatia ukweli kwamba zipo shughuli kama vile ulipuaji wa baruti zinazoweza kusababisha madhara makubwa katika eneo linatumwi na vivuko.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Michezo ya Kubahatisha (Sura ya 41) kama ifuatavyo:-

(i) Kurekebisha Ibara ya 23 inayoanzisha Kifungu kipyga cha 9(A), kwa kuweka utaratibu wa kisheria (*Due process*) utakaoitaka Bodi ya Michezo ya Kubahatisha kuzingatia wakati wa kufanya upekuzi, kukamata na kutaifisha mashine zinazotumika kuchezesha michezo ya kubahatisha bila ya kukiuka haki za wachezesaji wa michezo hiyo. Lengo la mapendekezo haya ni kuondoa uwezekano wa matumizi mabaya ya mamlaka yanayoweza kusababisha usumbufu mkubwa kwa wachezesaji wa mashine za michezo ya kubahatisha na pia kuhakikisha misingi ya haki inafuatwa na kuzingatiwa.

(ii) Kufanya marekebisho ya Ibara ya 26 ya Muswada inayohusiana na dhana ya *performance bond*, ili kuweka neno lenye maana inayokusudiwa na kifungu husika.

(iii) Marekebiso yafanyike katika Kifungu cha 51 (3) kinachopendekezwa chini ya Ibara ya 29 kiboreshwe kwa kuongeza maneno '*in consultation with the minister*' katikati ya neno *may na make*. Msingi wa mapendekezo ya Kamati ni kuhakikisha Waziri mwenye dhamana anahuishwa katika mchakato wa ukusanyaji ada na ushuru.

(iv) Ibara ya 32 ya Muswada kwa kufuta neno *Septemberna* badala yake kuweka neno *after 31<sup>st</sup> December*. Lengo ni kuhakikisha marekebisho yanayopendekezwa yaendane na Sheria ya Ukaguzi wa Hesabu za Umma (*The Public Audit Act*).

(v) Kurekebisha Kifungu cha 33 kwa kufuta maneno *above the age of eighteen years*ili kosa la kuruhusu mtoto kuingia maeneo yanayochezeshwa michezo ya kubahatisha liweze kumhusu mtu yejote pasipo kujali suala la umri.

(vi) Kurekebisha Ibara ya 34 inayopendekeza kurekebisha Kifungu cha 72 (2) kwa kuweka adhabu chini ya Kifungu hicho. Uchambuzi wa Kamati umebaini adhabu inayopendekezwa katika kifungu hiki imeweka kiwango cha chini tu cha adhabu ya faini, *shall on conviction be liable to a fine of not less than one million shillings* bila kuweka kiwango cha juu yaani ukomo. Kama ilivyo itakuwa sahihi kabisa kwa Mahakama kutoa adhabu yoyote zaidi ya shilingi milioni moja kwenye kosa hilo. Pendekezo hili lina lengo la kuzuia matumizi mabaya ya kifungu hiki.

(vii) Kufanya marekebiso katika Ibara ya 35 inayopendekeza kuanzisha Kifungu kidogo cha (4), kwa kuongeza maneno *and gaming system* katikati ya neno *device* na *used*. Lengo la mapendekezo haya ni kupanua wigo kwa Bodi Kutafisha vifaa vya michezo ya kubahatisha visivyokidhi masharti ya sheria ambavyo vinapatikana katika aina mbalimbali za michezo ya kubahatisha.

(viii) Kufanya marekebiso katika Ibara ya 36 inayopendekeza kuanzisha Kifungu kipyaa cha 86 B(2) kwa kukiandika upya, kwa kuwa kinakosa baadhi ya maneno hivyo kutoleta maana iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapendekeza marekebiso katika Ibara ya 38 ya Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1 ya sheria za nchi inayorekebisha Kifungu cha 54 kama ifuatavyo:-

(i) Kuweka utaratibu wa kisheria ili majukumu yaliyoainishwa katika vifungu vidogo nya (2), (3) na (4) yatekelezwe na Katibu Mkuu baada ya kuidhinishwa na Waziri. Msingi wa pendekezo ya kumhusisha Waziri kutoa idhini ya kwa Katibu Mkuu wa Wizara husika kutekeleza majukumu ya Bodi ya Wakurugenzi ambayo bado hajiateuliwa, unatokana na ukweli kwamba Waziri ndiye mwenye dhamana ya kisera na msimamizi wa majukumu ya Wizara na vyombo vyote vilivyo chini yake.

(ii) Sheria iweke ukomo wa muda wa utekelezaji wa majukumu hayo. Lengo la pendekezo la Kamati ni kuhakikisha kuwa hakuna ucheleweshaji wa uundwaji wa Bodi za Wakurugenzi kwa kuzingatia sheria za nchi.

(iii) Kuweka Kifungu kinachoweka kinga kwa Katibu Mkuu wa Wizara kwa maamuzi aliyoyatoa kwa nla njema wakati wa utekelezaji wa majukumu ya Bodi. Lengo ni kumlinda Katibu Mkuu kwa maamuzi aliyoyafanya kwa nia njema.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapendekeza marekebisho katika Ibara ya 66 ya Sheria ya Kanuni za Adhabu (Sura ya 16) inayoanzisha Kifungu kipyaa cha 162(1) kuhusu makosa ya kusambaza picha za watu waliofariki au waathirika wa matukio mbalimbali kama vile ya uhalifu, ajali au matukio ya kutisha. Mapendekezo ya Kamati katika Ibara hii ni katika maeneo yafuatayo:-

(i) Kufanya marekebisho katika aya ya (a) kwa kuongeza picha za video na kuweka dirisha (*proviso*) katika aya hiyo kwa madhumuni ya kuruhusu upigaji picha katika baadhi ya matukio kama vile, kwenye mazishi yaliyoruhusiwa na ndugu wa marehemu, upigaji picha kwa ajili ya kutoa taarifa kwa vyombo nya ulinzi na usalama au kwa ajili ya matumizi ya ushahidi wa kielektroniki.

Mheshimiwa Spika, lengo la mapendekezo ni kubainisha matukio ambayo yanaweza kuruhusiwa kupigwa

picha. Aidha ni kwa kuzingatia ukweli kwamba, maudhui ya Kifungu kinachopendekezwa yanaweza kuondoa uhuru wa watu binafsi pale panakuwa na matukio binafsi kama vile misiba, kuingilia uhuru wa kazi za kawaida za Wanahabari na Waandishi wa Habari pamoja na masuala ya matumizi ya picha kama ushahidi wa kielektroniki.

(ii) Kufanya marekebisho katika aya (b) kwa kuongeza kosa la usambazaji wa picha za video za matukio yanayotajwa katika Kifungu hiki na kuongeza maneno *without permission from a Police Officer or any other lawful authority* mwishoni mwa aya hii. Lengo la mapendekezo ya Kamati ni kuhakikisha kuwa Kifungu kinazungumzia aina zote za picha iwe ni kosa kuzisambaza kwa mujibu wa kifungu hiki.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapendekeza marekebisho kufanyika katika Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Hifadhi ya Jamii (Sura ya 135) kama ifuatavyo:-

(i) Kurekebisha Ibara ya 72 kwa kufuta neno *Ministry* na badala yake kuweka neno linalopendekezwa *respective authority*. Kamati inaona kuwa, mapendekezo ya muswada ya kuhamishia majukumu ya iliyokuwa ya Mamlaka ya Udhibiti na Usimamizi wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwenye Wizara inayohusika na Masuala ya Hifadhi ya Jamii hauko sahihi, kwani utaratibu wa mgawanyo wa majukumu ya Wizara yoyote ni kwa mujibu wa Hati Idhini ya Rais na si vinginevyo.

(ii) Kuhusu Ibara ya 76, Kamati inashauri kwamba sheria itamke kuwa masuala ya Sera na usimamizi wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii yatakuwa chini ya Waziri mwenye dhamana na masuala ya Hifadhi ya Jamii. Msingi wa mapendekezo ya Kamati ni kuweka wazi namna ya kusimamia sera, uendeshaji na usimamizi wa sekta hifadhi ya jamii nchini.

(iii) Kufuta Ibara ya 77 na badala yake marekebisho yafanyike ili sheria itamke kuwa masuala ya sera

na usimamizi wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii yatakuwa chini ya Waziri mwenye dhamana na masuala ya hifadhi ya jamii. Lengo ni kuweka wazi usimamizi wa masuala ya sera na sekta ya hifadhi ya jamii hapa nchini.

(iv) Sheria iweke ufanuzi kuhusu namna itakavyosughulikia watumishi wanaotoka katika mamlaka inayovunjwa (*Social Security Regulatory Authority*), kwa kuwa lbara ya 97 ya Muswada imeyaweka masuala ya watumishi hao kwa ujumla jumla tu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua nia njema ya Serikali kupitia mapendekezo ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani kuhusu misamaha wa kodi hiyo kwa miradi inayotekelizwa na Serikali yenye au itakayotekelizwa na Serikali kwa fedha za Washirika wa Maendeleo inayohusisha mikataba ya misaada au mikataba ya mikopo itakayoingiwa baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mabenki au Taasisi za fedha za nje kwa mikopo ya masharti ya kibiashara au masharti nafuu.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa, Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani inampa mamlaka Waziri wa Fedha ya kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani pale ambapo kuna mikataba baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya nchi nyingine unaotoa msamaha wa kodi hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 6(2) cha Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani kinazuia kutoa msamaha wa kodi hiyo hata kwa miradi inayotekelizwa na Serikali yenye. Aidha, katazo hili linajumuisha pia miradi ya Serikali inayotekelizwa kwa fedha za mikopo ya masharti ya kibiashara na masharti nafuu kutoka katika mabenki na taasisi za fedha za nje. Zuo hili limeleta changamoto ya kukwamisha utekelezaji au ucheleweshaji wa utekelezaji wa miradi mingi ya Serikali kwenye sekta mbalimbali kama vile barabara, maji, ujenzi wa viwanja vya ndege na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hii, kwa vile itawezesha miradi mingi inayofadhiliwa kwa njia mbalimbali ikiwemo mikopo ya masharti ya kibiasara au masharti nafuu, kuweza kupata msamaha wa kodi na hivyo kuondoa vikwazo na ucheleweshaji wa utekelezaji wa miradi ya Serikali usio wa lazima. Hata hivyo, kwa kuwa pendekezo hili litanufaisha tu...

Mheshimiwa Spika, narudia, hata hivyo kwa kuwa pendekezo hili litanufaisha tu miradi itakayoanza kutekelezwa katika siku za usoni baada sheria hii kuanza kutumika, wasiwasi wa Kamati ni kwa miradi ambayo tayari imeshaanza kutekelezwa na ambayo kwa masharti ya mikataba yake inataka msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani utolewe na Serikali.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya jumla. Kamati ilibaini masuala mbalimbali ya jumla ambayo ni muhimu yakaboreshwe kwa lengo la kuleta ufanisi kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika,

KWA KUWA, Kamati imebaini kuwepo kwa mapungufu kadhaa katika udhibiti na usimamizi wa michezo ya kubahatisha nchini.

NA KWA KUWA, mapungufu hayo ya kiusimaizi kwa michezo ya kubahatisha kunaweza kuwa na madhara katika nguvu kazi ya vijana hapa nchini na shughuli nyingine endelevu kama vile kilimo.

HIVYO BASI, Kamati inashauri kuwa Serikali ikamilishe mchakato wa uundaji wa mfumo wa kielektroniki wa kudhibiti michezo ya kubahatisha ili kuongeza mapato ya Serikali na papo hapo kulinda vijana ambao ni nguvu kazi ya Taifa hili.

(b) Mheshimiwa Spika,

KWA KUWA, mara kwa mara Serikali imekuwa ikileta Bungeni mapendekezo ya kutoa misamaha ya kodi kwa baadhi ya miradi mbalimbali inayotekelzeza hapa nchini.

NA KWA KUWA, misamaha hiyo imesaidia kwa kiasi kikubwa kufanikisha miradi mbalimbali kutekelezeka kwa tija kubwa.

HIVYO BASI, Kamati inashauri kuwa ni vema Serikali ikaja na mapendekezo ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa namna au kwa njia itakayowezesha kukwamua miradi mbalimbali iliyoanza kutekelezwa ambayo kwa masharti ya mikataba yake inataka msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani utolewe na Serikali.

(c) Mheshimiwa Spika,

KWA KUWA, Serikali inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Kanuni za Adhabu (Sura ya 16) kwa kulifanya kuwa kosa la jinai tendo la kupiga picha na kusambaza katika jamii.

HIVYO BASI, Kamati inashauri kwamba pamoja na nia nzuri ya Serikali kuleta marekebisho haya, mamlaka zinazohusika zitoe elimu zaidi kwa umma kuhusu madhara ya usambazaji wa picha za kutisha za matukio mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, hitimisho. Kwa mara nyingine naomba nikushukuru sana wewe kwa kutoa kibali ili Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo iweze kuufanya uchambuzi Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, naomba kumtambua na kumshukuru Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Jenista Mhagama; Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Prof. Adelardus Kilangi; Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango; Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji; Naibu Mawaziri wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano,

Mheshimiwa *Eng.* Atashasta Nditiye; na Mheshimiwa Elias Kwandikwa; Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Jumaa Aweso; pamoja na Watendaji wote wa Serikali na Watumishi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ushirikiano wao wa dhati waliounesha mbele ya Kamati wakati wa uchambuzi wa Muswada huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati inatambua na kumshukuru kila Waziri na Watendaji wote waliofika mbele ya Kamati kwa lengo la kuisaidia Kamati kukamilisha kazi yake kwa ufanisi mkubwa na kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee kabisa naomba niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Sheria Ndogo kwa weledi na umahiri wao walliouonesha wakati wa kuchambua Muswada huu na hatimaye kutoa mapendekezo ya msingi ya kuuboresha. Naomba Majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge hususan Katibu wa Bunge Ndugu Stephen Kagaigai kwa uongozi thabiti ambao umerahisisha utendaji kazi wa Kamati. Aidha, namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Gerald Magili, Mkurugenzi Msaidizi wa Kitengo cha Huduma za Kisheria Bungeni, Ndugu Leocardo Kapongwa, Mwanasheria wa Bunge Ndugu Prudence Rweyongeza na Mwanasheria Msaidizi wa Bunge, Ndugu Maria Mdulugu, Makatibu wa Kamati Ndugu Angela Shekifu, Ndugu Stanslaus Kagisa, Ndugu Mkuta Masoli pamoja na Msaidizi wa Kamati Ndugu Paul Chima waliofanikisha kazi ya uchambuzi na uratibu wa shughuli za Kamati kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo na kukamilisha taarifa hii kwa wakati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

MAONI NA USHAURI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE  
YA SHERIA NDOGO KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA  
MAREKEBISHO YA SHERIA MBALIMBALI (NA.6) WA MWAKA  
2019 (*THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS)*)  
*(NO.6) BILL, 2019* KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI

---

1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, tarehe 4 Septemba, 2019, wakati wa Kikao cha Pili cha Mkutano wa Kumi na Sita wa Bunge, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbali mbali Na.6 wa Mwaka 2019 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.6) Bill, 2019*] ulisomwa mara ya kwanza Bungeni. Baada ya hapo, Mheshimiwa Spika alizingatia masharti ya Kanuni ya 84(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 na kuupeleka Muswada huo kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo. Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa, Kamati iliujadili Muswada huo kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni za Kudumu za Bunge hususan Sehemu ya Nane inayohusu masharti ya Jumla kuhusiana na kutunga Sheria.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha Maoni na Ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo Kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbali mbali (Na.6) wa Mwaka 2019 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.6) Bill, 2019*), kwa mujibu wa Kanuni ya 86 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza masharti ya Kanuni ya 84(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilikutana na Serikali katika **Ukumbi Na.9** uliopo Jengo la Utawala katika Ofisi za Bunge Dodoma, mnamo tarehe 5 Septemba, 2019 ili kupokea maelezo ya Serikali kuhusu Muswada husika. Katika kikao hicho, Mtoa Hoja alijulisha Kamati kuwa, Muswada huu

unakusudia kufanya marekebisho katika Sheria Tisa (9) ili kuondoa upungufu ambao umebainika wakati wa utekelezaji wa Sheria hizo kwa lengo la kuongeza ufanisi kwa Taasisi zinazosimamia utekelezaji wa Sheria hizo.

**Mheshimiwa Spika**, Maelezo ya Serikali yalionesha kuwa, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 6) wa Mwaka 2019 unapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria Tisa (9) zifuatazo:

- i) Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Huduma za Maji (Sura ya 414) (*The Energy and Water Utilities Regulatory Authority Act, (Cap. 414)*);
- ii) Sheria ya Vivuko (Sura ya 173) (*Ferries Act, (Cap. 173)*);
- iii) Sheria ya Michezo ya Kubahatisha (Sura ya 41) (*The Gaming Act, (Cap. 41)*);
- iv) Sheria ya Tafsiri ya Sheria (Sura ya 1) (*The Interpretation of Laws Act, (Cap. 1)*);
- v) Sheria ya Usafiri Majini (Sura ya 165) (*Merchant Shipping Act, (Cap. 165)*);
- vi) Sheria ya Kanuni za Adhabu (Sura ya 16) (*The Penal Code, (Cap. 16)*);
- vii) Sheria ya Utumishi wa Umma (Sura ya 298) (*The Public Service Act, (Cap. 298)*);
- viii) Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Hifadhi ya Jamii (Sura ya 135) (*The Social Security (Regulatory Authority) Act, (Cap. 135)*); na
- ix) Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (Sura ya 148) (*The Value Added Tax Act, (Cap. 148)*).

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kupokea maelezo hayo, Kamati ilizingatia masharti ya **Kanuni ya 84(2)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge na kutuma mialiko na kutoa matangazo ya kuwaalika wadau mbalimbali wafike mbele ya Kamati kwa lengo la kuisaidia katika Uchambuzi wa Muswada huu.

**Mheshimiwa Spika** Kwa mialiko hiyo, Asasi ya kiraia ya Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania (*Tanzania Women Lawyers Association – TAWLA*) ilifika mbele ya Kamati na kutoa maoni yao. Napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru kwa dhati Wadau hao kwa ushirikiano wao na Bunge lako tukufu, ambao kwa nyakati tofauti, waliwasilisha maoni yao kuisaidia Kamati kuboresha Muswada huu.

## 2.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kuzungumzia masuala ya awali katika utangulizi wa Taarifa hii, napenda kuwasilisha mbele ya Bunge lako tukufu maoni ya Kamati ambayo yametokana na maelezo ya Serikali pamoja uchambuzi wa Kamati katika Sehemu na Ibara mbalimbali za Muswada na ambayo kwa sehemu kubwa yamezingatiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

### 2.1 Maelezo ya Jumla kuhusu uchambuzi wa Muswada

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipitia na kufanya uchambuzi wa Ibara zote Mia Moja (100) na vifungu vyote vya Sheria vinavyopendekezwa kurekebishwa.

**Mheshimiwa Spika**, kwa maoni hayo, Kamati ilipendekeza marekebisho katika baadhi ya sehemu za Muswada huu, ambayo kwa ujumla yamepokelewa kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho lililowasiishwa na Serikali.

## 2.2 Maoni na Mapendekezo kwa kila Ibara

**Mheshimiwa Spika**, ili kulisaidia Bunge lako tukufu kuititia ibara kwa ibara na kufanya uamuzi bora wa Kibunge, Kamati ilifanya mapitio ya ibara zote Mia Moja (100) katika Sehemu Kumi za Muswada huu. Matokeo ya hatua hii kwenye ngazi ya Kamati ni pamoja na kubaini baadhi ya ibara za Muswada huu kuwa zinatafaa kuboreshwa zaidi. Kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 84 (3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilimshauri ipasavyo Mtoa hoja.

Naomba kutoa taarifa kuwa, ushauri huo umechangia kuwasilishwa kwa Jedwali la Marekebisho lililowasilishwa na Mtoa Hoja. Kwa ujumla mapendekezo ya Kamati ni kama ifuatavyo:-

### 2.2.1 Mapendekezo ya Marekebisho ya kiuandishi

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini jumla ya ibara Tisa (9) zenyе dosari mbalimbali za kiuandishi, ambazo ni Ibara ya **6, 8, 12, 13, 18, 26, 30, 66** na **88** na kutoa mapendekezo yake ambayo yote yamekubaliwa na Serikali, kama yalivyoainishwa katika Jedwali la Marekebisho.

### 2.2.2 Mapendekezo ya Marekebisho ya Msingi

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kubaini dosari za kiuandishi, pia Kamati ilibaini baadhi ya ibara za Muswada kuwa na dosari zinazohitaji marekebisho ya msingi ili kuziwesha Sheria hizi kuleta mantiki iliyokusudiwa na kurahisisha utekelezaji wake kama ifuatavyo:-

- a) **Mheshimiwa Spika**, Kamati inapendekeza marekebisho katika **Sheria ya Mamlaka ya Udhhibiti wa Nishati na Huduma za Maji, (Sura ya 414)** kama ifuatavyo:-

- i) Kufuta Kifungu kipywa cha **6(2)** kinachoanzishwa na **Ibara ya 6** ya Muswada, ambacho kinatoa nafasi kwa mkosaji kufikishwa mahakamani wakati kosa lake limeshafifilishwa. Lengo la mapendekezo haya ni kuweka wajibu kwa Mamlaka kutompeleka mkosaji mahakamani pale ambapo kosa lake limeshafifilishwa.
- Aidha, msingi wa mapendekezo haya unazingatia ukweli kwamba, dhana ya kufililisha makosa ni makubaliano kati ya mtuhumiwa na chombo chenye mamlaka, ambapo mtuhumiwa anakiri kwa maandishi kufanya kosa au makosa husika na kukubali kulipa kiasi cha pesa alichotakiwa kulipa kwa makubaliano ya kutofikishwa mahakamani.
- b) **Mheshimiwa Spika**, Kamati inapendekeza marekebisho katika **Sheria ya Vivuko, (Sura ya 173)** kama ifuatavyo:-

- i) Kurekebisha kwa kuongeza adhabu inayopendekezwa katika **Ibara ya 18** inayofuta na kuandika upya kifungu kipywa cha **12.-(3)** kinachoweka adhabu ya faini isiyopungua shilingi elfu hamsini na isiyozidi shilingi laki tano au kifungo kisichozidi miezi sita.

Msingi wa mapendekezo ya Kamati kufanya marekebisho ni kuzingatia ukweli kwamba zipo shughuli kama vile ulipuaji wa baruti zinazoweza kusababisha madhara makubwa katika eneo linatumwiwa vivuko.

c) **Mheshimiwa Spika**, Kamati inapendekeza marekebisho katika **Sheria ya Michezo ya Kubahatisha (Sura ya 41)** kama ifuatavyo:

- i) Kurekebisha **Ibara ya 23** inayoanzisha kifungu kipya cha **9A**, kwa kuweka utaratibu wa kisheria (*Due process*) kwa Bodi ya Michezo ya Kubahatisha wa jinsi ya kufanya upekuzi, kukamata na kutaifisha mashine zinazotumika kuchezesha michezo ya kubahatisha bila ya kufuata taratibu zilizowekwa na Bodi ya Michezo ya Kubahatisha.

Lengo la mapendekezo haya ni kuondoa uwezekano wa matumizi mabaya ya mamlaka yanayoweza kusababisha usumbu mkubwa kwa wachezeshaji wa mashine za michezo ya kubahatisha, na pia kuhakikisha misingi ya haki inafuatwa.

- ii) Kufanya marekebisho ya **Ibara ya 26** inayohusiana na “*Perfomance bond*”, ili kuweka neno lenye maana inayokusudiwa na kifungu husika kinachopendekezwa.
- iii) Marekebiso yafanyike katika **kifungu cha 51 (3)** kinachopendekezwa chini ya **Ibara ya 29** kiboreshwwe kwa kuongeza maneno “*in consultation with the minister*” katikati ya neno “*may*” na “*make*”. Msingi wa mapendekezo ya kamati ni kuhakikisha Waziri anashiriki katika mchakato wa ukusanyaji ada na ushuru.
- iv) Ibara ya 32 kwa Kufuta neno “*September*” na badala yake kuweka neno “*after 31<sup>st</sup> December*”. Lengo ni kuhakikisha marekebiso

yanayopendekezwa yaendane na Sheria ya Ukaguzi wa Hesabu za Umma (*Public Audit Act*).

- v) Kurekebisha **kifungu cha 33** kwa kufuta maneno "*above the age of eighteen years*" ili kosa la kuruhusu mtoto kuingia katika maeneo yanayochezwa michezo ya kubahatisha liweze kumhusu mtu yejote pasipo kujali suala la umri.
- vi) Kurekebisha **Ibara ya 34** inayopendekeza kurekebisha **kifungu cha 72 (2)** kwa kuweka adhabu chini ya kifungu hicho. Uchambuzi wa Kamati umebaini adhabu inayopendekezwa katika kifungu hiki imeweka kiwango cha chini tu cha adhabu ya faini ("*shall on conviction be liable to a fine of not less than one million shillings*") bila kuweka kiwango cha juu/ mwisho.

Lengo la kuweka ukomo wa juu wa adhabu ni kuondoa uwezekano wa matumizi mabaya ya kifungu hiki (*abuse of discretion*).

- vii) Kufanya marekebiso katika **Ibara ya 35** inayopendekeza kuanzisha **kifungu kidogo cha (4)**, kwa kuongeza maneno "*and gaming system*" katikati ya neno *device* na *used*. Lengo la mapendekezo haya ni kupanua wigo kwa Bodii kutaifisha vifaa vyaa michezo ya kubahatisha visivyokidhi masharti ya Sheria ambavyo vinapatikana katika aina mbalimbali za michezo ya kubahatisha.
- viii) Kufanya marekebiso katika **Ibara ya 36** inayopendekeza kuanzisha kifungu

kipywa cha **86B-(2)** kwa kukiandika upya, kwa kuwa kinakosa baadhi ya maneno hivyo kutoleta maana iliyokusudiwa.

- d) **Mheshimiwa Spika**, Kamati inapendekeza marekebisho katika **Ibara ya 38 ya Sheria ya Tafsiri ya Sheria (Sura ya 1)** inayorekebisha **Kifungu cha 54** kama ifuatavyo:-

i) Kuweka utaratibu wa kisheria ili majukumu yaliyoainishwa katika vifungu vidogo vya **(2), (3) na (4)** yatekelezwe na Katibu Mkuu baada ya kuidhinishwa na Waziri.

Msingi wa pendekezo kumhusisha Waziri kutoa idhini ya kutekeleza majukumu ya Bodi ya Wakurugenzi ambayo bado hajateuliwa, unatokana na ukweli kwamba Waziri ndie mwenye dhamana ya Kisera na msimamizi wa majukumu ya Wizara na vyombo vyote vilivyo chini yake.

ii) Sheria iweke ukomo wa muda wa utekelezaji wa majukumu hayo. Lengo la pendekezo la Kamati ni kuhakikisha kuwa hakuna ucheleweshaji wa uundwaji wa Bodi kwa kuzingatia Sheria za nchi.

iii) Kuweka Kifungu kinachoweka kinga kwa Katibu Mkuu wa Wizara kwa maamuzi aliyoyatoa kwa nia njema wakati wa utekelezaji wa majukumu ya Bodi. Lengo ni Kumlinda Katibu Mkuu kwa maamuzi aliyoyafanya kwa nia njema.

- e) **Mheshimiwa Spika**, Kamati inapendekeza marekebisho katika **Ibara ya 66 ya Sheria ya Kanuni za Adhabu (Sura ya 16)** inayoanzisha

**Kifungu kipy cha 162.-**(1) kuhusu makosa ya kusambaza picha za watu waliofariki au waathirika wa matukio mbalimbali ya uhalifu, ajali au matukio ya kutisha. Mapendekezo ya Kamati katika Ibara hii ni katika maeneo yafuatayo:-

- i) Kufanya marekebisho katika aya ya **(a)** kwa kuongeza picha za video na kuweka **proviso** katika aya hii kwa madhumuni ya kuruhusu upigaji picha katika baadhi ya matukio kama vile, kwenye mazishi yaliyoruhusiwa na ndugu wa marehemu, upigaji picha kwa ajili ya kutoa taarifa kwa vyombo vya ulinzi na usalama au kwa ajili ya matumizi ya ushahidi kielektroniki.

Lengo la mapendekezo ni kubainisha matukio ambayo yanaweza kuruhusiwa kupigwa picha. Aidha ni kwa kuzingatia ukweli kwamba, maudhui ya kifungu kinachopendekezwa yanaweza kuondoa uhuru wa watu binafsi pale panakuwa na matukio binafsi kama vile misiba, kuingilia uhuru wa kazi za kawaida za wanahabari pamoja na masuala ya matumizi ya picha kama ushahidi wa kielektroniki

- ii) Kufanya marekebisho katika **aya (b)** kwa kuongeza kosa la usambazaji wa picha za video za matukio yanayotajwa katika kifungu hiki na kuongeza maneno **without permission from a police officer or any other lawful authority** mwishoni mwa aya hii.

Lengo la mapendekezo ya Kamati ni, kuhakikisha kuwa kifungu kinazungumzia

aina zote za picha iwe ni kosa kuzisambaza kwa mujibu wa kifungu hiki.

f) **Mheshimiwa Spika**, Kamati inapendekeza marekebisho kufanyika katika **Sheria ya Mamlaka ya Udhiliti wa Hifadhi ya Jamii (Sura ya 135)** kama ifuatavyo:-

(v) Kurekebisha **Ibara ya 72** kwa kufuta neno "*ministry*" na badala yake kuweka neno "*respective authority*". Kamati inaona kuwa, Mapendekezo ya Muswada ya kuhamishia majukumu yaliyokuwa ya Mamlaka ya Udhiliti wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwenye Wizara inayohusika na Masuala ya Hifadhi ya Jamii hauko sahihi, kwani Utaratibu wa mgawanyo wa majukumu ya Wizara ni kwa mujibu wa Hati Idhini ya Rais na sio Sheria.

(vi) Kuhusu **Ibara ya 76**, Kamati inashauri kwamba Sheria itamke kuwa masuala ya Sera na Usimamizi wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii yatakuwa chini ya Waziri mwenye dhamana na masuala ya Hifadhi ya Jamii. Msingi wa mapendekezo ya Kamati ni kuweka wazi namna ya kusimamia Sera, Uendeshaji na usimamizi wa sekta hifadhi ya jamii nchini.

(vii) Kufuta **Ibara ya 77** na badala yake marekebisho yafanyike ili Sheria itamke kuwa masuala ya Sera na Usimamizi wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii yatakuwa chini ya Waziri mwenye dhamana na masuala ya Hifadhi ya Jamii. Lengo ni kuweka wazi usimamizi wa masuala ya Sera na sekta hifadhi ya jamii.

(viii) Sheria iweke uafafanuzi kuhusu namna itakavyoshughulikia watumishi wanaotoka katika Mamlaka inayovunja (SSRA), kwa kuwa **Ibara ya 97** imeyaweka masuala ya watumishi hao kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua nia njema ya Serikali kupitia mapendekezo ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani kuhusu msamaha wa kodi kwa baadhi ya miradi inayotekelizwa na Serikali yenye we au inayotekelizwa na Serikali kwa fedha za Washirika wa maendeleo kupitia Mikataba ilioingiwa kati ya Serikali yetu na benki au taasisi za fedha za nje kwa mikopo ya masharti ya kibiashara au masharti nafuu.

Hivi sasa, kifungu cha 6(2) cha Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani kinazuia kutoa msamaha wa kodi hiyo **hata kwa miradi inayotekelizwa na Serikali yenye we**. Aidha, katazo hili linahusu pia miradi ya maendeleo inayotekelizwa na Serikali kwa fedha za mikopo ya masharti ya kibiashara na masharti nafuu kutoka katika benki na taasisi za fedha za nje. Zuo hili limeleta changamoto ya kukwamisha miradi mingi kwenye sekte mbalimbali kama vile barabara, maji, viwanja vyta ndege n.k.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hii, kwa vile itawezesha miradi mingi ya maendeleo inayofadhiliwa kwa njia mbalimbali ikiwemo, mikopo yenye masharti ya kibiashara au masharti nafuu kuweza kupata msamaha wa kodi na kutekelezeka bila vikwazo. Kwa kuwa pendekezo hili litanufaisha miradi itakayoanza kutekelezwa baada sheria hii kuanza kutumika, wasiwasi wa Kamati ni kwa miradi ambayo imeshaanza kutekelezwa na ambayo kwa masharti ya mikataba yake inataka msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani utolewe.

## 2.2.3 Mapendekezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini masuala mbalimbali ya jumla ambayo ni muhimu yakaboreshwe kwa lengo la kuleta ufanisi wa kutosha kwenye sekta husika kama ifuatavyo:-

### a) **Mheshimiwa Spika**,

**Kwa kuwa**, Kamati imebaini kuwepo kwa mapungufu kadhaa katika udhibiti na usimamizi wa michezo ya kubahatisha nchini, na kwa kuzingatia ukweli kwamba sekta hiyo inahusisha idadi kubwa ya watanzania wengi hasa vijana ambaao ni nguvu kazi ya Taifa,

**Na kwa kuwa**, mapungufu hayo ya kiusimaizi kwa michezo ya kubahatisha kunaweza kuwa na kuathiri katika nguvu kazi ya taifa na shughuli nyininge endelevu kama vile kilimo,

**Hivyo basi**, Kamati inashauri kuwa Serikali ikamilishe mchakato wa uundai wa mfumo wa kielektroniki wa kudhibiti michezo ya kubahatisha ili kuongeza mapato na kulinda vijana ambaao ni nguvu kazi ya Taifa.

### b) **Mheshimiwa Spika**,

**Kwa kuwa**, mara kwa mara Serikali imekuwa ikileta Bungeni mapendekezo ya misamaha ya kodi kwa baadhi ya miradi mbalimbali inayotekelizwa hapa nchini

**Na kwa kuwa**, misamaha hiyo imesaidia kwa kiasi kikubwa kufanikisha miradi mbalimbali kutekelezeka kwa tija kubwa.

**Hivyo basi**, Kamati inashauri kuwa ni vema Serikali ije na marekebisho ya Sheria ya Kodi

ya Ongezeko la Thamani kwa lengo la kukwamua miradi mbalimbali iliyoanza kutekelezwa ambayo kwa masharti yake inataka msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani.

c) **Mheshimiwa Spika,**

**Kwa kuwa**, Serikali inapendekeza marekebisho katika **Sheria ya Kanuni za Adhabu (Sura ya 16)** kwa kuweka kosa la upigaji na usambazaji wa matukio ya ajali na yale yakutisha.

**Na Kwa kuwa**, inaonesha kwamba kumekuwepo na matukio mengi ya usambazaji wa picha za matukio mbalimbali ya aina hiyo yanayofanywa na wananchi kwa kutokujua madhara yake.

**Hivyo basi**, Kamati inashauri kwamba pamoja na nia nzuri ya Serikali kuleta marekebisho haya, mamlaka zinazohusika zitoe elimu zaidi kwa umma kuhusu madhara ya usambazaji wa picha za matukio mbalimbali.

### 3.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, kwa mara nyingine naomba nikushukuru sana wewe kwa kutoa kibali ili Kamati ya Sheria Ndogo iweze kuufanya kazi Muswada huu.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kumtambua na kumshukuru, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Mhe. Jenesta Mhagama - Mb, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Prof. Adelardus Kilangi, Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe. Dr. Philip Mpango - Mb, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe. Ashatu Kijaji - Mb, Manaibu Waziri wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhe. Eng. Atashasta Nditiye - Mb na

Mhe. Elias Kwandikwa - Mb, Naibu Waziri wa Maji, Mhe. Juma Aweso - Mb, pamoja, na Watendaji wote wa Serikali na watendaji wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ushirikiano wao wa dhati ulioiwezesha Kamati kukamilisha Uchambuzi wa Muswada huu kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa namna ya pekee kabisa naomba niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Sheria Ndogo kwa weledi na umahiri wao walionunesha wakati wa kuchambua Muswada huu na hatimaye kutoa Mapendekezo ya msingi ya kuuboresha. **Naomba Majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu rasmi za Bunge (*Hansard*)**.

1. Mhe. Andrew John Chenge, Mb - **Mwenyekiti**
2. Mhe. William Mganga Ngeleja, Mb - **Makamu**  
**Mwenyekiti**
3. Mhe. Aida Joseph Khenani, Mb
4. Mhe. Khamis Mtumwa Ali, Mb
5. Mhe. Rashid Ali Abdallah, Mb
6. Mhe. Mlinga Goodluck Asaph, Mb
7. Mhe. John John Mnyika, Mb
8. Mhe. Halima James Mdee, Mb
9. Mhe. Elibariki Emmanuel Kingu, Mb
10. Mhe. Ridhiwani Jakaya Kikwete, Mb
11. Mhe. Sabreena Hamza Sungura, Mb
12. Mhe. Sadifa Juma Khamis, Mb
13. Mhe. Anne Kilango Malecela, Mb
14. Mhe. Zainab Athman Katimba, Mb
15. Mhe. Salome Wycliffe Makamba, Mb
16. Mhe. Twahir Awesu Mohammed, Mb
17. Mhe. Taska Restituta Mbogo, Mb
18. Mhe. Mary Deo Muro, Mb
19. Mhe. Easter Lukago Midimu, Mb
20. Mhe. Catherine Nyakao Ruge, Mb
21. Mhe. January Yusuf Makamba, Mb

**Mheshimiwa Spika**, nawashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge hususan Katibu wa Bunge **Ndg. Stephen Kagaigai** kwa Uongozi thabiti ambao umerahisisha utendaji kazi wa Kamati. Aidha, namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Gerald Magili, Mkurugenzi Msaidizi wa Kitengo cha Huduma za Kisheria Bungeni, Ndg. Leocardo Kapongwa, Mwanasheria wa Serikali Mkuu, Ndg. Prudens Rweyongeza, Mwanasheria Msaidizi wa Bunge, Ndg. Maria Mdulugu, Makatibu wa Kamati Ndg. Angela Shekifu, Ndg. Stanslaus Kagisa, Ndg. Mkuta Masoli, pamoja na Msaidizi wa Kamati Ndg. Paul Chima waliofanikisha kazi ya Uchambuzi na uratibu wa shughuli za Kamati kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo na kukamilisha taarifa hii kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha.

Andrew J. Chenge, Mb  
**MWENYEKITI**  
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO**

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Andrew Chenge, MwenyeKITI wa Kamati ya Sheria Ndogo kwa kutupitisha katika maoni ya Kamati yake kuhusiana na Muswada ulio mbele yetu ambao hoja imetolewa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. (*Makofii*)

Sasa nimuite Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Wizara ya Katiba na Sheria. Mheshimiwa Salome karibu. (*Makofii*)

**MHE. SALOME W. MAKAMBA (MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA):** Mheshimiwa Spika, nakushukuru naomba niwasilishe maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 6 ya mwaka 2019 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments)(No.6) Act, of 2019*).

Mheshimiwa Spika, Sheria hii inawasilishwa chini ya Kanuni ya 86(6) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016. Muswada ulioletwa mbele ya Bunge lako tukufu, unapendekeza marekebisho katika Sheria Tisa. Sheria hizo ni Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Huduma za Maji, Sura ya 414, Sheria ya Vivuko, Sura ya 173, Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, Sura ya 41, Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1, Sheria ya Usafirishaji Majini, Sura ya 165, Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura ya 16, Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 298, Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Hifadhi ya Jamii, Sura ya 135 na Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani itatoa maoni yake haya kama ambavyo imekuwa ikifanya mara zote kwa kutoa mapendekezo ya marekebisho yaliyotolewa na Serikali kwa lengo ya kuyaboresha ili kuwezesha Bunge lako tukufu kutunga sheria bora ambayo itatekelezeka na kurahisisha ufanisi kwa maslahi mapana ya Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Marekebisho ya Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Huduma za Maji (Sura ya 414), Sehemu ya pili ya Muswada ni marekebisho ya sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Huduma za Maji. Kifungu cha 6 cha Muswada kinarekebisha sheria mama kwa kuongeza kifungu kipyga cha 42A kinachohusu mfumo wa kufilisha makosa, kwa maelezo ya kwamba jambo hilo litaepusha mchakato mrefu wa mashitaka hivyo kuokoa gharama na muda na pia kupunguza mlundikano wa kesi.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 6 cha Muswada kinafanya marekebisho ya sheria mama kwa kuingiza kifungu kipyga cha 42A(1) na kinampa mamlaka Mkurugenzi Mkuu wa EWURA kufanya maamuzi ya kufilisha kosa peke yake. Kwa namna ya kifungu hiki kilivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza kwamba Mkurugenzi Mkuu asifanye

maamuzi haya peke yake badala yake ashauriwe na Bodi ya *EWURA* ili kuepusha matumizi mabaya ya madaraka. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Kifungu kidogo cha 42A(ii) kinatoa mamlaka kwa Serikali kupeleka shauri liliolofilishwa mahakamani. Kifungu hiki kinasema nanukuu; “*where an offence is compounded in accordance with subsection (1) and proceedings are brought against the offender for the same offence, it shall be a good defense for the offender to prove to the satisfaction of the Court, that the offence with which the offender is charged has been compounded under subsection (1)*” . Kambi Rasmi ya Upinzani inaona utaratibu huu unaanzisha msingi mpya wa uandishi wa sheria kama siyo kupingana na utaratibu uliozoleka wa uandishi wa sheria.

Mheshimiwa Spika, tunapendekeza kwamba, kifungu kipywa cha 42A(2) kifutwe kwa sababu hakitoi haki na kwa sababu kinaleta utaratibu wa kushitakiwa mara mbili kwa kosa lilelile na hakina mantiki kisheria. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kifungu kidogo cha 42A(3) kinatoa mamlaka kwa Mkurugenzi Mkuu kuongeza riba kwa mtu aliyeshindwa kulipa kiwango kilichotakiwa kulipwa kama ilivyoelekezwa kwenye kifungu cha 42A(2) hapo juu. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona Serikali inataka kutumia njia hii kama moja ya chanzo cha kukusanya mapato badala ya kulea na kukuza sekta ya Biashara nchini. Kwa sababu mtu kushindwa kulipa faini aliyoikiri inaweza kusababishwa na mambo mengi ikiwemo kuzorota kwa biashara, hivyo Kambi Rasmi ya Upinzani ilitegemea Serikali kutoa mwanya kwa mdaiwa kuongezewa muda wa kulipa badala ya kumuongezea riba. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inakubaliana na kifungu cha 42A(4) kuwa mtu atakayeshindwa kulipa deni liliolofilishwa apelekwe mahakamani lakini siyo aongezewe riba. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Marekebisho ya Sheria ya Vivuko, Sura Na. 173, Kifungu cha 18 cha Muswada kinafanya marekebisheso ya kifungu cha 12 cha sheria ya vivuko, kwa kufuta kifungu hicho na kukiandika upya. Kifungu cha 12(A) kinazuia mtu kufanya shughuli yoyote ndani ya eneo la kivuko cha umma.

Mheshimiwa Spika, kifungu hiki cha 12(2) hakitaji shughuli hizo ni zippi hasa, hasa ukizingatia ukubwa na madhara ya shughuli zinazoweza kufanyika katika maeneo ya vivuko vya umma unatofautiana kwa kiasi kikubwa. Kwa mfano Mtu anayeogelea hawezi kuwa na madhara sawa na mtu anayevua kwa kutumia nyavu.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 12(3) kinatoa adhabu kwa mtu atakaye vunja kifungu kidogo cha 12(2) kuwa ni adhabu Isiyopungua elfu hamsini na isiyozidi laki tano au adhabu ya kifungo kisichozidi miezi sita au vyote kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 12(3) kinatoa adhabu hiyo ya mtu atakaye kwenda kinyume na kifungu cha 12(2), wakati huo huo kifungu hicho cha 12(2) hakitaji shughuli husika hivyo kuacha ukakasi katika kifungu hicho. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaishauri Serikali kuja na jedwali la orodha ya shughuli zinazozuiliwa kufanywa na adhabu zake kwa sababu ziko shughuli ambazo madhara yake ni makubwa kulinganisha na makosa mengine katika eneo la feri kwa mujibu wa kifungu cha 12(2). (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Marekebisheso ya Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, Sura ya 41, biashara ya michezo ya kubahatisha imejipatia umaarufu mkubwa katika miaka ya hivi karibuni hususani Ukombe wa Afrika ya Mashariki. Makundi mbalimbali ya vijana yamekuwa wakivutiwa sana na kujishughulisha na michezo hii. Katika Muswada huu wa mapendekezo ya sheria ya michezo ya kubahatisha yaani "*(Gaming Act Cap 41)*" kifungu cha 23 cha Muswada Kilichoongeza kifungu kidogo cha 9A kinazungumzia mamlaka ya Bodi ya michezo ya kubahatisha yaani (*Gaming Board of Tanzania*).

Mheshimiwa Spika, bodi hii imepewa mamlaka makubwa sana ambayo kimsingi ni mamlaka yanayoingilia Taasisi zingine za kiuchunguzi na za kutoa haki kama Polisi na Mahakama. Kifungu hiki kinasema kuwa, nitanukuu *"The Board shall, for the purpose of implementing its functions, have powers to inspect audit, seizure, forfeiture and destroying illegal gaming devices or any other item related or connected directly or indirectly with gaming activities.*

Mheshimiwa Spika, ni hatari sana kuzipa Bodi hizi mamlaka ya kutaifisha au kuharibu mali za watu. Jambo hili la kuzipa Bodi Mamlaka makubwa hivi ni hatari katika hatua nzima za utafutaji haki. Kila mtu ana haki ya kusikilizwa. Endapo Bodi ina mgogoro na mtuhumiwa basi ni wazi kuwa mtuhumiwa huyo atakosa nafasi ya kuitafuta haki yake.

Mheshimiwa Spika, sio tu katika Sheria hii ambapo tumeanza kuona Bodi zikipewa mamlaka haya makubwa hata katika Marekebisho ya Sheria ya Wasanii jambo hili liliijitokeza. Madhara yake ni kuwa wapo wengi watakao ingia katika migogoro ya kisheria na kukosa haki zao kwa kuwa tayari mali zao na utu wao utakuwa umedhalilishwa.

Mheshimiwa Spika, katika kifungu cha 29 cha Muswada kifungu cha 51(2) ambacho kinazungumzia masuala ya utoaji wa leseni katika biashara ya matangazo ya michezo ya kubahatisha. Kifungu hiki kinasema leseni itaweza kutumika kwa kipindi cha miezi sita kuanzia siku leseni inapotolewa.

Mheshimiwa Spika, matangazo ya biashara ni uwekezaji wa muda mrefu. Kitendo cha kuwataka wafanya biashara hao kukata leseni kwa gharama za kodi na tozo kila baada ya miezi sita ni muda mdogo sana kwa mwekezaji kuweza kufaidi uwekezaji alioufanya. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Michezo hii ya kubahatisha ni michezo ambayo inaweza kusababisha uraibu yaani (*addiction*) Kambi Rasmi ya Upinzani inaishauri Serikali kuweka bayana mikakati ya kudhibiti michezo hiyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Marekebisho ya Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura Na. 1 Kifungu cha 38 cha muswada kinachofanya marekebisho ya kifungu cha 54 kwa kukiandika upya, na kuwa kifungu kidogo cha 54(1). Pamoja na mabadiliko hayo, kifungu hiki cha 38 cha Muswada kinapendekeza kuongezwa vifungu vidogo vitatu (3) na hivyo kukifanya kifungu cha 54 kuwa na vifungu 54(1), 54(2), 54(3) na 54(4). Vifungu vyote vitatu vinatalenga kumpatia madaraka Katibu Mkuu anayehusika na Bodi au Wizara kufanya maamuzi ambayo yangefanywa na Bodi husika ikitokea mazingira ya bodi iliyokuwepo imevunjwa.

Mheshimiwa Spika, bodi imemaliza muda wake kisheria na endapo bodi husika haijaundwa kwa mujibu wa sheria. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona marekebisho ya kifungu hiki hayana tija kiutendaji kwa kuwapa Makatibu wakuu wenyewe dhamana na bodi husika au na Wizara ambazo bodi husika zipo kufanya maamuzi kwa niaba ya Bodi. Ikumbukwe kwamba, Bodi hizi zinaanzishwa na sheria mbalimbali na kupewa majukumu ya kufanya kwa mujibu wa sheria. Aidha Bodi hizi zimekuwa zikifanya kazi ikiwemo kusimamia utendaji wa Sekta husika na kufanya maamuzi ya Mashirika au Sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, watendaji katika sekta hizo wako chini ya makatibu wakuu ambao leo kwa mujibu wa marekebisho haya, sasa atakuwa na mamlaka ya kufanya maamuzi kwa niaba ya bodi. Sheria hii endapo itapita kama ilivyo bila kufanyiwa marekebisho, basi itakuwa ni miongoni mwa sheria mbaya kuwahi kutungwa na Bunge lako Tukufu, na jambo hili halitakuwa na afya Kwa ustawi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka haya ambayo sheria inapendekeza kuwapatia Makatibu Wakuu, hayana kikomo na katika hali ya kawaida yanakwenda kuchukua nafasi za Bodi mbalimbali. Inashangaza kwanini hasa tunafikiria kuziondolea mamlaka bodi na kama dhamira ya serikali ni kudhibiti utendaji wa bodi, ni bora sasa kuletwe sheria ya kufuta bodi zote ili majukumu yafanywe na Serikali yenyewe, kuliko kuziweka bodi kama geresha.

Mheshimiwa Spika, Madhara mengine ya mabadiliko haya ni kwamba, sasa bodi hazitaundwa kwa sababu makatibu wakuu wapo na wanaweza kufanya maamuzi kwa niaba ya bodi, au ikitokea jambo ambalo bodi hajakubaliana nalo, basi Serikali itakuwa na njia moja tu, nayo ni kuvunja bodi husika ili katibu Mkuu afanye maamuzi kwa niaba ya bodi. Mabadiliko haya hayawezi kutusaidia kama Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa badala ya kumpatia mamlaka katibu Mkuu kufanya maamuzi kwa niaba ya Bodi husika, Sheria iweke kiwango cha muda wa miezi Mitatu ili kuundwa kwa bodi mpya, tangu bodi iliyokuwepo kumaliza muda wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Ikiwa ni sheria mpya, kipindi cha miezi mitatu tangu kuanza kutumika kwa sheria husika inayoanzisha Bodi hiyo. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona kwamba mamlaka ya Bodи mbalimbali yanapokwa na hivyo Serikali kupitia makatibu wakuu watafanya maamuzi yote na dhana ya bodi kusimamia Sekta husika haitakuwepo na hii itakuwa ni sawa na kuwa na utawala wa kiimra. Ni ushauri wetu kwamba, Serikali izingatie maoni na mapendekezo haya kwa kuweka sheria inayozitaka mamlaka za kuunda Bodи husika, kufanya hivyo ndani ya kipindi cha miezi mitatu ili bodi ziweze kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, Marekebisho ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura Na. 298 kifungu cha 68 cha mswada kinafanya marekebisho ya kifungu cha 4(3) cha Sheria ya Utumishi wa Umma kwa kuongeza kifungu kidogo cha 4(3)(e) kwa kile kinachosemwa kwenye maudhui na sababu za Muswada huu, kuwa ni kumuwezesha katibu Mkuu Kiongozi kuwa na mamlaka ya mwisho ya uhamisho wa watumishi wa umma.

Mheshimiwa Spika, kwa majukumu aliyonayo Katibu Mkuu Kiongozi, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kwamba, kumpatia jukumu la kuwa mamlaka ya mwisho ni kutetea

ukiritimba katika uhamisho wa wafanyakazi wa umma bila sababu za msingi. Tunashauri na kupendekeza mfumo uliokuwa unatumika hapo awali uendelee ili dhana ya kugatua madaraka ionekane pia kwa vitendo. Jambo hili halina tija kwa Taifa isipokuwa kusababisha mlundikano wa majalada kwenye Ofisi ya Katibu Mkuu Kiongozi kwa mambo ambayo hata mamlaka za chini zingweza kufanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 70 cha Muswada kinafanya marekebisho sheria ya utumishi wa umma kwa kuingiza kifungu kipyaa cha 27 kinachompa mamlaka Katibu Mkuu Kiongozi kumsamehe mtumishi wa umma masharti yoyote yanayohusiana na malipo ya mafao ya kustaafu na mafao mengine baada ya ajira kukoma. Kifungu hiki kinakinzana na Sheria ya mifuko ya Hifadhi ya Jamii ambayo tulipitisha hapa mwaka jana 2018 pamoja na Kanuni zake ambazo zinampa Waziri mwenye dhamana mamlaka hayo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**MAONI YA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI, KUHUSU  
MUSWADA WA SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA  
MBALIMBALI NA.6 YA MWAKA 2019 (THE WRITTEN LAWS  
(MISCELLANEOUS AMENDMENTS) (NO.6) ACT, 2019) (Chini  
ya Kanuni ya 86(6) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, toleo  
la Januari, 2016) – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

**A. UTANGULIZI**

1. **Mheshimiwa Spika**, Muswada ulioletwa mbele ya Bunge lako tukufu, unapendekeza marekebisho katika Sheria Tisa. Sheria hizo ni Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Huduma za Maji, Sura ya 414, Sheria ya Vivuko, Sura ya 173, Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, Sura ya 41, Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1, Sheria ya Usafirishaji Majini, Sura ya 165, Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura ya 16, Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 298, Sheria ya Mamlaka

ya Udhibiti wa Hifadhi ya Jamii, Sura ya 135 na Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148.

2. **Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni itatoa maoni yake kama ambayo imekuwa ikifanya mara zote kwa kutoa mapendekezo ya marekebisho yaliyotolewa na Serikali kwa lengo la kuyaboresha ili kuliwezesha Bunge lako tukufu kutunga sheria bora ambayo itatekelezeka kwa urahishi na kwa ufanisi, kwa maslahi mapana ya Tanzania.

B. **MAONI KATIKA MAREKEBISHO YA SHERIA MAHUSUSI**

- i. **Marekebisho ya Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Huduma za Maji** (Sura ya 414)
3. **Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya pili ya muswada ni marekebisho ya sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Huduma za Maji. Kifungu cha 6 cha mswada kinarekebisha sheria mama kwa kuongeza kifungu kipyä cha 42A kinachohusu mfumo wa kufilisha makosa, kwa maelezo ya kwamba jambo hilo litaepusha mchakato mrefu wa mashitaka na hivyo kuokoa gharama na muda na pia kupunguza mlundikano wa kesi.
4. **Mheshimiwa Spika**, kifungu cha 6 cha mswada kinafanya marekebisho ya sheria mama kwa kuingiza kifungu kipyä cha 42A (1) kinampa mamlaka Mkurugenzi Mkuu wa EWURA kufanya maamuzi ya kufilisha kosa peke yake. Kwa namna kifungu hiki kilivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza kwamba Mkurugenzi Mkuu asifanye maamuzi ya kufilisha peke yake badala yake ashauriane na Bodi ya EWURA ili kuепusha matumizi mabaya ya madaraka.
5. **Mheshimiwa Spika**, kifungu kidogo cha 42A (ii) kinatoa mamlaka kwa Serikali kupeleka shauri

lililofifilishwa mahakamani. kifungu hiki kinasema ninanukuu; “**where an offence is compounded in accordance with subsection (1) and proceedings are brought against the offender for the same offence, it shall be a good oofence for the offender to prove to the satisification to the Court, that the offence with which the offender is charged has been compounded under subsection (1)**”

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona utaratibu huu ukianzisha msingi mpya wa uandishi wa sheria kama siyo kupingana na utaratibu uliozoeleka wa uandishi wa sheria. Tunapendekeza kwamba, kifungu kipywa cha 42A (2) kifutwe kwa sababu hakitoi haki kwa sababu kinaleta utaratibu wa kushitakiwa mara mbili kwa kosa lilellile na hakina mantiki yoyote kisheria.

6. **Mheshimiwa Spika**, kifungu kidogo cha 42A (3) kinatoa mamlaka kwa Mkrugenzi Mkuu kuongeza riba kwa mtu aliyeshindwa kulipa kiwango kilichotakiwa kulipwa kama ilivyoelekezwa kwenye kifungu cha 42A(2) hapo juu, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona Serikali inataka kutumia njia kama moja ya chanzo cha kukusanya mapato badala ya kulea na kukuza sekta ya Biashara nchini, kwa sababu mtu kushindwa kulipa faini aliyokiri inaweza kusababishwa na mambo mengi ikiwemo kuzorota kwa biashara, hivyo Kambi Rasmi ya Upinzani ilitegemea Serikali kutoa mwanya kwa mdaiwa kuongezewa muda wa kulipa badala ya kumuongezea riba.
  
7. **Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inakubaliana na kifungu cha 42A (4) kuwa mtu atakayeshindwa kulipa deni lililofifilishwa apelekwe mahakamani **LAKINI** asiongezewe riba.

ii. Marekebisho ya Sheria ya Vivuko, Sura ya 173.

8. **Mheshimiwa Spika**, kifungu cha 18 cha mswada kinafanya marekebisho ya kifungu cha 12 cha sheria mama ya vivuko, kwa kufuta kifungu hicho na kukiandika upya. Kifungu kipyga cha 12(2) kinazuia mtu kufanya shughuli yoyote ndani ya eneo la kivuko cha umma.
9. **Mheshimiwa Spika**, kifungu hiki cha 12(2) hakitaji shughuli hizo ni zippi hasa ukizingatia ukubwa na madhara ya shughuli zinazoweza kufanyika katika maeneo ya vivuko vya umma unatofautiana kwa kiasi kikubwa. Kwa mfano Mtu anayeogelea hawezu kuwa na madhara sawa na mtu anayevua kwa kutumia nyavu.
10. **Mheshimiwa Spika**, kifungu cha 12(3) kinatoa adhabu kwa mtu atakaye vunja kifungu kidogo cha 12(2) kuwa ni adhabu isiyopungua elfu hamsini na isiyozidi shilingi laki tano au adhabu ya kifungo kisichozidi miezi sita.
11. **Mheshimiwa Spika**, kifungu cha 12(3) kinatoa adhabu kwa mtu aliye kwenda kinyume na kifungu cha 12(2), wakati huo huo kifungu cha 12(2) hakitaji shughuli husika na hivyo kuacha ukakasi katika kifungu hicho. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri Serikali kuja na jedwali la orodha ya shughuli zinazozuiliwa kufanya na adhabu zake kwa sababu ziko shughuli ambazo madhara yake ni makubwa kulinganisha na makosa mengine katika eneo la fери kwa mujibu wa kifungu cha 12(2).

iii. Marekebisho ya Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, Sura ya 41

12. **Mheshimiwa Spika**, biashara ya michezo ya kubahatisha imejipatia umaarufu mkubwa katika miaka ya hivi karibuni hususani katika Ukanda wa

Afrika ya Mashariki. Makundi mbalimbali ya vijana yamekuwa wakivutiwa sana na kujishughulisha na michezo hii.

13. **Mheshimiwa Spika**, katika muswada huu wamapendekezo ya sheria ya michezo ya kubahatisha yaani "(Gaming Act Cap 41)" kifungu cha 23 cha Muswada huu kilichoongeza kifungu kidogo cha 9A kinazungumzia mamlaka ya Bodi ya michezo ya kubahatisha yaani (Gaming Board of Tanzania).
14. **Mheshimiwa Spika**, Bodi hii imepewa mamlaka makubwa sana ambayo kimsingi ni mamlaka yanayoingilia taasisi nyingine za kiuchunguzi na zakutoa haki kama polisi na mahakama. Kifungu hiki kinasomeka kuwa "*The Board shall, for the purpose of implementing its functions, have powers to conduct inspection, auditing, seizure, forfeiture and destroying illegal gaming device or any other item related or connected directly or indirectly with gaming activities*"
15. **Mheshimiwa Spika**, ni hatari sana kuzipa Bodi hizi mamlaka ya kutaifisha au kuharibu maliza watu. Jambo hili la kuzipa Bodi Mamlaka makubwa hivi ni hatari katika hatua nzima za utafutaji haki. Kila mtu ana haki ya kusikilizwa. Endapo Bodi ina mgogoro na mtuhumiwa ni wazi kuwa mtuhumiwa huyo atakosa nafasi ya kuitafuta haki yake.
16. **Mheshimiwa Spika**, sio tu katika Sheria hii ambapo tumeanza kuona Bodi zikipewa mamlaka haya makubwa hata katika Marekebisho ya Sheria ya Wasanii japokuwa hili lilijitokeza. Madhara yake ni kuwa wapo wengi watakao ingia katika migogoro ya kisheria na kukosa haki zao kwa kuwa tayari mali zao na utu wao utakuwa umedhalilishwa.
17. **Mheshimiwa Spika**, katika kifungu cha 29 cha Muswada huu kifungu kidogo cha 51 (2) ambacho

kinazungumzia masuala ya utoaji wa leseni katika biashara ya matangazo ya michezo ya kubahatisha. Kifungu hiki kinasema leseni itaweza kutumika kwa kipindi cha miezi sita kuanzia siku leseni ilipotolewa.

**18. Mheshimiwa Spika**, Matangazo ya biashara ni uwekezaji wa muda mrefu. Kitendo cha kuwataka wafanya biashara hao kukata leseni kwa gharama za kodi na tozo kila baada ya miezi sita ni muda mdogo sana kwa mwekezaji kuweza kufaidi uwekezaji aliofanya.

**19. Mheshimiwa Spika**, Michezo hii ya kubahatisha ni michezo ambayo ni inaweza kusababisha uraibu (addiction) Kambi Rasmi ya Upinzani inaishauri Serikali kuweka bayana mikakati ya kudhibiti michezo hiyo!

iv. **Marekebisho ya Sheria ya Tafsiri ya Sheria,**  
**Sura ya 1**

**20. Mheshimiwa Spika**, kifungu cha 38 cha muswada kinachofanya marekebisho kifungu cha 54 kwa kukiandika upya, na kuwa kifungu kidogo cha 54(1). Pamoja na mabadiliko hayo, kifungu hiki cha 38 cha mswada kinapendekeza kuongezwa vifungu vidogo vitatu (3) na hivyo kukifanya kifungu cha 54 kuwa na vifungu vya 54(1), 54(2), 54(3) na 54(4). Vifungu vyote vitatu vinalenga kumpatia madaraka Katibu Mkuu au anayehusika na Bodi na au Wizara kufanya maamuzi ambayo yangefanywa na Bodi husika ikitokea mazingira ya bodi iliyokuwepo imevunjwa, Bodi imemaliza Muda wake kisheria na endapo bodi husika haijaundwa kwa mujibu wa sheria.

**21. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona marekebisho ya kifungu hiki hayana tija kiutendaji kwa kuwapatia Makatibu wakuu wenye dhamana na bodi husika na au wizara ambazo bodi husika zipo kufanya maamuzi kwa niaba ya Bodi husika. Ikumbukwe kwamba, Bodi hizi zinaanzishwa na

sheria mbalimbali na kupewa majukumu ya kufanya kwa mujibu wa sheria.

- 22. Mheshimiwa Spika**, Aidha Bodi hizi zimekuwa zikifanyakazi ikiwemo kusimamia utendaji wa sekta husika na kufanya maamuzi ya mashirika au sekta binafsi. Watendaji katika sekta hizo wako chini ya makatibu wakuu ambao leo kwa mujibu wa marekebisho haya, sasa atakuwa na mamlaka ya kufanya maamuzi kwa niaba ya bodi. Sheria hii endapo itapita kama ilivyo bila kufanyiwa marekebisho, basi itakuwa ni mionganoni mwa sheria mbaya kuwahi kutungwa na Bunge lako Tukufu, na jambo hili halitakuwa na afya Kwa ustawi wa Taifa letu.
- 23. Mheshimiwa Spika**, Mamlaka haya ambayo sheria inapendekeza kuwapatia Makatibu Wakuu, hayana kikomo na katika hali ya kawaida yanakwenda kuchukua nafasi za Bodi mbalimbali. Inashangaza kwanini hasa tunafikiria kuziondolea mamlaka bodi na kama dhamira ya serikali ni kudhibiti utendaji wa bodi, ni bora sasa kuletwe sheria ya kufuta bodi zote nchini ili majukumu yafanywe na serikali yenye, kuliko kuziweka bodi kama geresha. Madhara mengine ya mabadiliko haya ni kwamba, sasa bodi hazitaundwa kwa sababu makatibu wakuu wapo na wanaweza kufanya maamuzi kwa niaba ya bodi, na au likitokea jambo ambalo bodi haijakubaliana nalo, basi Serikali itakuwa na njia moja tu, nayo ni kuvunja bodi husika ili katibu Mkuu afanye maamuzi kwa niaba ya bodi. Mabadiliko haya hayawezি kutusaidia kama Taifa.
- 24. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa badala ya kumpatia mamlaka katibu Mkuu ya kufanya maamuzi kwa niaba ya Bodi husika, Sheria iweke kiwango cha muda wa miezi Mitatu ili kuundwa kwa bodi mpya, tangu bodi iliyokuwepo kumaliza muda wake, ikiwa ni sheria mpya, kipindi

cha miezi mitatu tangu kuanza kutumika kwa sheria husika inayoanzisha Bodi hiyo.

**25. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona kwamba mamlaka ya Bodi mbalimbali yanapokwa na hivyo Serikali kuititia kwa makatibu wakuu watafanya maamuzi yote na dhana ya bodi kusimamia sekta husika haitakuwepo na hii itakuwa ni sawa na kuwa na utawala wa ki imra. Ni ushauri wetu kwamba, Serikali izingatie maoni na mapendekezo haya kwa kuweka sheria inayozitaka mamlaka za kuunda Bodi husika, kufanya hivyo ndani ya kipindi cha miezi mitatu ili bodi ziweze kutekeleza majukumu yote.

v. **Marekebisho ya Sheria ya Utumishi wa Umma,**  
**Sura ya 298**

**26. Mheshimiwa Spika**, kifungu cha 68 cha mswada kinafanya marekebisho ya kifungu cha 4(3) cha Sheria ya Utumishi wa Umma kwa kuongeza kifungu kidogo cha 4 (3) (e) kwa kile kinachosemwa kwenye madhumuni na sababu za Muswada huu, kuwa ni kumuwezesha katibu Mkuu kiongozi kuwa kuwa mamlaka ya mwisho ya uhamisho wa watumishi wa umma.

**27. Mheshimiwa Spika**, kwa majukumu aliyonayo Katibu Mkuu kiongozi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona kwamba, kumpatia jukumu la kuwa mamlaka ya mwisho ni kuleta ukiritimba katika uhamisho wa wafanyakazi wa umma bila sababu za msingi. Tunashauri na kupendekeza mfumo uliokuwa unatumika hapo awali uendelee ili dhana ya kugatua madaraka ionekane pia kwa vitendo. Jambo hili halina tija kwa Taifa isipokuwa kusababisha mlundikano wa majalada kwa Ofisi ya Katibu Mkuu Kiongozi kwa mambo ambayo hata mamlaka za chini zingweza kuyafanya.

28. **Mheshimiwa Spika**, kifungu cha 70 cha mswada kinafanya marekebisho sheria ya utumishi wa umma kwa kuingiza kifungu kipy Cha 27 kinachompa mamlaka Katibu Mkuu kiongozi kumsamehe mtumishi wa umma masharti yoyote yanayohusiana na malipo ya mafao ya kustaaifu na mafao mengine baada ya ajira kukoma. Kifungu hiki kinakinzana na Sheria ya mifuko ya hifadhi ya jamii ya mwaka 2018 pamoja na kanuni zake ambazo zinampa waziri mwenye dhamana mamlaka hayo.

Salome Wycliffe Makamba (Mb)

Kny: **MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI  
BUNGENI  
KATIKA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA**

12 Septemba, 2019

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Makamba kwa maoni hayo. Sasa tunaendelea na uchangiaji, Mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa William Mganga Ngeleja atafuatiwa na Mheshimiwa Sabreena Sungura na Mheshimiwa Zainab Katimba atafuatiwa. Mheshimiwa Ngeleja tafadhali.

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ya kuwa mchangiaji wa kwanza katika Muswada huu ulioko mbele yetu. La kwanza ni kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa namna ambavyo ametuongoza kufikia siku ya leo, lakini zaidi ya hapo nitumie nafasi hii kusema kabisa kwamba naungana na taarifa ya Kamati yetu kama ambavyo imewasilishwa na Mwenyekiti wetu Mtemi Chenge na tunaiunga mkono hoja ya Serikali pamoja na Marekebisho ambayo yamefanyika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Llakini jambo la pili, likiwa ni sehemu ya utangulizi kwa niaba ya Kamati yetu naongezea maneno ya kukushukuru sana wewe Mheshimiwa Spika,

Kamati yetu ya Kudumu ya Sheria Ndogo ni mara ya kwanza inapewa heshima ya kuchambua Muswada kwa asili ya Kamati yetu tumekuwa tukichambua Sheria zingine ambazo zimeshapitishwa na Bunge ama Sheria Ndogo ambazo zinaletwa kwa ajili ya uchambuzi. Lakini tunakushukuru sana kwa heshima uliyotupa na kimsingi Kamati yako iko tayari kuendelea kufanya uchambuzi wa Miswada mbalimbali kwa kadri ambavyo Mwenyezi Mungu atakujalia kuipa majukumu zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tumekutana na Serikali na mimi naungana na Mheshimiwa Mwenyezeki wangu kuipongeza sana Serikali ikiongozwa na Mheshimiwa Jenista Mhahama pamoja na Profesa Kilangi kwa namna ambavyo wametushirikisha kufafanua maeneo ambayo tulikuwa na wasiwasi na matokeo yake ndiyo haya ambapo tunaona kuna jedwali la marekebisho mengi ambayo kimsingi ni maridhiano kati ya Serikali na Kamati yako. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, moja, kabla sijahamia kwenye uchambuzi wa vifungu vya Sheria, ni dakika chache zimepita toka ulipozungumza kati ya maneno makubwa uliyozungumza leo ikiwa ni taarifa ya Mheshimiwa Spika, umetumia fursa ya jukwaa leo kunipongeza mie lakini pia na wenzangu kwa hatua tulioichukua ya kumuomba radhi Mheshimiwa Rais kwa yaliyotokea bila kufungua mjadala nataka niseme na ni kwa sababu wanajua kibinadamu, wote tunajua msamaha siku zote unaleta faraja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, natumia nafasi hii, mimi mwenyewe, lakini pia kwa niaba ya Wapiga kura wa Jimbo la Sengerema kuelezea faraja niliyo nayo ya kupata huo msamaha lakini pia kukushukuru sana kwa namna ambavyo umeliweka, ahsante sana na ninaamini kwamba Mwenyezi Mungu atazidi kumjalia Mheshimiwa Rais, kukujalia wewe, Watendaji Wakuu, Viongozi Wakuu wa Serikali, Makamu Rais pamoja na Waziri Mkuu na Serikali kwa ujumla na sisi kwa nafasi kama Taasisi kuendelea kutimiza majukumu yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Muswada uliowasilishwa kwetu kama alivyosema Mheshimiwa Mwenyekiti ulikuwa unapendekeza marekebisho katika Sheria Tisa, mimi nitapita katika baadhi ya maeneo nikijenga msingi wa kuwashawishi baadhi ya watakaopata nafasi kwa niaba ya Bunge lako kuiunga mkono Serikali kwa sababu maeneo haya mengi yaliyoletwa mbele yetu yamefanyiwa uchambuzi wa kina na tumeelewana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kwanza, naanza kuchangia ni sehemu ya Sheria ya Mamalaka ya Udhibiti wa Nishati na Huduma za Maji, jambo kubwa lililojitekeza hapa ilikuwa ni kuingiza dhana ya ushirikishwaji wa watendaji ambao wako chini ya hii Mamlaka ya Udhibiti *EWURA* zikiwemo Wizara zingine nje ya Wizara ambako Mamlaka inaripoti.

Mheshimiwa Spika, kwa mfumo tuliokuwa nao kwa sasa, tulio nao sasa hivi *EWURA* wanaripoti kiutaratibu kwenye Wizara ya Maji, lakini kuna Wizara zingine ambazo majukumu yake pia yanadhibitiwa na *EWURA* ikiwemo Wizara ya Nishati. Sasa hapa wanaleta dhana ya kuwashirikisha katika baadhi ya mambo, Katibu Mkuu ama Makatibu Wakuu katika Wizara ambazo siyo Wizara ya Mama ambako Mamlaka inaripoti ikiwemo Wizara ya Nishati lakini pia Mawaziri husika katika maeneo haya. Ni wazo zuri, na sidhani kama linahitaji mvutano katika hili kwa ajili ya kuelewana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwenye sehemu ya nne ya Muswada ambao inahusu Marekebisho ya Sheria ya Michezo ya Kubahatisha yako mambo mengi yamezungumzwa. Lakini moja ni kuweka bayana sasa kwamba Kifungu cha 9A kinazungumzia kuwapa fursa Watuhumiwa watakaobainika katika haya makosa ya kufifilisha *compounding offence* ya kujitetea.

Mheshimiwa Spika, hili ni jambo jema, kwa sababu mkishakubaliana kwenda nje ya utaratibu wa kimahakama, ni vyema huyu mtu ambaye unakubali sasa kwamba anaweza kutimiza majukumu yake nje ya mfumo wa

kimahakama basi mpe nafasi ya kujitetea na kujieleza. Kwa hili ni jambo jema na kwa kweli tumelizungumzia, tumelewana na Serikali na imeridhia ushauri ambao Kamati yako imeutoa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine katika eneo hili, eneo hili la mchezo wa kubahatisha lina sura mbili. Upande mmoja ni chanzo cha mapato binafsi kwa wanaochezza lakini biashara kwa wanaochezeshaa na kwa upande mwingine lina ukakasi wa kiimani, yote yamezingatiwa. Ndiyo maana tunasema, kwa namna ambavyo limeletwa na Serikali na tafakari tulioifanya kwa pamoja, hapo tulipofikia ni pazuri na nawashawishi wenzangu tuiunge mkono Serikali. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tano ya Sheria kuna suala la tafsiri ya sharia. Moja katika vifungu ambavyo vinapendekezwa kufanyiwa marekebisho ni cha 54. Nimesikla mjadala utaendelea, nadhani tutaendelea kushauriana vizuri, lakini Serikali imekuja kutufanulia vizuri kwamba Serikali inaleta mabadiliko kwamba kwa kipindi ambacho kitakuwa cha mpito Bodi haijateuliwa basi Makatibu Wakuu wapate nafasi ya kutimiza majukumu ambayo kimsingi yanatekelezwa na Bodi katika taasisi ambazo zinalengwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sasa hapa ni jambo la hekima na busara lakini pia na uhalisia, Serikali ina mambo mengi, tunajua Bodi zina muda wake na nydingi zina muda wa miaka mitatu, lakini hizi sheria wakati mwingine zina *contemplate*, zinatungwa zikijaribu kubashiri hali ambayo inaweza kujitokeza, sasa kama hamjaweka utaratibu mzuri wa ku-*address* changamoto hizo ambazo zinaweza kujitokeza bila kutarajiwa inakuwa shida kidogo katika maamuzi na wakati mwingine maamuzi makubwa yanafanywa. Kwa hiyo, tunaamini kwamba Serikali imekuja na marekebisho haya kwa nia njema, naamini kwamba jambo hili litakwenda vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Saba inahusu marekebisho katika makosa mbalimbali ambayo

yameingizwa lakini kikubwa ambacho tunaipongeza Serikali ni kuridhia ushauri wa Kamati kwamba yako baadhi ya mambo, matukio ya picha ambazo zinazungumzwa hapa, kwa mfano masuala ya misiba, labda unasafiri ukakuta ajali imetokea, unapiga picha lakini lengo lako unataka kutuma taarifa sasa kwenye mamlaka husika, labda kwa *RPC* au Mkuu wa Trafiki ama Mheshimiwa Waziri mhusika, jambo hilo lisiwe kama ni kosa kwa sababu wewe utakuwa unafikisha taarifa kwenye mamlaka husika. Kwa hiyo, hilo ni jambo la kheri na tunaiomba Serikali ilikubali. Tunaomba Waheshimiwa Wabunge tukubaliane katika hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nane inahusu Sheria ya Utumishi wa Umma na kubwa katika hili Katibu Mkuu Kiongozi anafanywa kuwa ndiyo mkubwa, ndiyo mamlaka ya mwisho kabisa katika masuala ya uhamisho pamoja na masuala mengine lakini hili jambo ni kama lilikuwa ni *formality*. Tunafahamu Katibu Mkuu Kiongozi au *Chief Secretary* ndiye mkuu wa nidhamu katika utumishi wa umma, sasa masuala ya uhamisho ni sehemu ya utumishi wa umma. Kwa kweli hili jambo na la lenyewe, nadhani haliwezi kuleta mvutano mkubwa, lilikuwa ni jambo la busara na hekima kukubali kwamba liingizwe katika utaratibu unaopendekezwa na Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo tumeliona ni katika maeneo ya sheria inayohusu Udhibiti wa Hifadhi ya Jamii na hii ni Sura ya 135. Tunaishukuru Serikali, imetafakari, sheria hii kwa kweli inaondoa sasa uwepo wa muundo wa kitaasisi au mamlaka ambayo ilikuwa inaanizishwa katika ile Sheria ya Hifadhi ya Mifuko ya Jamii lakini majukumu yake yanahamia katika Wizara husika.

Mheshimiwa Spika, kubwa katika hili ambalo napenda kulzungumzia ni kwamba mojawapo ya mambo makubwa ambayo yamezungumziwa ni kuhakikisha kwamba fursa ya mlalamikaji yeyote kwa ajili ya fao lolote linalomhusu, halijawekewa ukomo, ukomo umeondolewa, kiasi kwamba sasa kama mtu anaweza kuwa amejisahau, baadaye akabaini kwamba kuna fao lake halijatendewa

haki, hana ukomo wa kuendelea kufuatilia ama kuwasilisha malalamiko yake. Sisi tukaona kwamba ni jambo kubwa kwa sababu lina manufaa kwa wananchi wetu ambao wananaufaika na mifuko hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho kabisa ni hili la kurekebisha Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, ni jambo zito, tumelizungumza sana. Ipo miradi mingi ambayo tunaifadhili wenyewe kwa fedha yetu ya ndani lakini iko miradi mikubwa inafadhiliwa kutokana na fedha za mikopo ya kibiasara, ama mikopo yenye masharti nafuu lakini kwa msimamo wa sheria zetu imekuwa ni kikwazo na kwa sababu Kodi ya Ongezeko la Thamani kimsingi imekuwa ikiongeza gharama za utekelezaji wa miradi hii.

Mheshimiwa Spika, Sasa kwa utaratibu ambao tumeshauriana na Serikali na Serikali tunajua kwamba itakuja itoe ufanuzi wa ziada namna ambavyo tutaikwamua miradi ambayo sasa imeshaanza kutekelezwa, naamini kwamba tutakwenda vizuri na tutapunguza gharama na tutarahisisha utekelezaji wa miradi hiyo na ni kwa manufaa ya Watanzania wote, hili halilengi mradi wowote kwa manufaa ya mtu binafsi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru sana, naunga mkono ya Serikali, naendelea kuwashawishi wenzangu tuiunge mkono Serikali tukatimize majukumu kwa mafufaa ya Watanzania wote. Ahsante sana. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa William Mganga Ngeleja kwa mchango wako. Sasa nimuite Mheshimiwa Sabreena Sungura na Mheshimiwa Zainab Katimba ajiandae. Mheshimiwa Sabreena.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata bahati ya kuchangia Muswada huu ambao umeletwa kwa Hati ya Dharura lakini pia tungependa kuikumbusha Serikali kwamba Miswada hii inayokuja kwa Hati

ya Dharura mara nyingi tunakosa maoni mengi ya wadau. Kwa hiyo, wajitahidi Miswada iwe inakuja kwa njia ya kawaida kuliko Hati ya Dharura. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, binafsi napenda nikushukuru wewe mwenyewe kwa kuleta Muswada huu kwenye Kamati yetu na hivyo kama Kamati kupata *experience* ya kuititia Miswada ya mabadiliko mbalimbali ya sheria za nchi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, napenda nichangie kwenye Ibara ya 6 ya Muswada ambayo inafanya marekebisho na kuongeza kifungu kipyga cha 42A(1)(2)(3) na (4). Kwenye mabadiliko haya ya sheria, tunaambiwa kwamba Mkurugenzi Mkuu atakuwa na mamlaka ambayo amepewa ya kufilisha makosa lakini tunaona kwamba ni vyema basi mamlaka hayo asingeachiwa ye ye peke yake, angeweza kufanya pamoja na Bodl ya *EWURA* ili kupanua wigo na kuondoa *autonomy*. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini suala lingine ni kwamba pale ambapo kosa litakuwa limefifilishwa na baadaye yule mtu hajakubaliana na suala lile akaamua kwenda mahakamani, hapa tunaona kabisa kwamba kutakuwa kuna *offence* moja ambayo inakuwa *charged twice*. Kwa hiyo, ni vyema basi mtu angeweza kuhukumiwa kwa mara moja kuliko kuwa na *repetition* ya kesi katika mahakama zetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini suala la tatu pia ni pale ambapo mtu aliyefifilishiwa kosa atashindwa kulipa lile deni kwa wakati. Mapendekezo yalitoka kwamba kutakuwa kuna *interest*. Naona hapa kuna changamoto kwa sababu kuna mwingine anashindwa kulipa labda kwa sababu tu alikuwa ni mgonjwa kwa maana alikuwa na matatizo ya kiafya ambayo yamepelekea mpaka akashindwa kuilipa hiyo fedha kwa wakati. Kwa hiyo, tunapomwambia kwamba atachajiwa na *interest*, inamaanisha kwamba hapo hatujaangalia ule utu na uhalisia wa ubinadamu kwa sababu kila mtu ana sababu zake, kuna mwingine ni mkaidi tu ameshindwa kulipa lakini kuna mwingine amepata matatizo.

Mheshimiwa Spika, Kwa hiyo, hapa busara itumike kuhakikisha kwamba hiki kipengele cha kuongeza riba tuklondoe, hata kama kweli Serikali inataka mapato, lakini kiwe na sababu maalumu na kesi maalumu, kesi na kesi, siyo kwamba tu tuwachaji kwamba mtu aweke riba hata kwa mtu ambaye alikuwa na matatizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili ambayo napenda kuchangia ni Sheria za Vivuko. Ibara ya 18 ya Muswada, kifungu cha 12(2) kinasema: "*A person shall not carry any activities within the prescribed distance of public ferry which are likely to interfere with the ferry services operations or pollute public ferry environment*". Kifungu cha 12(3), kinasema: "*Any person who contravenes the provision of this section commits an offence and upon conviction shall be liable to a fine not less than fifty thousand shillings but not exceeding five hundred thousand shilling shillings*".

Mheshimiwa Spika, pamoja na sheria kuwa na nia njema lakini bado tunaona kabisa ile kusema *two miles* kutoka kwenye *public ferry* yoyote kulia na kushoto mtu asifanye shughuli zozote, basi ni vyema Serikali ingeweza kuelezea kinagaubaga kwamba ni shughuli gani hizo ambazo zinazuilliwa kufanya kwenye eneo husika. Kwa mfano, mtu anaweza kufanya shuguli ambazo zinazuilliwa kwenye eneo husika labda anafanya uvuvi wa kutumia mabomu lakini kuna watu wengine siku hizi tumeona hata wasanii wetu wanakwenda ku-shoot videos na vitu vingine kutokana na mambo ya sanaa kwenye maeneo kama hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaposema *any activities* maana yake ni kwamba kuna mwengine anaweza akafanya tu *activities* kwa nia njema lakini akajikuta ameingia kwenye huu mkumbo wa sheria. Ni vema Serikali ingeweza kusema ni shughuli gani ambazo zita-interfere hii *public ferry* na kusababisha madhara ndiyo hao waweze kuhusika na kifungu hiki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini Ibara ya 23 ya Muswada imeongeza baada ya *section 9, section* mpya ambayo

*inaelezea power of inspection, seizure and forfeiture.* Hii ipo kwenye hizi *legal gaming activities*. Pia imewekwa kipengele ambacho Bodi itakuwa na mamlaka ya ku-*destroy* hizo *gaming materials*.

Mheshimiwa Spika, hapa mapendekezo yangu ambayo nayaona, ni vyema basi wangeweza ku-*seizure, forfeiture* na *inspection* na *auditing* lakini wasi-*destroy* kwa sababu unapo-*destroy* pale ambapo huu jamaa atawea kwenda mahakamani na kuonekana kwamba hayo *material* yake hayakuwa *illegal devices*, itakuwa tena ni hasara kwake, kwa sababu tayari wameshaharibu mali yake. Kwa hiyo, kipengele hiki tungeweza kukitoa kwa sababu ni kibaya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia napenda kuiomba Serikali iweze kuweka tahadhari. Pamoja na ku-*promote* hii michezo ya *gaming* na *sport betting* kwenye taifa lakini bado kuna vitu ambavyo vinaonekana moja kwa moja vinaathiri shughuli za wananchi na uchumi kwa taifa kwa ujumla. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, kumekuwa kuna kundi kubwa la vijana na hata watoto, wanafunzi wa vyuo na sekondari, wamejingiza kwenye michezo hii ya kubahatisha na *sport betting* wakiamini kwamba kuna fedha nydingi sana ambazo zinapatikana huko na ni kweli ikitokea mtu ameshinda anapata fedha nzuri. Hata hivyo, tuangalie fedha anayoipata mtu mmojammoja na hali ya vijana na nguvukazi ya vijana kila siku kupotea ni fedha nydingi sana. Pamoja na ku-*promote* michezo hii lakini pia Serikali iangalie ni kwa namna gani nyanja nydingine za kiuchumi zinaweza zikaathirika kutokana na michezo hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, kuna watu ambao wana uwezo mzuri wa kulima, kufanya kazi za *mechanical*, za magari, za kupaka rangi na kadhalika lakini mtu anaamua kuacha kazi zote hizo na kwenda kufanya *sport betting* kwa kutegemea kwamba iko siku ambayo atapata *boom* na atapata fedha ambayo itamkidhi mahitaji yake. Pia kwa

wanafunzi, wamekuwa wakila ada wakienda kwenye michezo hii ya kubahatisha wakiamini kwamba watapata fedha nyingi zaidi watajikimu lakini pia wataweza kulipa na ada kutahamaki siku ya siku wanakuwa wamekosa vyote, amekosa ada lakini pia fedha za kijikimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini hata ndoa za watu zimekuwa hatarini kwa sababu michezo hii haina muda maalumu ambao inachezwa. Kuna wanaocheza usiku, mchana, kina mama wengi wanakuwa hawaoni familia zao. Pia hata familia zimekuwa zikiathirika kwa sababu wababa wengi wamekuwa ni rahisi kuchukua fedha kuipeleka kwenye *sport betting* kuliko kuipeleka nyumbani familia iweze kula. Kwa hiyo, tuangalie, kama kweli Serikali ina nia ya kukusanya kodi kwenye eneo hili husika pia iangalie sekta nyingine za kijamii na za kiuchumi ni jinsi gani zinaathirika kutokana na michezo hili ya kubahatisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sheria nyingine ambayo napenda kuchangia ni mabadiliko ambayo yanafanywa kwenye Sheria ya Tafsiri ya Sheria, yaani *Amendment of the Interpretation of Laws Act*. Kifungu cha 38 cha Ibara ya Muswada huu kinapendekeza section mpya ya 54(a)(b)(2), ambayo inasema: "*Where any written laws establishes a board and the board duly constituted, it shall lawfully for any prescribed operations requiring the decisions of the board to be performed by the Permanent Secretary of the Ministry responsible for the board until such time the board is duly constituted.*"

Mheshimiwa Spika, kipengele hiki naona na chenyewe kina shida kwa upande mmoja ama mwingine kwa sababu Bodi imewekwa kwenye taasisi ama idara za Serikali kwa sababu tu ya ile *check and balance* kwamba hawa wanatenda na hawa wengine wanakuwa na maamuzi na ile kuondoa *autonomy* kwenye Wizara ama taasisi husika. Sasa tunaposema kwamba majukumu ambayo yatakuwa *performed*na Bodi pale ambapo Bodi haipo ama imevunjwa afanye Katibu Mkuu wa Wizara kwa niaba ya Bodi, naamini kabisa hii itaenda kutofautiana hata na sheria nyingine za nchi. Kwa sababu inaweza ikatokea Katibu Mkuu ama Waziri

ana *personal interest* kwenye suala ambalo linakwenda kuamuliwa, kwa hiyo, tunaposema tulitoe kwenye Bodi tuliweke kwa mtu mmoja itakuwa ni shida. Kwa hiyo, kipengele hiki nacho kinaweza kikaathiri taasisi za kiserikali kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, lakini pia hata kama kuna ulazima Bodi imevunjwa na kuna maamuzi ya msingi yanataka kufanyika, basi itumike *budget authority* ambayo itakuwa na Katibu Mkuu wa Wizara lakini pia na Wakuu wa Idara, kwa umoja wao pamoja waweze kuamua hilo jambo kuliko kumuacha mtu mmoja ndiyo aamue kwa majukumu ya Bodi. Hii itakuwa inaharibu dhana nzima ya *good governance*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kipengele kingine ambacho napenda kuchangia ni Ibara ya 99 ya Muswada ambayo inatoa *exemption ya value added tax* kwa *materials* na mambo mengine yote ambayo yatazihusu *government entities*. Napenda kuiomba Serikali ingebadilisha msimamo na kuzitambua *private sectors* lakini pia hata Wabunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wewe ni Mbunge mwenzetu, tumekuwa tukiona majimboni kuna Wabunge ambao wanaomba misaada kwa ajili tu ya kusaidia jamii husika, labda jamii imekutwa na mafuriko, ama jamii inaathirika, kwa mfano, sisi kina mama, vijana wengi wa kike wamekuwa hawana pedi za kuwasaidia. Kwa hiyo, kama tutawawekea *exemption ya value added tax*, hata kwa sekta binafsi ili mradi tu ni kwa *public interest* basi na wenyewe tuweze kuwa-*include* kwenye kipengele hiki badala ya kuacha iwe ni idara za Serikali peke yake. (*Makofi*)

Mweshimiwa Spika, pia kulikuwa kuna mabadiliko ya kuivunja *Social Security Regulatory Authority* na kuwa na *Social Security Act*. Hiyo pia imeelezea majukumu mbalimbali ambayo yalikuwa yakifanya na mamlaka hayo ambayo yanaenda kufutwa kwenye sheria hii na kuhahamishiwa kwenye Wizara mbalimbali lakini bado yakiwa yamebakia

kwenye *Social Security Act*. Hii italeta mkanganyiko kwenye utekelezaji wa majukumu kwa sababu tunaamini Wizara husika zimekuwa zikifanya kazi kutokana na *instruments* ambazo zipo kwenye Wiraza zao.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, unapomwambia Waziri afanye kazi ambayo ipo kwenye chombo kingine na haipo kwenye *instrument* yake, ataitekeleza kwa bajeti ipi? Kwa hiyo, ni vyema tuliangalie pia suala hili ili majukumu ambayo yalikuwepo kwenye *Social Security Regulatory Authority* yaweeze kupelekwa kwenye Wizara husika, kwa maana ya kisheria ili kusiwe kuna mkanganyiko katika kutekeleza kazi hizi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Zainab Katimba nilikwishakutaja.

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika hoja iliyopo Mezani.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, kwanza nianze kuunga mkono maoni ya Kamati ya Sheria Ndogo kuhusiana na hoja iliyopo Mezani. Pia niwashawishi Wabunge wenzangu waweze kuunga mkono hoja hii ya Serikali. (*Makof*)

Mweshimiwa Spika, lakini nitambue ushirikiano mkubwa ambao umeonyeshwa na Serikali katika mchakato wa uchambuzi wa Muswada huu. Nawapongeza sana Serikali kwa ushirikiano na kazi kubwa ambayo mmekuwa mkifanya katika kipindi chote cha uchambuzi wa Muswada huu. (*Makof*)

Mweshimiwa Spika, sasa nikijielekeza katika ukurasa wa 20 wa Muswada ambapo kuna Marekebisho ya Sheria ya Adhabu (*The Penal Code*). Marekebisho haya yamelenga kwenda kuongeza adhabu ambazo zilikuwa zimeainishwa

katika kifungu cha 29 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu (*The Penal Code*) na imeziongeza ili ziweze kuendana na wakati huu tuliokuwa nao. Kwa mfano, kuna maeneo unakuta kwamba adhabu ilikuwa ni shilingi mia moja, sasa marekebisho haya yameenda kubadilisha adhabu ile ya shilingi mia moja kwa sababu haiendani na wakati, kwa hiyo, imeongezwa kufika shilingi elfu hamsini na maeneo mengine imeongezwa kutoka shilingi mia moja kwenda shilingi laki moja na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, hili ni jambo jema kwa sababu sheria inabidi ziende na wakati. Wakati sheria inatungwa shilingi mia moja ilikuwa inaweza kutoa faini kwa kosa fulani lakini kwa wakati huu shilingi mia moja haitoshi na hivyo, marekebisho haya yanaenda kurekebisha matakwa ya nyakati.

Mweshimiwa Spika, hili ni jambo jema ila ushauri wangu, kuna umuhimu sana wa kuangalia ni wakati gani au inachukua muda gani kufanya marekebisho ya sheria ili ziweze kuendana na wakati. Kwa hiyo, kuna mamlaka na kuna vyombo ambavyo vimeundwa kwa mujibu wa sheria ambavyo vimepewa madaraka au kazi ya kuweza kufanya mapitio ya sheria ili kuhakikisha kwamba zinaenda na wakati. Kwa hiyo, vyombo hivi viweze kupewa nguvu ili viweze kufanya kazi ya kufanya marekebisho ya sheria kwa kadri inavyohitajika.

Mweshimiwa Spika, lakini nikijielekeza pia katika ukurasa wa 21 ambapo kuna marekebisho ya Sheria hii hii ya Kanuni ya Adhabu ambayo imeweka katazo la kusambazwa kwa picha, video za maiti au mazingira ambayo ni hatari (*gruesome incidents*), mazingira ambayo yanaweza kuleta woga au siyo mazuri kuonyesha katika jamii. Marekebisho ya kifungu hiki kwenye sheria ni muhimu sana kwa sababu sisi wenyewe tumeshuhudia kwenye vyombo vya habari, hata kwenye simu zetu sisi wenyewe, kwenye *media outlets* mbalimbali unakuta kuna picha zimesambaa za kuonesha *dead bodies*, maiti, kuonyesha ajali na wahanga wameumia, mazingira ambayo siyo mazuri sana, yanasantazwa.

Mheshimiwa Spika, kuna familia, kuna ndugu wa hata hao marehemu ambao wanasantabaza kwenye picha na video, kitu ambacho siyo kizuri sana, kinasababisha matatizo makubwa sana ya kisaikolojia pia kwa wanafamilia na wananchi kwa ujumla. Kwa hiyo, kitungu hiki kinakuja kutibu na kuweka katazo la kusambaza picha za namna hiyo au video za namna hiyo.

Mheshiiwa Spika, cha msingi cha kufanya pamoja na marekebisho haya mazuri ni kuendelea kuelimisha jamii ili waweze kuelewa madhara ya usambazaji wa picha na video za namna hii. Siyo hivyo tu, hata sisi Wabunge tuna jukumu kubwa sana la kuwaelimisha wapiga kura wetu. Kwa sababu kuna usemi wanasema kwamba *ignorance of law is no defense*, yaani kutojua sheria siyo utetezi dhidi ya kosa.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu marekebisho ya sheria leo hii yakipita yataenda kuwa na nguvu ya kisheria, kwa hiyo, pale mtu atakaposambaza picha za aina hii ambazo zimebekewa makatazo kwenye kifungu hiki ina maana ataingia kwenye mkondo wa sheria na atahukumiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sisi kama wawakilishi wa wananchi wa Bunge pia tuna jukumu la kuwaelimisha wananchi wetu, wapiga kura wetu wafahamu kwamba kuanzia sasa hivi picha za ovyo ovyo hajitaruhusiwa kusambaa kwenye vyombo vyahabari pasipo kufuata utaratibu. Kifungu hiki kimeweka masharti vizuri.

Mheshimiwa Spika, nijielekeze katika ukurasa wa 15 wa Muswada ambapo kuna marekebisho ya Sheria ya Tafsiri ya Sheria (*The Interpretation of Laws Act*) ambapo Ibara hii katika Muswada imeenda kufanya marekebisho katika Kifungu cha 54 cha sheria ambacho sasa pale kunapokuwa Bodii haijaundwa na kuna matakwa ya sheria ya Bodii kuundwa na haijaundwa au imemaliza wakati wake wa kufanya kazi au imevunjwa; sasa yale majukumu yote yaliyokuwa yanafanywa na Bodii, yaweze kufanywa na Katibu Mkuu wa Wizara husika.

Mheshimiwa Spika, hili ni jambo jema kwa sababu linaondoa rasimu (*bureaucracy*). Kwa sababu mwisho wa siku Serikali ni moja na hata yale majukumu yanayofanywa na bodi ni majukumu ya Kiserikali ambapo mwisho wa siku Katibu Mkuu ndio Mtendaji Mkuu kwenye Wizara husika ambayo Bodi imeundwa. Kwa hiyo, kipindi ambacho kunakuwa hamna Bodi ili shughuli za Serikali ziweze kuendelea, nimeona ni vizuri sana hiki kifungu kimewekwa ili kuhakikisha kwamba Katibu Mkuu anaendelea na majukumu ya Kiserikali.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hili ni jambo zuri sana na ninawashawishi Waheshimiwa Wabunge wenzangu waweze kuunga mkono. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia kuna mabadiliko ya marekebisho ya sheria katika Sheria ya Mamlaka ya Udhhibit wa Hifadhi ya Jamii (*The Social Security Regulatory Authority Act*) ambayo yenye we imeenda kuondoa mamlaka ile ya udhibiti, *SSRA* imefutwa.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, tukumbuke hapa Bungeni sisi wenyewe tulikuwa sehemu ya kutunga sheria ya kufanya marekebisho ya sheria kuunganisha mifuko ya hifadhi za jamii. Hapo awali kulikuwa na mifuko mingi ya hifadhi za jamii ambapo ililetu hali fulani ya ushindani baina ya hii mifuko.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa sababu sasa hivi tumebakia na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa ajili ya Sekta ya Umma, lakini kuna Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa ajili ya Sekta Binafsi na pia tuna Mfuko wa Bima za Afya (*NHIF*) pamoja na *CHF*, ule shindani ambaa ulikuwa unaonekana hapo awali haupo tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kimsingi hata ile kazi iliyokuwa inafanywa na mamlaka hii ya udhibiti inakosekana na hivyo ni muhimu sana kama marekebisho yalivyolewa na Serikali kwamba Mamlaka au majukumu yale yabakie Wizarani kwenye Wizara husika. Mamlaka ilivyofutwa,

inaokoa fedha nyingi sana ambazo zilikuwa zinatokana na michango ya ile Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ambayo kimsingi ni pesa za wanachama. Kwa hiyo, fedha hizi ambazo zilizkuwa zinatumika kwa ajili ya bajeti kwenye hii mamlaka sasa hivi zitaenda kuimarisha masuala mengine katika nchi yetu, yataenda kusaidia sektanya za maendeleo katika nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, haitoshi hivyo tu, ukiangalia katika ukurasa ...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Zainab, ni kengele ya pili...

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nakushukuru kwa nafasi hii. Naunga mkono hoja ya Serikali. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa kwa muda uliobaki, naomba nimpatie nafasi Mheshimiwa Peter Serukamba kwa suala alilonalo. Mheshimiwa Serukamba nakuruhusu.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 50(1) Kanuni za Bunge Toleo la 2016 naomba kutoa maelezo binafsi mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, nimesimama kwa sababu kuu moja ambayo ni kufafanua na kisha kuomba radhi Chama changu na Viongozi wangu wa Chama cha Mapinduzi kutokana na matamshi niliyoyatoa wakati nikichangia hoja hapa Bungeni mwezi Juni, 2019. Wakati nikihitimisha hoja yangu, nilitumia neno "Ujamaa" katika mukhtadha ambaa baadaye nilikuja kubaini ulisababisha tataruki iliyotokana na tafsiri ambayo sikuimaanisha.

Mheshimiwa Spika, sentensi ya mwisho katika hoja, ilikuwa ni maneno yafuatayo: "kama kuna jambo siliamini, ni Ujamaa."

Mheshimiwa Spika, msingi wa hoja yangu haikuwa kuupinga Ujamaa kama itikadi ya kisiasa ya kujenga uchumi wa Kitaifa na badala yake illenga kuchochera mjadala wa kujenga uchumi wa kijamaa unaotambua mchangano wa Sekta Binafsi katika juhudini za kukwamua kilimo chetu.

Mheshimiwa Spika, mimi ni zao la Chama cha Mapinduzi ambacho kinaamini katika dhana ya Ujamaa na Kujitegemea na hivyo, haiwezekani mimi tena nikakaririwa kwa makosa na hata kutafsiriwa ninaukana msingi wa kuwepo kwango Bungeni na ndani ya CCM. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mimi ni mjamua kwa kulitambua hilo na kwa ajili ya maslahi mapana ya Taifa, napenda tena kukiomba radhi Chama changu, Viongozi wote wa CCM kwa usumbufu uliotkana na matamshi yangu ambayo yalitafsiriwa katika muktadha usio sahihi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Peter Serukamba, tunakushukuru kwa tamko lako hilo; na hata vazi ulilovaa leo linaonesha kwamba wewe mjamua. (*Makofii*)

Sasa naona nina dakika kidogo, tuzitumie vizuri. Mheshimiwa Salome Makamba, uendelee kuchangia. (*Makofii*)

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kwa dakika hizi chache nami niweze kutoa mchangano wangu katika mabadiliko haya Na. 6 ya sheria yaliyoletwa kwenye Bunge letu Tukufu.

Mheshimiwa Spika, mimi yangu leo ni mawili ambayo ningependa kufafanua baada ya hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani. Napenda kushauri Serikali katika mabadiliko aliyoyleta katika Sheria ya EWURA Kifungu cha 6 wafute Kifungu cha 3 ambacho kinasema kwamba mtu

anaposhindwa kulipa deni la kosa ambalo limefifilishwa, basi Mamlaka, yaani Mamlaka ya *EWURA* ina huwezo wa kumtoza riba.

Mheshimiwa Spika, lengo la kufifilisha kosa na wameeleza vizuri kwenye madhumuni ya Muswada huu kwamba wanafifilisha kwanza ni kuokoa muda wa kupeleka kesi Mahakamani lakini pili ni kuruhusu biashara ziweze kuendelea. Mtu huyu ameshakiri kwamba ni kweli amefanya kosa na akakubaliwa kulipa nusu ya deni ambalo angeweza kulilipa akienda Mahakamani, sasa katika mazingira ya kawaida ya kibiashara tuseme *EWURA* ina-deal na wanaomiliki vituo vya mafuta na maeneo ya namna hiyo. Kama ameshindwa kulipa deni na hajakataa kulipa, ukimtoza riba tafsiri yake unamwongezea kwenye deni lile la msingi.

Mheshimiwa Spika, kwa kufanya hivyo tunafahamu wote mazingira ya kibashara Tanzania yalivyo sasa hivi, wakati mwagine biasharahaziendi vizuri, wakati mwagine mtu anakwama kwa sababu watu wanaohusika na biashara zinazohusiana na *EWURA* wengi wana mikopo benki, kwa hiyo, wakati mwagine mtu anaweza kushindwa kulipa kwa sababu ya kibiashara. Kumtoza riba mtu huyu ni kumwongezea mzigo juu ya mzigo ambao tayari amekiri.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naishauri Serikali isimtoze riba mtu ambaye amekiri kosa lake, amekubali kulipa, lakini ameshindwa kulipa. Badala yake wanazo nafasi mbili za kufanya; kwanza, wanaweza kukaa mezani na kuzungumza naye namna bora ya kumsaidia aweze kulipa deni hilo. Hii alifanya Mheshimiwa Dkt. Mpango wakati wa wasilisho lake la Wizara ya Fedha kwenye Bajeti iliyopita, akawaongezea muda watu ambao walikuwa wanadaiwa madeni ya kikodi na *TRA* na ambao walikubali. Kwa nini tusifanye hivyo kwa watu ambao makosa yamefifilishwa? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Serikali ili kuonesha kwamba wao sio washitaki, sio waamuzi na wao ndio kila kitu, wanaweza

kupeleka jambo hili Mahakamani kama inavyoelezwa kwenye Kifungu kidogo cha (4) kilicholetwa kwenye marekebisho ya Mswada bila kumtoza riba mfanyakishashara huyu. Kwa hiyo, kama ameshindwa kulipa na Serikali wameshindwa kuafikiana, basi kesi hiyo ipelekwe Mahakamani ikaamuliwe Mahakamani na mtu yule aweze kulipa kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu za nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo niongeze pia katika kifungu kinachohusiana na vifuko vya feri. Katika mabadiliko *clause No. 18* ya Muswada huu wa Marekebisho, wanasema kwamba kwenye Kifungu kidogo cha (3), mtu ye yote atakayeingilia shughuli za kivuko, shughuli zozote zile; atakayefanya shughuli ambazo zitaingilia kivuko, basi atatakiwa kulipa faini ya shilingi 50,000/= mpaka shilingi milioni 10 nimeona kwenye mabadiliko ya Serikali au kufungwa miezi sita au vyovoyote kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa jumla sana kwenye kifungu hiki na tuliwashauri vizuri sana kwenye Kamati, waeleze hizo shughuli za binadamu wanazosema zitaingilia kivuko ni zipi? Kwa sababu nimesoma vizuri kwenye hotuba yetu kwamba unaposema shughuli za kibinadamu zitakazoingilia shughuli za kivuko, zipo tofauti na zinatofautiana kwa madhara. Leo huwezi kusema unamtoza mtu aliyeingilia shughuli za kivuko, kwa mfano, pale kwenye kivuko cha Kigamboni Dar es Salaam, kwa sababu ameogelea, basi unamtoza shilingi milioni 10 kwa mfano, kwa sababu kiwango cha ukomo ni shilingi milioni 10. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, wakati mwingine kuna watu kweli nakubali wanafanya makosa makubwa kama uvuvi wa kutumia nyavu ambaa unaweza ukaharibu kabisa feri yetu. Kwa hiyo, niseme, moja kati ya jambo ambalo linawapa wakati mgumu watafsiri wa sheria kwa maana ya Mahakama ni kuelewa dhamira ya Bunge. Nasema hayo kwa sababu sisi leo tutapita, hii sheria inabaki inaishi, tutawapa changamoto kubwa watakaokuja mbele yetu kuelewa kwamba tulitoa shilingi 500,000/= mpaka shilingi milioni 10

kwa sababu tulikuwa tunawaangalia watu ambao labda wanaweza wakaharibu kabisa kivuko.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naishauri Serikali ije na jedwali, linaweza lisi- *cover* kila kitu, lakini angalau lioneshe msingi wa faini yake inayotolewa katika kifungu hiki na ile itasaidia kupunguza watu ambao wanafanya makosa madogo kutozwa faini kubwa au wanaofanya makosa makubwa kutoza faini ndogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niende moja kwa moja katika sheria ya Utumishi wa Umma. Sheria ya Utumishi wa Umma imempa nafasi *Chief Secretary* ya kusamehe *conditions* zote ambazo zinaweza kumsababishia mtu ashindwe kulipa mafao yake. Najaribu kutafsiri kwa Kiswahili ili niweze kueleweka, lakini kifungu kiko *very clear*.

Mheshimiwa Spika, sasa mwaka 2018 tumetunga sheria hapa ya *Social Security* ile ambayo ni almaarufu kama Sheria ya Kikokotoo, tukatunga na tukampa Waziri mwenye dhamana mamlaka. Tukatoka hapo, kuna Bodi ambayo inahusika na *pension* na mafao ya kustaafu.

Mheshimiwa Spika, sasa leo tukisema tunatoa mamlaka ya Bodi ambapo Bodi haiongozwi na mtu mmoja, tunatoa mamlaka ya Waziri, leo tunachukua nafasi ile tunampa *Chief Secretary*. *Chief Secretary* kwa Kiswahili anaitwaje kwani?

**MBUNGE FULANI:** Katibu Mkuu Kiongozi.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** ...tunampa Katibu Mkuu Kiongozi, ahsante. Tunampa Katibu Mkuu Kiongozi peke yake mamlaka ya kusamehe mazingira yoyote na imeandikwa kwenye *act*, mazingira yoyote ambayo yanaweza kufanya mtu asilipwe *pension* yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hii sheria inayotungwa leo inakinzana na sheria ambayo tulitunga mwaka 2018. Kwa hiyo, naomba Serikali iweze ku-harmonize sheria hizi mbili kwa

kuweka ama kurudisha mamlaka kwa Bodi ambayo iko chini ya Sheria ya Mifuko ya Jamii Na. 2 ya Mwaka 2018, irudishe mamlaka hayo na kwa *minister*. Sheria ile imeeleza bayana namna mamlaka haya yanavyogawanya.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa sheria ya ongezeko la thamani (*VAT*). Sheria hii Serikali kwa kweli imefanya vizuri kuondoa kodi kwenye miradi yote, fedha za miradi yote ambayo inahusisha Serikali. Hii wamesema vizuri kwamba inasaidia kuongeza kasi ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, nakuomba na niiombe Serikali ione haja ya kufanya hivyo hivyo kwa dhamira hiyo hiyo ya *ku-speed up* miradi ya maendeleo kwa *private sectors*. Najua hofu ya Serikali ni kwamba *private sectors* au watu wanaweza kutumia vibaya nafasi hii kujinufaisha wenyewe.

Mheshimiwa Spika, juu ya kifungu kile mwanzoni wanasema, "*in consultation with the minister*," tena lazima ridhaa hiyo iwe *published* kwenye *Government Gazette*. Ile tu pekee inatosha kulinda watu wasitumie vibaya madaraka haya ya kutokutozwa kodi kwa vitu ambavyo wameingiza ndani ya nchi kwa ajili ya maendeleo au manufaa ya Umma.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, kwenye Bunge hili lako Tukufu, wapo Wabunge ambao wanapewa vitu na wahisani na marafiki zao mbalimbali. Kuna watu wanaleta zile balskeli za walemavu, kuna watu wanaleta pedi za kike, wanapewa na makampuni huko nje; basi hii iwe ni fursa kwao kuweza kuomba ridhaa ya Waziri wapate msamaha wa kikodi ili waweze kufikisha huduma kwa wananchi. Nchi hii ni yetu sote na tunajenga wote kwa umoja wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kufafanua hayo, naiomba sana Serikali, ni mengi tumerekebisha kwenye Kamati, lakini bado tunayo nafasi ya kubadilisha zaidi, yawezekana mazingira yakawa ni magumu hasa kwenye suala la *VAT*, lakini dhamira ile ile ikitumika na njia ile ile ikitumika kuboresha misamaha katika miradi ya maendeleo kwenye jamii, Bunge lako ni Taasisi, Wabunge wako wana

uwezo mkubwa wa kuweza kupata misaada kwa ajili ya kuwasaidia watu mbalimbali katika nchi hii, hii itumike kama fursa na VAT iondolewe katika miradi au katika misaada ambayo Wabunge wanapata, katika misaada ambayo Makanisa wanapata, katika misaada ambayo *private sector* wanapata kwa ajili ya kusaidia na kuwasaidia na kusaidia kusukuma gurudumu hili la maendeleo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana, ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Salome Makamba.

Waheshimiwa Wabunge, mmetaja hili jambo la pedi, hili ni jambo kubwa jamani, nawaunga mkono mnachosema. Juzi katika nchi jirani; nchi jirani si mnajua jamani! Nafikiri mmesikia, mtoto mmoja wa shule ya msingi wa miaka 14 amejinyonga kwa sababu alipokuwa shule akawa kwenye *menstruation* halafu Mwalimu wake mmoja akamsema vibaya kuhusu hiyo hali yake. Basi mtoto katoka pale shule, karudi nyumbani, kamkuta mama yake, akamwelezea kilichotokea shulenii, mama naye akadhani amem-*console*, akamwambia aah, wewe endelea na shughuli zako tu. Kumbe limeshamsumbuwa sana kisaikolojia, hakupata ile *comfort* aliyoitarajia, akachukua ndoo kama vile anaenda kuchota maji kisimani, akajinyonga akafa.

Kwa hiyo, hili jambo linahitaji tuwe tunaliangalia, ni jambo kubwa na vilevile kutoa elimu kwa watoto wetu hasa wa *primary* hata na *secondary* kuhusu hali hii waweeze kuifahamu.

Nakumbuka hata sisi tulipokuwa shule ya msingi tulikuwa tunawacheka wadada wa namna hiyo, kwa sababu tulikuwa hatuelewi. Umeona kakaaje sijui, basi eeh, huyo, huyo, kumbe ni kitu ambacho *psychologically* kibaya sana.

Kwa hiyo, jambo hili tunahitaji litazamwe vizuri zaidi kwa kweli. Mimi baada ya hilo nikashtuka, nikaona dah!

Wabunge wengi mnasemaga humu tunaliona kama ni jambo la kawaida tu, lakini ni katika *priorities* kwa kweli. (*Makofi*)

Baada ya hapo, Waheshimiwa wengi wameniandikia hapa, mbona Spika humpongezi Mheshimiwa Sugu kwa kuo? (*Kicheko*)

Sasa naye hajanitaarifu vizuri bwana! Hata hajaniandikia *note*; hongera sana Mheshimiwa Sugu. Kwa niaba ya Waheshimiwa Wabunge wote tukupongeze kuingia katika utaratibu wa ndoa takatifu kwa kufuata utaratibu kabisa. Sasa karibu kwenye klabu sasa, ukitaka mafunzo kidogo, basi tutakuwa tunakupatia patia, tuko wengi hapa, lakini vinginevyo tunakupongeza sana. Hongera sana. (*Makofi*)

Ila sasa inatakiwa ubadilishe na mwenendo sasa. Ukipishaoa unabadijika sasa! Mambo ya kurudi saa nane ya usiku sijui nilikuwa wapi, hamna tena. Hapo lazima ujieleze, ulikuwa wapi? Ahsante sana. (*Makofi/Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na suala letu hili vizuri tu leo jioni kuanzia saa 11.00, tutakuwa na wachangiaji wanne, halafu atafuata Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Ataaanza Mheshimiwa Mariam Kisangi, Mheshimiwa Taska Mbogo, Mheshimiwa Goodluck Mlinga na Mheshimiwa Jitu Soni halafu Mheshimiwa Waziri wa Fedha, atafuata AG halafu utaratibu utaendelea, Bunge zima tutapitia kama kawaida yetu. Naomba tuitendee haki hii sheria, tuwahi kufika saa 11:00.

Niwakumbushe Wabunge wa CCM kwenda CCM kule *Whitehouse* saa 7.00 ili by saa 8.00 mpate chakula, by saa 9.00 tukutane pale wote pale Msekwa kama niliviotangaza mapema, nasisitiza kuhudhuria Msekwa pale na saa 11.00 tutaendelea na ratiba yetu kama kawaida.

Basi kwa hatua hiyo, naomba nisitishe shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni ya leo.

*(Saa 7.02 Mchana Bunge lilitishwa hadi Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilitrudia)*

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:**

*Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 6) wa Mwaka 2019(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 6) Bill, 2019)*

*(Majadiliano yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na wachangiaji, tutaanza na Mheshimiwa Mariam Kisangi, atafuatiwa na Mheshimiwa Taska Mbogo, Mheshimiwa Goodluck Mlinga ajiandae.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia muswada huu muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda niipongeze Serikali nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Bunge, Sera na Wenye Ulemavu, Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu, Naibu, Mawaziri, Uchukuzi, Fedha, Naibu Waziri wa Maji, Makatibu Wakuu, Watendaji wa Serikali, lakini kipekee napenda kumshukuru, Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria Ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwenyekiti huyu kwa kweli ni mtu muhimu sana na amenipa somo leo kwa mara ya kwanza katika Bunge lako tukufu, namimi najaribu kuchangia

muswada wa sheria kutokana na elimu ambayo nimeipata kwa Mwenyekiti huyu, pia naomba niwapongeze Wajumbe wote wa Kamati ya Sheria Ndogo kwa kazi kubwa walioifanya na ushirikiano wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Muswada huu ya Mabadiliko ya Sheria Mbalimbali mchango wangu utajikita katika sehemu ya pili; Marekebisho ya Sheria ya *EWURA* Sura namba 414, lakini pia utajikita katika Sheria ya Michezo ya Kubahatisha Sura Namba 41, lakini pia nitazungumzia kidogo Sheria ya Vivuko Sura 173.

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze sana Serikali kwa mara nyininge muswada huu kuleta kwa hati ya dharura, mimi nafikikiri ni jambo muhimu sana na tumpongeze sana Mheshimiwa Rais wetu kwa kazi kubwa anayoiifanya ya kuwajali makundi mbalimbali ambayo yalibanwa na sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Muswada wa Sheria wa *EWURA* naomba nichangie katika maeneo yafuatayo; kwanza kabisa suala ambalo lilikuwa linawaudhi wengi na linatukera watu wengi ni pale ambapo Waziri wa Nishati alikuwa hana mamlaka ya kuweza kuamua chochote kwa sababu *EWURA* ilikuwa chini ya Wiizara ya Maji, Muswada huu muhimu sasa unamrudisha Waziri wa Maji na Waziri wa Nishati kufanya kazi pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika masuala ya mafuta ndiyo masuala makubwa katika uchumi wa nchi yetu na masuala haya yote yalikuwa yanasihamiwa na Waziri wa Nishati, leo hii katika maamuzi Mheshimiwa Waziri wa Nishati hakuwa na maamuzi, lakini muswada huu muhimu umeleta marekebisho katika eneo hilo, sasa Waziri wa nishati na Waziri wa Maji watafanya kazi pamoja, watatoa maamuzi ya pamoja, lakini pia watapitia taarifa zote kwa pamoja na hata kwenye bodi, Wajumbe wa Bodi watachaguliwa kutoka kwenye pande zote mbili, mimi niipongeze sana Serikali kwa hilo jambo muhimu walilolifanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pili katika sehemu hiyo ya pili muswada huu wa sheria unampa Mkurugenzi uwezo wa kufifilisha makosa. Naomba ni *declare interest* kwamba mimi ni mdau katika eneo hilo, masuala ya makosa wafanyabiashara wengi wa mafuta katika miji mbalimbali walikuwa wanafanya makosa, lakini mwisho wa makosa yao wanaambiwa wasubiri bodi, wanafungiwa miezi mitatu, miezi minne na wengine wanakimbilia kwa Mkurugenzi, lakini Mkurugenzi yule alikuwa hana meno, muswada huu unampa meno Mkurugenzi wa *EWURA* kwamba sasa awe na uwezo iwapo mfanyabiashara atleta shida na akakubali makosa yake basi Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kumfifilishia kosa lake na kuweza kulipa faini inayotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia muswada huu umetoa nafasi kubwa kwa na uhuru mkubwa kwa wananchi pale wanapoonaa kwamba makosa hayo waliopewa hawaridhiki nayo wamepewa uhuru wa kwenda mahakamani. Ni jambo jema sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye suala zima la *interest*, nakubaliana kabisa na Serikali na maamuzi yao kwamba lazima tuweke *interest* ili kujenga imani kwamba unapokopa deni lazima ulipe, naomba waangalie kwenye *regulation* yao kwamba waweke hizi *interest* zinazotolewa wazi, isiwe zimefinywa finywa wajuwe kwamba kosa fulani litalipiwa faini kiasi fulani na *interest* itakuwa vipi na kosa fulani itafanywa hivi natambua *EWURA* wana kanuni zao, nitaiomba Serikali kwenye hizo kanuni zao basi waweke wazi masuala yote kama vile Serikali ilivyoweka wazi katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niseme suala hili limechelewa, lakini nimeona kabisa juhudzi za wazi za Mheshimia Rais katika kuboresha mazingira ya biashara yawe rahisi katika Taifa letu. Ni jambo zuri na ni jambo ambalo huwa tunafikiri sheria hii itakaposainiwa wananchi na wafanyabiashara wetu watafurahia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye Sheria ya Michezo ya Kubahatisha; lengo la muswada huu ni kuhakikisha pia wanadhibiti, lakini pia kuipa bodi mamlaka ya kufanya ukaguzi, ukamataji na ufilisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona mara nydingi wananchi wetu ambao wanacheza michezo hiyo ya kubahatisha wamekuwa wakipata matatizo ambayo hakuna wa kuyatatua, sasa bodi imepewa mamlaka kama mfanyakishara au mwenye bahati nasibu anafanya vitu visivyooleweka, lakini pia anashindwa kulipa kodi, anashindwa kulipa watu wake basi sheria hii itashika mkondo wake, itamkamata na kumfilisi, lakini katika kufanya kazi hiyo naiomba Serikali katika kuangalia nao sheria zao waangalie kwamba haki itendeke, siyo kwa vile tumewapa mamlaka hayo wakafanye mambo yasiyofaa. (*Makofi*)

Mhehimiwa Naibu Spika, lakini pia sheria hiyo imeongeza wigo wa kutoa leseni ya michezo ya kubahatisha, tunashuhudia katika *tv* kwamba kuna michezo aina mbalimbali, mingine inachezwa hapa nchini na mingine inachezwa nchi za nje, sasa ile ya nchini walio tayari watapewa leseni, lakini sheria hii pia inaweza *security bond* kwa yejote yule atakayefanya biashara hii.

Mheshimiwa Spika, hiyo *security bond* itasaidia sana kwa sababu tumeona wanacheza michezo, wanawaahidi watu milioni mia tano, lakini unaambiwa yule mtu hajapata hiyo pesa. Sasa Serikali inamsimamia Mtanzania ambaye atakuwa amecheza huo mchezo, lakini akulipwa hii *security bond* itasaidia kumlipa lakini na yeje pia itamsaidia iwapo atakuwa ametenda kosa aondolewe kwenye eneo hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nichangie sehemu ya sita, ibara ya 165 kupanua wigo wa matumizi ya vivuko; kweli kabisa tunatambua umuhimu wa vivuko vya Serikali vinatakiwa viwekewe nafasi, lakini hiyo adhabu iliyowekwa tuangalie mbele na nyuma, kuna wakati katika maeneo ambayo yanawekwa vivuko vya Serikali kunatokea

hatari, kwa mfano kama hivyo Kivuko cha Kigongo sijui, huko kama vivuko kama Kigamboni maeneo hayo mara nyingine kinawenza kikawa *lime-fail engine*, viboti vidogo vidogo huwa vinakuja kuokoa wananchi; sasa je, sheria hiyo itakuwaje? Kwa hiyo, niombe kwenye kanuni za uokoaji, lakini katika kanuni nzima ambazo zitaongoza kwenye eneo hili basi waangalie jinsi gani hivyo viboti vidogo vidogo iwapo itatokea dharura au ajali yoyote kuweza kuingia kwenye eneo la vivuko.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sina mengi, niishukuru sana Serikali, nimshukuru Mheshimiwa Jenista Mhagama kwa jinsi anavyoliongoza Bunge kwa kweli tunampongeza sana mama huyu usiku na mchana mpaka kinaeleweka. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana lakini nimshukuru Mwenyekiti wangu tena kwa mara nyingine kwa kuniwezesha na mimi leo kuanza kuipenda sheria. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante. (*Makof!*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Taska Mbogo atafuatiwa na Mheshimiwa Goodluck Mlinga, Mheshimiwa Jitu Soni ajiandae.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kwanza naomba niipongeze Serikali kwa kuleta mabadiliko ya sheria hii, naomba nimpongeze Jenista Mhagama na Mawaziri wote waliokuja kwenye Kamati yetu, tuliiita Serikali na kwa kweli kwa mara ya kwanza tulishuhudia Mawaziri wanne walikuja kwenye Kamati yetu na kila mtu alikuwa anajibu hoja ambazo Kamati ilizuliza. Tulikuwa na Waziri wa Maji, mwanangu Mheshimiwa Aweso; tulikuwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Kwandikwa, tulikuwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali na tulikuwa na mwandishi Mkuu wa Sheria za Bunge

(CPD), wote walikuja kwenye Kamati yetu na wote waliweza kutuelekeza yale ambayo tuliyouliza kwenye Kamati na majibu tuliyapata.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye muswada huu mimi nakwenda kwenye *page* ya 14 na nitachangia kile kifungu ambacho kimeongeza adhabu ya mtu anachezesha *game* ambaye atamshawishi mtoto mdogo kuingia kwenye hiyo michezo na kuangalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiki kifungu kilikuwa kimewekwa adhabu ndogo ambayo ilikuwa inaishia shilingi 500,000; lakini kwa kuongeza adhabu kuanzia shilingi milioni moja mpaka shilingi milioni tano kitawafanya wale wanaochezesha hii michezo ya kuigiza na wale ambaou huwa wanapenda kuwashawishi watoto kwenda *casino* wataweza kuogopa, maana yake tabia nyingi za watoto/ watoto wengi wanaharibika baada ya kuangalia *movie* zile ambazo anaangalia, anapata ushawishi ambaou unamfanya na yeze anasema na yeze ebu nijaribu na mimi nijaribu hiki kitu. Kwa hiyo, kwa kuweka kifungu hiki, wale wote ambaou wanachezesha hii michezo hata kule vijijini, mikoani na wilayani wataogopa kuwaingiza watoto wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine ambacho ningependa kukichangia kwenye muswada huu ningependa kuipongeza Serikali kwa kuleta katazo la upigaji picha mtu aliyekufa na maiti kwenye kile kifungu cha 162, lakini hata pia ningeiomba Serikali iongeze wigo kwa sababu mtu unaweza ukawa unasafiri ukakuta basi limeanguka labda limeanguka kwenye mtaro na watu wamekufa ukataka uchukue zile picha kwa ajili ya kuhabarisha umma au kwa ajili ya kuzipeleka polisi ili ziwe ushahidi.

Mheshimiwa Spika, sasa maeneo mengi kama unavyojuwa nchi yetu, hatujafikia kile kiwango cha kuwa na kamera kwenye barabara zetu, kwa wenzetu wa Magharibi wao wanakamera kwenye barabara zao kila mahali, kwa hiyo, hata kama ukikataza upigwaji wa picha

unakuta kwamba ni sahihi, lakini kwetu sisi hatujawa na kamera kwenye barabara zetu ambazo zinaweza zikapiga picha ajali inapotokea mahali popote hata kama ni porini.

Kwa hiyo, nilikuwa naiomba Serikali ijaribu kuangalia kwa katika *circumstance* ambazo zinatokea mtu amekuta watu wamekufa pale anataka kutumia hiyo picha kama ushahidi basi aweze kupiga na kuhabarisha umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye kipengele hicho lakini niseme naipongeza kwa kuja na hiyo sheria kwa sababu watu wengine walikuwa wanaitumia vibaya kupiga miili ya watu kwa mfano mzuri ilikuwa ni ajali ya Morogoro iliyotokea hapa juzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipengele kingine ambacho ningependa kukzungumzia ni kile kipengele cha 54(2) chenye *interpretation act cap. 1*; kipengele hiki kimeandikwa katika lugha pana, ingependeza zaidi kama sheria ingeainisha ni maeneo gani mahususi ambayo Katibu Mkuu atayafanya, lakini kwa kuiacha tu ndani ya wigo kwamba Katibu Mkuu anaweza akafanya mambo fulani wakati ile bodi haipo na haiainishi yale mambo ambayo Katibu Mkuu anatakiwa afanye naona kipengele hiki kitampa mwanya mkubwa Katibu Mkuu kiasi kwamba kama ni mtu ambaye anataka ku-*misuse power* zake akatumia hiki kipengele cha 54(2) ningemba Serikali ijaribu kukiangalia na kukiandika vizuri zaidi ili kikidhi hitaji ambalo linahitajika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze Serikali kwa kufuta ule Mfuko wa SSRA. Naipongeza Serikali kwa sababu imeangalia ikaona kwamba ilikuwa inatumia pesa nyingi kuwa na huo mfuko, kwa hiyo imeondoa yale majukumu ya ule mfuko inayapeleka kwenye Wizara ya Mheshimiwa Jenista, lakini niiombe Serikali hiyo *division* itachukuwa majukumu ya ile mifuko yote ijaribu kuihudumia lle mifuko ambayo inaidumia kama jinsi ambavyo SSRA ilivyokuwa inafanya kazi zake, isiwe tu kwamba tumevunja kwa sababu leo kwa kipengele namba 72 ina maana tunaivunja rasmi SSRA hapa

Bungeni, ila tunaendelea kutumia sheria zake ambazo zimeainishwa kwenye kipengele 72 nafikiri kila mtu ana muswada huu anaweza akaenda akaangalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naipongeza Serikali na naiomba Serikali kama inaona vitu vingine ambavyo ilivianzisha, lakini imeshaona kwamba haiwezi ikaendelea kutumia pesa nyngi kuwa na mifuko ya aina hiyo inaweza ikaleta tu pia nayo tukabadiilisha kwa sababu hata nyumbani ukiona umefanya kitu lakini unaona hakiendi unabadiilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo sioni vibaya kwa Serikali kuvunja huo mfuko na kupeleka haya majukumu kwenye Wizara kwa sababu kuna kitengo kitaanzishwa pale, kuna idara itaanzishwa pale ambayo itakuwa inashughulikia majukumu hayo, lakini niseme tu kamba na kamba kuna taasisi nyngine ambazo zimeazishwa ambazo Serikali inaona kwamba ni mzigo mkubwa kuziudumia basi ilete zile sheria na niwaombe Wabunge humu Bungeni tuzibadilishe na tusione ubaya wa Serikali kuivunja *SSRA* na kubaki tunatumia zile sheria zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa pia kuzungumzia suala la adhabu ya kulipa *interest* ambayo imeshazungumzwa na Wabunge wengi kwa mtu ambaye ameshapewa adhabu na amekabiliwa lakini anapochelewa kulipa inabidi aliipe *interest*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali hajatoa kikokotoo cha *interest* na tulivyoiliza Serikali kwenye Kamati yetu ilisema italeta kwenye *regulations*. Kwa hiyo niombe tu Serikali itakavyoleta *regulations* hizo za kikokotoa hizo *interest* ilete kikokotoo kizuru isimuumizi yule mtu ambaye amepewa adhabu kwa sababu mtu anaweza akawa amepewa adhabu ya kulipa milioni 100, lakini sasa *interest* ikawa unaambiwa kila mwezi ulipe shilingi milioni 20 *by the time* miezi sita inaisha unakuta yule mtu anadaiwa milioni 300.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo niombe kikokotoa hicho kitakacholetwa kiwe ni kikokotoa ambacho kitakuwa rafiki, ambacho yule mdaiwa anaweza akakilipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni *bond* ambayo imeshazungumzwa na Wajumbe waliopita, niipongeze Serikali kwa kuleta utaratibu wa kuweka *security bond* kwa hawa wanaochezesa michezo siku hizi kwa sababu ni wengi wameibuka, wanachezesha hiyo michezo, kwa hiyo, kwa kuweka *security bond* ina maana mtu atakapo *win* kama asipolipa ile pesa yake ile *security bond* ya yule aliyechezesa mchezo inaweza ikatumika kumlipa yule mchezeshaji, kwa hapa niombe kuipongeza sana Serikali kuja na sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe tu kwa kutumila *floorhii*, Serikali ijaribu kuangalia sheria nyingine zote ambazo zimepitwa na wakati izilete ili tuweze kuzibadilisha hapa Bungeni kwa sababu tunazo sheria nyingi sana. Nitoe tu mfano, kuna sheria za *traffic* zimepitwa na wakati, anamgonga mtu amekufa, amevunjika mkono, lakini akienda mahakamani akikubali lile kosa anaishia kulipa 50,000 na Sheria nyingi tu ambazo zimepitwa na wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe Serikali kwa sababu inayo Tume ya Kubadilisha Sheria nchini, basi Tume hii ya Kubadilisha sheria nchini itumike vizuri katika kipindi cha mwaka mmoja tuone ile tume imefanya kazi kubadilisha sheria zippi. Tunazo sheria nyingi sana ambazo zimekaa, zingine ni za toka mwaka 1963, lakini bado zinatumika humu nchini. Ukiziangalia hata kwenye sheria nyingine ambazo si nzuri kwa wanawake kama mtu kupewa matunzo ya shilingi 100 kwa mwezi, zote hizi ambazo ziko kwenye Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 bado niiombe Serikali kama jinsi inavyoweza kubadilisha sheria hizi basi ichukue tena umuhimu wa kubadilisha hizo sheria nyingine ambazo zimepitwa na wakati ili ziweze kukidhi hitaji la Watanzania wote wanawake na wanaume.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu kwenye huu Muswada kwa sababu nilikuwa Mjumbe wa Kamati na tumeuchambua kwa undani, nikiendelea kusema mambo mengi ambayo hatukuchambua kwenye Kamati nitakuwa ninasema uongo. Naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante!

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Goodluck Mlinga, atafuatiwa na Mheshimiwa Jitu Soni, Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango ajiandae.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana naomba nichukue fursa hii kwanza kuipongeza Serikali kwa kuleta mabadiliko haya ya sheria tisa kwa mpigo. Lakini kama walivyotangulia wenzangu, kuna sheria nyngi ambazo zimepitwa na wakati, zingine zipo zinaumiza watu, nyngine zipo lakini hazina manufaa. Kwa hiyo zipo ambazo ni za kuboresha, zipo ambazo ni za kuzifuta kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano Sheria ya Ubakaji, kutohana na ongezeko kubwa la ubakaji ilitakiwa sheria iletwe tubadilishe sasa, siyo kufungwa miaka 30 tu, ilitakiwa wahasiwe wabakaji. Pia sheria ya *traffic*; pikipiki inabeba abiria mmoja inalipa *traffic case* shilingi 30,000, basi linabeba abiria 60 eti la lenyewe shilingi 30,000 hiyo hiyo. Kwa hiyo, hizi sheria zinatakiwa zinabilishwe siyo tunabeba kila kitu walichoacha wazungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nije sasa kwenye sheria ambazo tumezibadilisha. Sheria ya kwanza napenda kuipongeza Serikali, hii Sheria ya *SSRA*. Tulanzisha *SSRA* kwa sababu kulikuwa na mifuko mingi ya hifadhi ya jamii kwa hiyo ushindani ukawa mkubwa, mifuko mingine ikawa inamisuse jinsi ya kupata wanachama na wakawa wanatumia

pesa vibaya sasa mingine ikawa inaelekea kufa kwa hiyo tukaona ili kunusuru tukai-*merge* ile mifuko tukaiunganisha tukapata mifuko miwili; PSSSF na NSSF. Kwa hiyo, sasa jukumu la *SSRA* likapungua kwa kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tukaona bora tuiondoe kisheria kwa sababu ushindani ulikuwa umeisha, majukumu yamepungua sana na matumizi bora ya rasilimali ya taifa ambayo tunahitaji sana kwa sasa hivi kwa ajili ya kuijenga nchi yetu tipeleke sehemu nyiningine na majukumu kidogo yaliyobaki tuyaweke chini ya Wizara. Kwa hiyo, sasa *SSRA* ilibaki ni mzigo kwa Taifa letu na ikawa haina msaada tena. Kwa hiyo, naipongeza Serikali kwa ajili ya kuleta sheria ya kuifuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ni suala la michezo ya kubahatisha. Napenda niipongeze Serikali kwa sababu mwenyewe nilikuwa mpinzani sana wa hii michezo ya kubahatisha lakini naipongeza Serikali kwa kusikia kilio changu na kuleta haya mabadiliko ya sheria kwa sababu kumekuwa na wimbi kubwa sana la vijana wanaocheza michezo ya kubahatisha kwa mfano bodaboda na wanafunzi, akina mama wafanyabiashara wote, *VICOBA* wote wanakopa hela wankawenda kucheza kamali, mama wa nyumbani unampa pesa akanunue nyama anaenda kupikia watoto nyanya chungu hela anachezea kamali. Kwa hiyo, naipongeza sana Serikali kwa sababu athari zake zilikuwa kubwa sana katika jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia hii michezo ya kubahatisa ni ajira. Tumeshudia katika nchi yetu sasa hivi kuna shida kubwa ya ajira kwa sababu vyuo vya kawaida na vyuo vikuu kwa mwaka vinatoa wanafunzi zaidi ya laki sita na kumekuwa na tatizo kubwa la ajira. Kwa takwimu ambazo nimezipata ajira ya moja kwa moja ambayo inaletwa na michezo ya kubahatisha ni 20,000, wananchi 20,000 wameajiriwa ambaao ni wengi kuliko watendaji wa kata ambaao hawazidi 4,000 na ni wengi kuliko watendaji wa vijiji ambaao hawazidi 15,000. Na ajira za *indirect*, zisizo rasmi, ni zaidi ya laki moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ambayo inatoa ajira nyingi katika nchi yetu ni elimu ambayo imeajiri watu takribani watu laki tatu na nusu, kwa hiyo, inayofuatia kwa sasa hivi ni hii ajira ya michezo ya kubahatisha ambayo ni zaidi ya laki moja, na inafuatiwa na afya ambayo ni wastani wa lai moja. Kwa hiyo, lazima tuiwekee utaratibu rasmi kwa ajili ya kuiboresha na kui-*monitor*.

Mheshimiwa Naibu Spika, michezo ya kubahatisha ni chanzo cha mapato cha Serikali. Niipongeze hii Sekta ya Michezo ya Kubahatisha, hasa hii taasisi ya *Gaming Board*. Nimeangalia mapato yao, mwaka 2016/2017 ilikuwa bilioni 30, lakini 2017/2018 imepanda kwa shilingi bilioni 78, yaani *ime-double*, na 2018/2019 bilioni 95.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshuhudia kipato hiki ni kikubwa sana ambacho katika matumizi ya kawalda ni bajeti ya Wizara mbili; Wizara ya Michezo na Wizara ya Mazingira ambayo ni bilioni 30 na bilioni 36, yote inakuwa *accommodated* kutokana na michezo ya kubahatisha, na pia Wizara ya Viwanda na Biashara bilioni 100 ambayo kwa wastani ni hela ambayo inaingizwa kutokana na michezo ya Kamali tu. Kwa hiyo, naipongeza Serikali kwa kuleta sheria nzuri ya kuratibu hii michezo ya kamali.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni Sheria ya Kanuni ya Adhabu. Tumeshuhudia ongezeko kubwa la watumiaji wa mitandao ya *internet*. Kwa takwimu za TCRA watu takribani milioni 23 wanatumia *internet* katika nchi hii, kwa hiyo kumetokea na matumizi mabaya ya mitandao ya kijamii, hususani *instagram*, *facebook*, *twitter* na *snapchat*. Watu wamekuwa wakipiga picha mbaya za ajali, tukio mtu amepata ajali familia ina utaratibu wa kuhabarishwa lakini sasa hivi unaweza ukashtukia ukamuona ndugu yako amekufa kwenye mitandao ya kijamii. Kwa hiyo, naipongeza Serikali kwa kuleta sheria kali kwa ajili ya kuratibu hivi vitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda niwapongeze vyombo vyaa habari, watumiaji binafsi wa vyombo vyaa habari, mitandao ya kijamii ambao wanatumia mitandao vizuri kwa

ajili ya kuelimisha na kuacha kuposha kutuma picha mbaya na napenda niwataje; kwa mfano Millard Ayo amekuwa akitumia mitandao ya kijamii vizuri, huwezi ukakuta picha za marehemu katika mtandao kwa mfano wa Millard Ayo; Lemutuz, *Michuzi Blog*, wamekuwa wakitumia vizuri mitandao ya kijamii, huwezi ukakuta picha za hovyo, kwa hiyo, naomba niwapongeze. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache napenda kuunga mkono hoja na tuipongeze Serikali na tuiunge mkono kwa mabadiliko ya sheria hizi. Ahsante sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Jitu Soni, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuchangia jioni hii. Awali ya yote naomba nichukue fursa hii kuishukuru sana Serikali na kuipongeza kwa kuleta mabadiliko haya ya sheria mbalimbali na kwa kweli kwa kuleta hizi sheria kutakuwa na mabadiliko makubwa katika hizi sheria tisa walizoleta sekta hizo zitapata unafuu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijikite katika maeneo mawili; kwanza kabisa niipongeze Kamati ya Sheria Ndogo ikishirikiana na Serikali kwa uchambuzi wa ndani kwa sababu wameweza kutuletea na wakatafsiri ndio maana hakuna Mbunge hata mmoja aliyesimama hapa anahoji, kila mmoja anaunga mkono kwa ajili ya kazi nzuri na kubwa ambayo mmeifanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze Serikali kwa kuleta mabadiliko ya sheria sura 148 katika Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT*). Niipongeze Serikali kwa sababu ile misaada ambayo ilikuwa tupate au zile benki au taasisi ambazo zilikuwa zitukopeshe kwa riba nafuu sasa zitaweza kutukopesha na miradi mingi itaendelea kutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu; kwenye ambayo imewekwa kwa miradi ambayo inatekelezwa na Serikali, naomba kwenye hiyo tafsiri msije mkasahau Serikali za Mitaa, kwa sababu zote, Serikali na Serikali za Mitaa kwenye sheria isipokaa vizuri misaada ambayo itaelekezwa Serikali za Mitaa tunaweza kuja kukwama. Kwa hiyo, naomba m jitahidi katika tafsiri wakati inapowekwa basi suala hilo la tafsiri ya Serikali ya Mitaa muweke ili iweze kutusaidia katika misaada mbalimbali ambayo inakuja katika ngazi hiyo ya halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nipongeze kwa kuondoa kodi katika malighafi kwa kupitia hii sheria katika kiwanda kile ambacho kitazalisha neti za muda mrefu ile cha *A to Z* Arusha, itaweza kuwasaidia ili wawze kushindana katika soko la kimataifa ambapo soko kubwa ndiyo liko huko. Lakini ombi langu ni kwamba pamoja na hii sheria mtaweza kuwaondolea Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT*) kwenye hiyo bidhaa ambayo wanaingiza ya kutengenezea hizo neti, bado hawataweza kuwa kwenye ushindani sawa na wengine kwa sababu tatizo halipo Wizara ya Fedha, tatizo halipo kwenye hizi kodi zetu ambazo zinasimamiwa na *TRA*, tatizo lipo katika hizi *regulatory authorities*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaomba m jitahidi kuleta ile sheria ya marekebisho ya *blueprint regulatory reform*. Hizo ndiyo zitasaidia kuondoa na kupunguza gharama ya uzalishaji kwa sababu hapa mlipoondoa itaondoa kasehemu kadogo sana kwa hiyo bado kwenye ushindani wa bei bado hamtaona mafanikio makubwa. Lakini mkija na zile *reforms* za *regulatory authority* zile tukizifanyia kazi ile *blueprint* nina uhakika gharama ya uzalishaji itapungua na siyo kiwanda hiki kimoja tu, kuna viwanda vingi vitawenza kushindana katika soko la ndani lakini pia katika masoko ya nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu tozo ambazo zinatozwa na hizi taasisi zetu za udhibiti (*regulatory authorities*) ni nyingi sana na ni kubwa. Kwa hiyo, tatizo kubwa halipo Wizara ya Fedha kwa kupitia zile kodi zake ambazo huwa

tunapitisha za *TRA* lakini sehemu kubwa ya uzalishaji, gharama kubwa iko huku kwenye hizi *regulatory authorities*. Kwa hiyo, tunaomba mwezi Novemba kama inawezekana muiletu mapema ili tuifanyie marekebisho inayostahili yale ya kisheria ili gharama za uzalishaji zipungue na watu waweze kuzalisha kwa unafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nishukuru Serikali kwa kuleta katika Sura 41 kifungu 33 hii michezo ya kubahatisha. Nashukuru kwa sababu tatizo hili, pamoja na kuwa ni faida kubwa kwetu, inaingiza mapato makubwa, lakini tayari imeanza kuwa na athari kubwa katika jamii kwa sababu watoto wengi, vijana wengi wameingia huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, Babati limewenza kutokea tatizo wiki iliyopita tu mpaka imefika mahali mtoto wa miaka 12 amevunjwa mikono na amepelekwa hospitali. Sasa hiyo yote ni kwa sababu hizi mashine zimejazwa mpaka vijijini mashine zimejaa, watu sasa hivi wanaona ni bora kuliko kwenda kulima kufanya kazi ajaribu bahati yake. Mmoja kwenye kijiji akiweza kufanikiwa kupata shilingi laki mbili basi wote wanaona kila mmoja atawenza kufanikiwa lakini kwa upande mwingine inatumiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nishukuru kwamba kwa Ibara ya 66 Sura 16 katika matumizi ya kutuma picha mbalimbali, picha ambazo ni za kutisha. Nashukuru kwamba hii sheria sasa imeletwa na imepitishwa. Ombi moja kubwa kwamba tuendelee kutoa elimu kwa wingi, yaani muhimu sana elimu iendelee kutolewa ili watu waweze kuelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata tukiangalia katika mitando mbalimbali kwa mfano hata *TVsza* nje hawaoneshi picha hizi mbaya na za kutisha na wakitaka kuonesha wanatoa tahadhari kwamba kinachofuata kama huwezi kuangalia usiangalie kina *content* ambayo siyo nzuri. Kwa hiyo, niwashukuru kwamba jambo hili litaweza kuweka *privacy*, pia itaongeza haki za watu badala ya picha

mbalimbali wakiwa katika msiba au maeneo ambapo hawataki picha zao zipigwe na zitumwe katika mitandao na kutumika vibaya, itasaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nishukuru kwamba suala zima lile la kwamba bodi ambazo zitakuwa zimeisha muda wake bado patakuwa na fursa ndani ya mwaka mmoja bodi zitakuwa zimeundwa ili kurahisisha na kuhakikisha kwamba shughuli zote za taasisi hiyo ziweze kuendelea kama kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine kama walivyosema Wabunge wenzangu wengi, suala la kuweka *interest* kwenye adhabu. Ninaomba Serikali ifikirie suala hili la *interest* wakati inapotunga ile kanuni yake basi iwe *fair* na iangalie kwa undani. Kwa sababu inawezekana kwamba mtu hakukusudia kufanya kosa hilo, amejikuta kosa limefanyika anatakiwa kulipa adhabu na ile adhabu kwa wafanyabiashara wengine inaweza kuchukua muda kulipa kwa hiyo, bado hujamuondolea adhabu, itakuwa adhabu inaongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiangalia upande wa pili, kwamba je, kama ingekuwa ni kosa hilohilo limetendwa na kwa upande wa pili, upande wa Serikali wao walitakiwa kulipa; je, ingekuwa na wao wanalipa na *interest*? Sasa tungekuwa tunaiangalia kwa sura zote mbili kwamba ingekuwa tunaangalia kwa upande mmoja tu, kama ni *criminal offense* huko nakubaliana lakini kama ni hizi *offenses* za kawaida katika biashara za kawaida basi Serikali iendelee kuwa na ule msamaha na iendelee kuangalia watu wasije wakaitumia sura hii kwa ajili ya kutoza watu ili adhabu iwe kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sehemu kubwa jambo kubwa ambalo nimefurahia ni suala la *VAT* na niipongeze Serikali, muendelee kutuletea hizo *regulatory reforms* ili tuweze kuzifanyia kazi mwezi Novemba ili uchumi wetu uendelee kukua na tuingie katika uchumi wa viwanda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa fursa. Nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa hoja nzuri sana ambayo ametuletea; lakini pia Mheshimiwa Jenista Mhagama na Mawaziri wenzangu ambao wanasi mamia sheria ambazo zimeletwa Mezani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, nichangie tu hoja chache; moja kubwa ni ile rai kwamba tukwamue miradi ambayo imeshaanza kutekelezwa na ambayo kwa masharti ya mikataba inataka msamaha wa VAT utolewe. Niseme tu kwamba ushauri huu ulishatolewa wakati wa majadiliano juu ya Sheria ya Fedha ya mwaka huu na niseme tena kwamba Serikali inaendelea kuufanya kazi ili tupate suluhisho la kudumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachofanya sasa hivi tunafanya uchambuzi wa kina kwa miradi yote ambayo imekwama, mikataba ambayo inahusika, kiasi cha VAT ambacho kinapaswa kusamehewa na basi mapendekezo yatapelekwa kwenye ngazi za maamuzi Serikalini na pale itakapobidi kurekebisha Sheria ya VAT hatutasita kuiwasilisha hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani ni vizuri niseme kwamba Serikali imekuwa inachukua hatua mbalimbali kukwamua miradi hii, na moja wapo Serikali imekuwa inalipia kodi baadhi ya miradi husika lakini pia tumekuwa tunarekebisha vipengele vinavyohusika vya kimkataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, asubuhi leo lilitsemwa suala la kusamehe VAT kwenye taulo za kike, na ninaomba niseme tena kwamba tunaendelea kama Serikali kulifanya kazi kubaini namna bora zaidi ambayo tutawawezesha watoto wetu wa kike na hasa walioko shulen i waweze kupata

bidhaa hizo. Hii ni pamoja na uwezekano wa kuzigawa hizo taulo bure shulen na gharama na bajeti zake, litakapokuwa limeiva tutalileta hapa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nisisitize pia kwamba ni kweli tutazingatia Serikali; maana yake ni Serikali Kuu pamoja na Serikali za Mitaa. Vilevile kuhusu utekelezaji wa kupunguza zile tozo za taasisi za udhibiti, tulianza wakati wa bajeti iliopita na tunaendelea kufanya hivyo, yale yanayohusu marekebishesho sheria tutafanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda niseme tu la mwisho, ni kweli kabisa ilielezwa hapa michezo hii ya kubahatisha inaongeza mapato ya Serikali kama ilivyolelezwa lakini kuna madhara pia. Tunachofanya, madhumuni kabisa ya kuleta marekebishesho haya ni kuhakikisha kwamba tunadhibiti haya madhara na tunayo mikakati thabiti ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kwamba tunakuwa na udhibiti imara lakini pia kuhakikisha kwamba elimu kwa Umma inatolewa ili tudhibiti hizi *addiction* na hii michezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru tena kwa nafasi hii na ninaunga mkono hoja. (*Makof!*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, mtoa hoja.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ya kufanya majumuisho ya mjadala kuhusu Muswada wa Marekebishesho ya Sheria Mbalimbali Na.6 wa Mwaka 2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii pia kwa mara nyingine kuishukuru Kamati ya Bunge ya Sheria Ndogo ambayo ilifanya kazi kubwa sana ya kuuchambua Muswada huu na kwa ushauri wao na mashauriano tuliyofanya na Serikali ambayo kwa kweli kwa kiasi kikubwa yamefanya kazi imekuwa ndogo. Kwa sababu mambo mengi tumeweza kukubaliana na tumeyaingiza katika Jedwali la Marekebishesho. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwashukuru wadau mbalimbali waliotoa maoni yao mbalimbali ambayo mengi tumeyapokea na tumeyafanya kazi. Niwashukuru Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja hii na jumla ya Wabunge nane wamechangia kwa kuzungumza lakini pia Wabunge wawili wamechangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimshukuru pia Mheshimiwa Mheshimiwa Dkt. Mpango, Waziri wa Fedha na Mipango kwa kufanya majumuisho na kuchangia katika kutoa ufanuzi kwenye baadhi ya hoja zilizotolewa na hasa masuala yanayohusu ile Sheria ya VAT. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni mengi sana yametolewa, kwa ujumla kama Serikali tunasema tunayapokea na kila mara tunasema na kusitiza sheria ni kitu kinachoishi. Kwa hiyo, kama kutahitajika tena mahitaji mengine hapo baadaye, basi hatutasita kuyaleta hapa Bungeni kwa ajili ya kuyafanya marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huo, sasa niruhusu nипитие katika Muswada wenyewe. Nitaanza na hii Sheria ya *Energy and Water Utilities Regulatory Authority* ambapo tumepata maoni mengi na mengi tumeshayafanya kazi kwenye Jedwali la Marekebisho. Hapa nitagusia kwa ufupi hoja iliyoibuliwa na Mheshimiwa Sabreena ambaye alikuwa anazungumzia juu ya hili suala la kuffilishwa kwa makosa (*compounding of offences*), Bodi ya *EWURA* ihusishwe katika mchakato huo. Sisi kwa upande wa Serikali tunafikiri kwamba tukisema tuihusishe Bodi katika kufilisha makosa, mlolongo utakuwa mrefu zaidi na kutakuwa na ucheleweshwaji na hatutaweza kufikia ile azma tuliyokusudia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Sheria ya *Ferries* (Sheria ya Vivuko), kwanza katika hotuba ya Kambi Rasi ya Upinzani lakini pia kutoka kwa Mheshimiwa Sabreena, kulikuwa na pendekezo la kutaja zile shughuli mahsusizi zinazokatazwa katika kifungu cha 12(2) cha sheria hiyo. Katika majadiliano yetu na Kamati tulisema wazi kwamba shughuli ambazo zinaweza kukatazwa na nyingi na ukisema

uziorodheshe iko hatari ya kuziacha nyingine. Hata hivyo, kuna kigezo muhimu sana ambacho kinatumika nacho ni kwamba ni shughuli yoyote ambayo inaweza kuhatarisha usalama wa kivuko (chombo) pamoja na lile eneo kwa ujumla, kwa hiyo, shughuli hizo ndiyo zinakatazwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye sheria hiyo hiyo pia kulikuwa kuna maoni kutoka kwa Mheshimiwa Salome Makamba ambaye pia alipendekeza kuwekwe orodha ya makosa yanayozuiliwa kufanyika katika ule umbali ulioelezwa ambapo kivuko kinafanya kazi. Jibu langu kama jibu nillilotoa hapo juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Salome pia alipendekeza adhabu itoke kiwango cha juu kutoka shilingi milioni kumi iliyopendekezwa na Serikali hadi shilingi milioni tano na pengine kwa sababu labda hiyo shilingi milioni kumi iliyopendekezwa na Serikali haina kigezo. Napenda kusema kwamba pendekozo hili la kupandisha adhabu *actually* lilitokana na Kamati yenyewe ambayo Mheshimiwa Salome pia ni mjumbe.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia alikuwa na wasiwasi kwamba Mahakimu wanaweza kupata shida kujuu watoe adhabu gani kwa aina gani ya makosa. Napenda tu kumuondoa wasiwasi huo kwa sababu Mahakimu wamepata mafunzo ya namna ya kutoa adhabu. Kwa hiyo, wao watapima kosa liliofanyika na wataangalia kwa mujibu wa sheria ni adhabu kiasi gani itolewe kwa kosa hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa pia na pendekozo la Mheshimiwa Mariam kwamba kuna boti au wapiga mbizi au waogeleaji ambao wanafanya shughuli zao karibu na vivuko na kwamba wanaweza kushiriki kwenye masuala ya uokoaji ikitokea ajali. Anashauri uwekwe utaratibu ili watakaposhiriki kwenye kazi hizo isisemekane kwamba wamevunja sheria. Mapendekozo hayo yanachukuliwa na masuala mengine kama haya yanaweza kuelezwu vizuri katika Kanuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Sheria ya *Gaming*, kutoka katika hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, kulikuwa na pendekazo kwamba pawepo na mfumo wa kielektroniki wa kudhibiti michezo ya kubahatisha. Napenda kusema kwamba *actually* Serikali imeshaanza kutengeneza mfumo huo. Katika Bunge hili tulipitisha Sheria ya *e-Government* ambayo inatoa mamlaka kwa chombo hiki kuweza kusimamia masuala yote ya TEHAMA ndani ya Serikali. Kwa hiyo, hii ni mojawapo ya michakato inayosimamiwa katika utaratibu huo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kutoka kwenye hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani tena, palikuwa na wasiwasi kwamba Bodi imepewa mamlaka makubwa sana na pengine inaweza kuingilia vyombo vingine vya Serikali hasa vinavyohusika na uchunguzi. Majibu yetu ni kwamba Bodi hapa imepewa mamlaka na majukumu ya kushughulika na masuala ya *gaming* tu (michezo ya kubahatisha) na haitashughulika na masuala mengine. Pia, tunafahamu kwamba viko vyombo vingine vya Serikali, vyombo vya dola, ambavyo vina majukumu ya kijumla kwa mfano, polisi, hawa hawatazuiwa kuingilia kati katika masuala fulani fulani ambapo pengine kuna jinai imetendeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Sheria ya Tafsiri ya Sheria (*Interpretation of Laws Act*), kutoka Hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, palikuwa na mapendekezo kwamba mamlaka ya Makatibu Wakuu kutekeleza majukumu ya Bodi yapunguzwe kutoka miezi kumi na mbili hadi miezi mitatu. Maeleo ya Serikali ni kwamba mapendekezo ya Serikali yanaangalia uhalisia wa hali halisi, wakati mwingine michakato hii ya kuwapata Wajumbe wa Bodi na Wenyevitii ambayo inahusisha michujo na upekuzi inaweza ikachukua muda wa zaidi ya miezi mitatu ndiyo maana tulisema miezi kumi na mbili. Siyo lengo la Serikali kwamba michakato hii itakuwa inachukua miezi kumi na mbili, itakuwa inafanyika kwa haraka inavyowezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Sheria ya *Penal Code* (Kanuni ya Adhabu), kutoka kwenye mchango wa

Mheshimiwa Taska alieleza kwamba suala la upigaji picha, kunaweza kutokea mazingira ya kuhitaji kupiga picha ya yale matukio tuliyosema ya maiti au matukio ambayo yanaweza kuleta mshtuko. Panaweza kuwa na mahitaji ya kupiga picha kwa ajili ya kuhabarisha umma kwa nia njema, lakini pia kwa ajili ya kutunza ushahidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusema kumba katika Jedwali la Marekebisho tumeweka mazingira ambayo mtu anaweza kupita picha hizo na tumesema kuna utaratibu ambao utapaswa kufuatwa. Pia bado Waziri mwenye dhamana anaweza kutengeneza Kanuni ambazo zitaweka pia maelezo na utaratibu mzuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vinginevyo kwenye sheria nydingine pamekuwa na maoni mengi na mapendekezo kama nilivyosema, ni maoni na mapendekezo mazuri ambayo mengine tutayachukua na tutayaangalia na kuona ni namna gani hizi sheria zitakuwa zinatikelezeka na kama nilivyosema, ikionekana haja ya kufanya mabadiliko tena hatutasita kuyaleta hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nihitimishe kwa kusema kwamba nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao mizuri. Tumepokea maoni mengi mazuri ambayo yanalenga kuboresha Muswada huu na hata masharti ya sheria mama na sheria mbalimbali. Kwa ujumla maoni na ushauri uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge ni ushahidi kwamba suala la marekebisho ya sheria kwa lengo la kuboresha utekelezaji madhubuti wa sheria zilizopo ni jambo muhimu linamhusu kila mmoja wetu na ni jambo endelevu. Ndiyo maana kila mara na kila mwaka Serikali inakuja na Miswada ya aina hii ya kurekebisha sheria mbalimbali ili kuboresha masharti yaliyomo katika sheria hizo kuzifanya ziendane na wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, kwa hivyo tutaendelea na utaratibu wetu, Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

### **KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI - KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.6) wa Mwaka 2019 [The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 6), Bill, 2019]**

Ibara ya 1  
Ibara ya 2  
Ibara ya 3  
Ibara ya 4  
Ibara ya 5

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 6

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salome Makamba.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika Ibara hii ya 6 nilikuwa nimeshauri kifungu cha (3) kifutwe kwa sababu ni kifungu ambacho kinalazimisha mtu ambaye kosa lake limefifilishwa anaposhindwa kulipa deni ambalo amekubaliana na limefifilishwa basi mtu huyo atatozwa riba. Nimeomba kifungu hiki kifutwe kwa sababu sioni sababu ya msingi ya mtu kutozwa riba kwenye kosa ambalo amekubali, hasa

ikizingatiwa kwamba kama amekubali na ameshindwa kulipa hata ukimtoza riba hawezi kulipa. Kwa hiyo, nilikuwa nashauri kifungu hiki kifutwe ili tuweze kuendelea na taratibu zingine za kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salome kwa sababu hiki kifungu cha 6, naona una marekebisho (a) na (b). Hapo umezungumzia (a), kwa hiyo, malizia na (b) kwa sababu yote yanazungumzia kifungu kimoja.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kipengele cha (b), nilikuwa nashauri hiki kifungu kidogo cha (4) cha Ibara ya 6 kifutwe na kiandikwe upya kama ifuatavyo: *"Where the person fails to comply with the compounding order issued under subsection (1) above within prescribed period, the Authority may enforce the compounding order in the same manner as the decree of the court".*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa faida ya wote, kama kifungu cha (3) kitafutwa maana yake ni kwamba mtu ambaye atashindwa kulipa kosa liliolifilishwa kwenye kifungu cha 42A(1), ina maana Serikali au mamlaka inaweza ikachukua ile *compounding order*, yale makubaliano ya kulipa na kupeleka Mahakamani ili waweze kuiomba Mahakama imueleze mtu yule aweze kulipa. Mahakama itafanya vile kwa mujibu wa *Order XXXV ya Civil Procedure Act*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kujibu pendekezo alilotoa Mheshimiwa Makamba, nataka kuibua suala la kiteknikali, sijui kama tafsri ya neno teknikali ni ufundi, suala la kiufundi kwa namna alivyofanya rejea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu niseme kwamba suala hili liliijitokeza pia tulipokuwa tunajadili Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na.5 ambapo palikuwa pana rejea isiyo sahihi (*wrong referencing*) na hiyo ikapelekeea aliyekuwa amekalia Kiti kutoa maelekezo kwamba yanapoandaliwa Majedwali ya Marekebisho ni vyema kupata msaada na ushauri wa Sekretarieti ya Bunge ili Majedwali haya yaandaliwe kwa njia sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada ambao tunaujadili unabadilisha sheria halafu Jedwali linabadilisha au linarekebisha Muswada. Kwa hiyo, kwenye Jedwali unapokuwa unafanya rejea, unarejea kwenye Ibara zilizopo kwenye Muswada. Muswada unafanya rejea kwenye vifungu vya sheria. Hapa Mheshimiwa Makamba amefanya rejea kwenye Muswada na akachanganya na rejea kwenye sheria kwa wakati huo huo mmoja kiasi kwamba kwa lengo na nia ya kumbukumbu zetu *Hansard* itatuchanganya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Makamba amesema, *the Bill entitled, the Written Laws Miscellaneous Amendment No. 6 Act 2019, is hereby amended as follows.* Kwa hiyo, *the Bill is amended in clause 6.* Anasema (a), by deleting the proposed subsection (3). Hiyo ni mchanganyiko kwa sababu ukienda kwenye Muswada haukuti subsection (3) ilipaswa aseme subclause (3) kama ingekuwepo. Hivyo hivyo, ile (b) anayosema, *deleting the proposed subsection (4),* hiyo ilipaswa kuwa ni subclause (4) na haipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa labda kabla sijaendelea niombwe mwongozo wako.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, ni kweli kwa mujibu wa Kanuni zetu tunaongozwa na maamuzi ya Kiti ambayo yamepita lakini pia na Kanuni zetu. Kulingana na miongozo hiyo, ukiangalia marekebisho ya Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili tutumie mfano mzuri na ulio dhahiri na ukiyashika na marekebisho ya Mheshimiwa Salome Makamba, ukienda kwenye (a), ukurasa wa 1 wa marekebisho ya Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali,

yameandikwa kwa namna ambayo yanafanana na ya Mheshimiwa Salaome Makamba. Marekebisho ya Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali yanaanza kwa kusema, *in clause 6, by (a), deleting the proposed subsection (2).* Mheshimiwa Makamba marekebisho yake pia yanasomwa hivyo, *(a), in clause 6 by, deleting the proposed subsection (3).*

Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, maelezo ambayo umeyatoa hapa ambayo nimeyaelewa sana na Mwenyekiti ndiye alikuwa amekalia Kiti wakati huo, ni pale ambapo kifungu ambacho kinazungumzwa kwa namna kilivyoandikwa kinazungumzia jambo ambalo halipo kwenye Muswada. Sasa nikiwa nimeushika Muswada hapa, naona unasema, *the Principal Act is amended by adding immediately after section 42, a new section* na kuendelea na yeze Mheshimiwa Salome Makamba ameandika, *in clause 6, ambayo ndiyo hii hapa 6, by (a), deleting the proposed subsection (3).*

Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu, sasa nikienda kwenye yale ya kwako yanaenda hivyo hivyo. Inasema, *in clause 6, by, (a) deleting the proposed subsection (2),* kwa hiyo, yanafuata ule mtiririko. Pengine kama mimi ndiye nayeona tofauti wewe utoe maelezo ya ziada ili sasa tuweze kusonga kwa mujibu wa Kanuni zetu kwa haya marebebisho ambayo ameyaleta Mheshimiwa Salome Makamba.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilihitaji mwongozo, nadhani maelezo yako yametupatia mwongozo wa namna fulani, kwa hiyo, nafikiri tunaweza tukaendelea na kujadili marekebisho yaliyopendekezwa na Mheshimiwa Makamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nitaanza na hiyo *clause 6 kifungu chake cha (a) ambapo anapendekeza kufutwa kwa sub-section 3 ambayo itakuwa imeongezwa katika sheria na sub-section* hiyo inazungumzia masuala yakuondoa ile riba (*interest*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala hili tulijadiliana kwa kirefu sana na Kamati na Mheshimiwa Makamba naye ni Mjumbe wa Kamati hiyo. Tulisema kwamba baada ya Serikali kupokea pendekexo la kufuta kile kifungu kidogo cha (2) ambacho kilikuwa kiliwa kunazungumzia masuala ya kumpeleka huyu mtu Mahakamani ni vyema Serikali ingebaki na *option* ya kutoza riba ili iwe msukumo kwa huyu mtu kuona kwamba ana faini ya kulipa na kwa hiyo, asichelewe kulipa. Vinginevyo kama hakuna hiyo riba, basi anaweza akachukua muda wowote anaotaka kulipa hiyo faini kwa sababu anajua pia hatapelekwa Mahakamani baada ya kuwa amekubali kulipa faini hiyo katika ule utaratibu wa kufirisha kosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ilikuwa ni kama makubaliano kimsingi na Kamati kwamba, basi kama tunaondoa ule utaratibu wa kumpeleka Mahakamani baada yakufilisha kosa, basi serikali pia ibaki na *option* ya kutoza riba.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salome Makamba.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru. Kama sitaeleweka, nitaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu waniunge mkono wanisaidie kufafanua kuhusu hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja iliyopo hapa ya kwa nini naomba kifungu Na. 3 kifutwe, ni kwamba mtu amefanya kosa, amekiri, kwamba nimefanya kosa, akakubali kulipa faini kwamba nitalipa. Amekwama; na *section 3* inasema, *where a person fails*; siyo kwamba amekataa, amekwama kulipa ile hela kwa sababu mbalimbali, sasa Serikali inawongezea faini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio maana nikasema hicho kifungu kifugwe kwa sababu kama nimeshindwa kulipa ile ndogo ambayo tumekubaliana, hiyo kubwa nitaitoa wapi? Pia zipo njia mbalimbali ambazo Serikali inaweza zika *enforce*, zikatumia; nilisema hapa, nilichombeza kidogo

kuhusu Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Madai; Serikali inaweza kutumia namna ya kupata haki yake ya yule mtu aliyekubali na aliyekiri kosa kupitia Sheria ya Mwenyendo ya Makosa ya Madai na haichukui muda mrefu. *Summary procedure* inaruhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe hoja Wabunge wenzangu wanisaidie kulifafanua hili kwa maslahi mapana ya wafanyabiashara hasa katika sekta hii ya mafuta na nishati ya *EWURA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tafadhalii waniunge mkono.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kabla hamjaunga mkono hii hoja, hebu tuelewane vizuri, hili linakuwa ni deni kwa sababu mmeshakubaliana. Sasa kuna deni ambalo linaweza likasubiri miaka bila kudaiwa fedha kwa kuchelewesha kulipwa? Yaani kuna mtu amekopa mahali, miaka tatu ijayo amekopa shilingi 3,000/= akaja kulipa kulipa shilingi 3,000/= hiyo hiyo? Hebu tusaidie Mheshimiwa Salome.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwanasheria Mkuu wa Serikali alipokuja kwenye Kamati itaeleza vizuri kwamba kutakuwepo na *form specific* ambayo itaeleza namna ambavyo lile kosa liliolofilishwa litalipwa. Sasa ni matumaini yangu kwamba hiyo fomu itakuwepo kwenye kanuni na kwamba itaeleza muda muafaka wa ulipaji wa hilo deni ambalo wamekubaliana. Endapo muda ule utakuwa umekwisha; na niliwauliza vizuri, kwa nini mna-*entertain interest* na ham-*entertain extension of time?* Hammwongezei muda?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama muda ule utakuwa umekwisha na deni halijalipwa, Serikali inaweza kwenda Mahakamani kuiomba Mahakama imwelekeze yule mtu ali pe lile deni alikubaliana na Serikali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salome na wewe unafahamu wazi, ukishaenda Mahakamani, Mahakama itakaposema huu ni uamuzi sasa wa Mahakama, lazima utalipa na za ziada ukichelewasha kulipa. Si ndiyo utaratibu ulivyo? Sasa sheria ikisema hivi kuna tatizo gani? Kwa sababu hoja ni kwamba deni huwezi kukaa nalo halafu ukawa hulipi hiyo riba. Lazima ulipe riba. Hata hukumu za Mahakama, ukichelewa, riba inaongezeka.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge hapa mlikuwa mnaunga mkono hoja ya Mheshimiwa Salome, lakini kimsingi ni kwamba sheria hivi ilivyowekwa ndivyo utaratibu ulivyo, hakuna deni ambalo huwa linakaa hiyo hata ukishindwa kulipa. Utamaduni ni huo. Wabunge wenyewe hapa mna mikopo, kuna mtu akichelewesha kulipa hela analipa ile ya mwezi uliopita? Si huwa inaongezeka juu yake nyingine?

Nadhani hili Waheshimiwa Wabunge, kwa utararibu wa namna sheria zinavyotengenezwa tukubaliane na wazo la Serikali, kwa sababu ndivyo sheria zinavyotengenezwa na ndivyo zinavyotaka. Hili la Mheshimiwa Salome hata tukipeleka Mahakamani litaturudisha hivi hivi ilivyoandikwa sheria hapa.

Kwa hiyo kifungu hiki kilikuwa na marekebisho ya Serikali pia. Kwa hiyo, ya Mheshimiwa Salome kwenye hii Na. 6 kwa maeleo hayo nadhani Waheshimiwa Wabunge mtakuwa mmelewa, tutakuwa tunaitunga sheria wenyewe kwa namna ambayo itakuwa ngumu kutekelezeka.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 7

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 8

*(Ibara iliyo tajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na marekebisheso ya Serikali)*

Ibara ya 9

Ibara ya 10

Ibara ya 11

Ibara ya 12

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 13

*(Ibara iliyo tajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima pamoja na marekebisheso ya Serikali)*

Ibara ya 14

Ibara ya 15

Ibara ya 16

Ibara ya 17

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 18

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salome Makamba.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kifungu cha 18 kinachohusiana na Sheria ya Ferry, bila kusoma kwa ajili ya muda, Serikali ilikuja na mapendeleko ya kwanza kwamba, mtu ye yoyote atakayeingilia utendaji kazi wa kivuko, atatakiwa kutozwa faini ya shilingi 50,000/= au shilingi 500,000/= na baadaye wamebadilisha, nimeona kwenye marekebisheso yao wamefika mpaka shilingi milioni kumi. Msingi wa kufika shilingi milioni kumi ilikuwa ni aina ya makosa au hizo *activities* ambazo zikifanyika kwenye kivuko zinaweza zikakwamisha kivuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uchache tu niseme, aina makosa hayo inaweza kuwa mtu ameogelea, lakini yapo mengine ambayo ni makubwa zaidi, labda mtu amefanya uvuvi kwa kutumia mabomu jambo ambalo linaweza likahatarisha maisha ya watu. Sasa nilliomba Serikali hata kwenye Kamati, basi walete jedwali angalau kwa uchache linaloeleza aina ya hizo *activities* wanazisema na makosa yake ili liweze kutoa mwongozo kwamba tunapoweka adhabu kuanzia shilingi 50,000/= mpaka shilingi milioni kumi tulikuwa tunalenga hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekataa na balada yake wamekuja kubadilisha kifungu cha adhabu, jambo ambalo naona kama Serikali imekuwa na mtazamo wa kuingiza pesa badala ya kutibu changamoto ya watu wanaoweza kuingilia kivuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kuleta mjadala mrefu, kama Serikali imeamua kuweka adhabu, mimi naona shilingi milioni kumi ni fedha nydingi sana, wapunguze angalau basi iwe shilingi 50,000/= mpaka shilingi milioni tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ndiyo marekebisho yangu katika kifungu hiki. Nashukuru.

**MWENYEKITI:** Sasa Mheshimiwa Salome, marekebisho yako niliyonayo hapa mbele hayazungumzii hizo shilingi milioni tano ambazo unapendekeza wewe. Ilikuwa ni kufuta shilingi 500,000/= na kuweka shilingi milioni tano, ambayo na wewe unaiongea hiyo adhabu, wakati hata na wewe hujaleta hayo marekebisho unayoyasema ya kwamba ni makosa yapi sasa yapewe hiyo shilingi milioni tano uliyoweka.

Kwa sababu na Serikali ilichofanya, imeongeza kile kiasi cha fedha. Sasa unasema kutoka shilingi 500,000/= tuishie shilingi milioni tano ndiyo unayopendekeza, Serikali imeenda mpaka kumi. Sasa kwa kuwa makosa yale hayajaorodheshwa hapa na umesema mengine pengine ni

ya hatari zaidi, kwa nini usione kwamba hii hoja ndiyo hii ambayo Serikali inataka ku-*address* kabla Mheshimiwa AG hajajibu hapa?

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimimiwa Mwenyekiti, nashukuru umenielekeza vizuri. Msingi wa mimi kupunguza kutoka milioni kumi kwenda milioni tano ni *experience* ambayo Tanzania tunayo juu ya aina ya hayo makosa ambayo tulijaribu kuya-*foresee*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Tanzania hii haijawahi kutokea hata mara moja mtu amekwamisha kivuko kwa sababu amevua kwa mabomu hajawahi kutokea, wala haijawahi kutokea *propeller* za kivuko zimeharibika kwa sababu mtu amevua kwa nyavu. Kwa hiyo, *possibility* kubwa ya makosa yanayoweza kutokea ni makosa madogo madogo kama kuogelea, watu kufanya shughuli zao za kijamii kwenye eneo la *ferry* ambapo kwangu mimi naona kwa aina ya makosa ambayo yamewahi kutokea, kuweka kiwango cha shilingi milioni tano kama kiwango cha ukomo wa adhabu, inaleta maana zaidi kuliko kupata shilingi milioni kumi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo la kupandisha adhabu kile kiwango cha juu cha adhabu kutoka shilingi 500,000/= lilitoka kwenye Kamati na Serikali ilitoa pendekezo la shilingi milioni kumi na Mheshimiwa Makamba anatoa pendekezo la shilingi milioni tano. Kimsingi wote tumetoa mapendekezo. Serikali ilijaribu kuangalia baadhi ya makosa ambayo yakifanyika na hasa madhara yanayoweza kutokea baadhi ya makosa hayo yakifanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu makosa, tulisema kwamba siyo rahisi kuyaodhoreshwa hapa yote katika sheria hii, lakini ipo nafasi wakati wa kutengeneza kanuni, kanuni

hizo zinaweza zikaorodhesha makosa hayo na zikaweka wazi zaidi namna sheria hii inavyoweza kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Makamba, kikanuni nilikuwa natakiwa nikuruhusu kuzungumza, lakini kimsingi Waheshimiwa Wabunge mnayo haya mapendekezo ya Mheshimiwa Salome Makamba. Kuna makosa kidogo, sasa hata kama tutawahoji Wabunge kwa kutumiwa hiki, maana yake tutakuwa tunatunga sheria ambayo imeshakosewa tayari.

Hebu soma vizuri mapendekezo yako yanasema *five millions shilling*; sasa huwa hakuna *five millions shilling*. Huwa ni *five million shillings*. Kwa hiyo, tukiyachukua haya ndiyo tuyaweke hapa, tutakuwa wenyewe tumekosea kwa namna hiyo, kwa sababu hatuwezi kurekebishi hapa ndani. (*Makofii*)

Kwa sababu hiyo Waheshimwa Wabunge, haya mapendekezo ya Mheshimiwa Salome Makamba nadhani mmeelewa hoja yake ilikuwa wapi. Kwa hiyo, hili ndiyo Bunge linatunga sheria, kuna fursa ya marekebisho tena huko baadaye.

*(Ibara iliyo tajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 19

*(Ibara iliyo tajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 20

*(Ibara iliyo tajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 21

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 22

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 23

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 24

Ibara ya 25

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 26

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 27

Ibara ya 28

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 29

Ibara ya 30

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 31

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 32  
Ibara ya 33  
Ibara ya 34  
Ibara ya 35  
Ibara ya 36

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima pamoja na marekebishi ya Serikali)*

Ibara ya 37

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 38

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima pamoja na marekebishi ya Serikali)*

Ibara ya 39  
Ibara ya 40  
Ibara ya 41  
Ibara ya 42  
Ibara ya 43  
Ibara ya 44  
Ibara ya 45  
Ibara ya 46  
Ibara ya 47  
Ibara ya 48  
Ibara ya 49  
Ibara ya 50  
Ibara ya 51  
Ibara ya 52  
Ibara ya 53  
Ibara ya 54  
Ibara ya 55  
Ibara ya 56  
Ibara ya 57  
Ibara ya 58  
Ibara ya 59

Ibara ya 60  
Ibara ya 61  
Ibara ya 62  
Ibara ya 63  
Ibara ya 64  
Ibara ya 65

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 66

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 67

*(Ibara iliyotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 68

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 69

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 70

**MWENYEKITI:** Kifungu cha Sabini kina marekebisho ya Mheshimiwa Makamba.

**MHE. SALOME W. MKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kifungu cha sabini ni sheria inayohusiana na Utumishi wa Umma na inampa; naomba nisome tu, inasema: “*The principle act is amended by adding immediately after section 26 the following new sections:*

*Notwithstanding any other condition from to the contrary the Chief Secretary shall have power to exempt a public servant from any condition required for grant of pension and other terminal benefit."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwenye mchango wangu hapo awali, kifungu hiki kinampa mamlaka Katibu Mkuu Kiongozi kuweza kumpatia mtu aliyestaafu; tafsiri yangu siyo ya moja kwa moja, lakini ni mtumishi wa Umma aliyestaafu *termination benefits* zake, yaani kumu-exempt kwenye *condition* yoyote ambayo inaweza ikamfanya asipate *termination benefit*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lako Tukufu ni Bunge la watu makini sana na sitegemei tunaweza tukatunga sheria ambayo inakinzana yenyewe kwa yenyewe. Sheria tuliyotunga mwaka 2018 sheria Na. 2 ya mwaka 2018 inayohusiana na *Social Security Fund* iweka wazi *conditions* ambazo mtu anatakiwa ku-comply nazo ili aweze kulipwa *pension* yake na *termination benefit*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na yote hayo, imeweka Bodi ambayo itafanya kazi kwa umakini na Waziri amepewa dhamana, akatunga kanuni, vile vikokotoo, tukakubaliana navyo na Mheshimiwa Rais akaingilia. Leo tunampa Katibu Mkuu Kiongozi Mamlaka ya kuweza kumwondolea mtu hizo *conditions* ambayo zipo kwenye sheria ile. Kwa nini hawasema, lakini anaweza akaondolewa na akalipwa hata kama hajatimiza vigezo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi *personally* na Kambi Rasmi ya Upinzani tunaoina sheria hii inakinzana na sheria tulipitisha mwaka jana. Kwa hiyo, naitaka Serikali kufuta kifungu hiki ili tuweze kuendelea na sheria ambayo tulipitisha ndani ya Bunge lako. Nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salome, hebu rudia kusoma kuanzia hapo "*have power to...*"

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, inasema; “*have power to exempt a public servant from any condition required for grant of pension or other terminal benefits.*”

**MWENYEKITI:** Kwa maelezo hayo yaliyoko hapo huoni kama *Chief Secretary* anapewa mamlaka ya kuangalia yale masharti ambayo huyu mtumishi wa umma kuna masharti hayo tuliyoyatunga kwenye sheria ambayo ye ye yanamfanya asipate mafao, kwa hiyo anawekewa kifungu kwamba huyu Kiongozi mkubwa anayetazama utumishi wa umma amuangalie huyu mtu ambae mazingira yake ameshindwa kutimiza kigezo fulani kimoja kinamfanya asipate kabisa hiyo *pension* ndiyo lengo hasa lilioandikwa hapa, lakini maelezo uliyoyatoa ni kana kwamba anapewa nguvu za kumnyima mtu *pension*.

Kifungu kina lengo la kumpa nguvu ili apewe mtu *pension* ambae kuna masharti fulani ambayo sheria tuliyotunga yanataka yote yatimie. Kwa mfano, sheria inataka tuseme awe amechangia miezi 20, si ndiyo? Nataja kwa mfano au mingi huwa ni 120 kitu kama hicho nadhani. Kama ye ye amefikisha 119 ule mwezi mmoja unamfanya asipate *pension*. Kifungu hiki kinataka yule wa mwezi mmoja, yule *Chief Secretary* akiangalia mazingira ule mwezi usimfanye huyu akose *pension* ndiyo lengo la kifungu. (*Makofii*)

Kwa hiyo yale maelezo uliyokuwa umeyatoa mwanzo ili hiki kifungu tukifute sasa ndiyo usimame ili Mheshimiwa *AG* aweze kujibu. Nitataku uweke sawa hii maana ya hiki kifungu ambacho unataka kukifuta.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitafsiri tu, nafikiria kwa Kisukuma, naongea kwa Kiswahili kidogo tafsiri inakuwa ngumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lengo langu na niseme tu wazi, lengo la Serikali ni zuri, inawezekana mtumishi wa umma amechangia kama ulivyoeleza vizuri sana, lakini hajatimiza vigezo, sasa kwanza tukumbuke kwamba *Chief*

Secretaryndiye Mwajiri Mkoo wa Serikali, mwajiri namna moja hao wengine wanakasimiwa tu mamlaka. Unavyompa mamlaka hiyo dhana unayosema wewe ya kumuondolea vikwazo nya aina yoyote mtumishi wa umma ambae amechangia ili aweze kupata haki yake tayari umeshaingiza mgongano wa kimaslahi, maana yeye ndiyo anatakiwa athibitishe kwamba huyu mtu kweli amefanyakazi, amefanya vizuri na namna hiyo, tayari umeshaweka mgongano.

Ninachotaka mimi nikiseme, lengo hili la Serikali kuliweka kwenye Sheria ya Utumishi wa Umma tuna-*overrule* ile *decision* ambayo tuliamua kuweka hili lengo kwa Bodi ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na Waziri, kwa hiyo, ninachokisema tukiweka hapa *Chief Secretary* akawa ndiye mtu anayeweza kusema, *okay* huyu mtu kachangia miezi kadhaa kidogo, lakini alipwe tunaingiza mgongano wa kimaslahi kwanza, lakini pilli tunakinzana na masharti tunayojiwekea wenyewe kwamba ili mtu aweze kulipwa, *condition* zitakuwa *determined* na Bodi na Waziri wenye dhamana ndiye mwenye mamlaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo lengo langu Serikali wameleta sheria nzuri lakini kwenye eneo ambalo halihusiki, hilo ndiyo nilitaka kusema.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkoo wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa maelezo kwa kifupi kabisa halafu nimuombe Waziri, Mheshimiwa Jenista aweze kutoa maelezo ya ziada kwa ruhusa yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 70 inarekebisha Sheria ya *Public Service*, lakini rejea aliyoifanya Mheshimiwa Makamba ni ile Sheria ya *PSSSF*, nilitaka tu nitoe angalizo hilo. Sheria hii ya *Public service* ndiyo ina-*cut across* utumishi wa umma kwa ujumla, lakini ile Sheria ya *PSSSF* inahusu masharti katika mifuko na kwa hiyo, hauna mgongano na kuna misingi ya kisheria (*lex specialis* na *lexis generalis*) masharti ya ujumla

na masharti mahususi, basi ikigongana unatumia ile sheria inayozungumzia masharti mahsusи.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba kwa ruhusa yako Mheshimiwa Jenista aongezee maelezo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jenista Mhagama.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza niungane na Mheshimiwa AG kwa sababu ya namna ambavyo muswada huu umeleta marekebisho ya sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hii kama alivyosema *AG*imejikita kwenye ku-*amend* Sheria ya Utumishi wa Umma na tunajua majukumu ya *Chief Secretary* kwenye utumishi wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini umezungumza jambo zuri sana, umeeleza nini ambacho *Chief Secretary* atakifanya katika ile *due procedure* yote ya kumfanya mtumishi awe *awarded* kile anachotakiwa kukipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama anataka kwenda kwenye Sheria ya *PSSSF*; kwenye Sheria ya *PSSSF*kuna mfumo mzima wa utaratibu wa malipo ya *pension*, lakini uko pia mfumo wa kufanya *exemption* na mfumo huo kama anataka ku-refer kwenye sheria hii sasa ya mafao ya utumishi wa umma akienda kwenye kifungu cha 46 na vifungu vingine vinavyofuata atakuta *authorities* ambazo zimetajwa zinaweza kuwa na mamlaka ya kutoa *recommendation* ya kupelekea kwenda kuweka huo utaratibu mzima wa msamaha na mamlaka ambazo zimepewa nafasi ya kufanyakazi hiyo na *Chief Secretary* pia ametajwa kwenye Sheria hii ya *PSSSF*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi nafikiri hapa tukiendelea kujikita kwenye ku-*amend* Sheria ya Utumishi wa Umma tunaweza tukamtazama *Chief Secretary* kwa

majukumu yake kama kwenye Sheria ya Utumishi wa Umma, lakini ukifika kwenye sheria zetu ukiniacha mimi Waziri, ukiliacha bodi, lakini viko vifungu vingine pia ambavyo vinazungumzia kutoa msamaha na unakuta kwenye vifungu vile mpaka Mheshimiwa Rais anatajwa katika mlolongo ule wa kutoa msamaha na ziko *authorities* ambazo zinatajwa katika utaratibu ile *due process* yote ya kutoa huo msamaha.

Kwa hiyo nadhani tujikite kwenye Sheria ya Utumishi wa Umma ambayo inakuwa *amended* hapa, lakini haina *effect* yoyote kwenye ile sheria nyingine ya PSSSF.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge nadhania tunakwenda pamoja. Kifungu hiki kina lengo la kumpa mfanyakazi wa umma faida zaidi kuliko kumpunguzia faida. Mheshimiwa Salome pia amekaa, kwa hiyo, naamini ameelewa.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tena Mheshimiwa Jenista amenisaidia vizuri sana; *powers* za kutoa *exemption* kwenye Sheria ya hiyo PSSSF ziko *vested* kwa *President*, nitasoma kifungu namba 46 kinasema; "A President may exempt from certain condition. A member may by application to the President supported by affidavit and on recommendation of a specified authority apply for exemption from the application to him, any condition under this act."

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo anachokisema Mheshimiwa Jenista siyo kweli kwamba wanachokifanya ni kurekebisha kifungu cha 27, kifungu cha 27 ni kipyा ndiyo kimeanzishwa. Kimeanzishwa kwenye hii Sheria ya Utumishi wa Umma na wamekianzisha *specifically* kwa ajili ya kumpa nguvu Katibu Mkuu Kiongozi kumu-*exempt* mtumishi kwenye *any condition* ambazo alitakiwa azifuate kwa Sheria Namba Mbili ya 2018 kumu-*exempt* ili aweze kulipwa. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi inawezekana sieleweki, niombe Wabunge wenzangu wanisadie kufafanua na waniunge mkono. Sheria hii imewekwa kwenye sheria ambayo haihusiki. *Improvement* kama Serikali inataka kufanya wakafanye kwenye Sheria ya PSSSF na siyo Sheria ya *Public Services*. Naomba tafadhali Wabunge wenzangu mniunge mkono. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Hoja haijaungwa mkono kaa Mheshimiwa Salome

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Lakini pamoja na hayo, hoja haijaungwa mkono hamko 10 hata sasa miliosimama mnabisha nini sasa na mko sita?

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ulikuwa unaongea.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hawa hiyo inaitwa *after faults*. Watu waliosimama ni sita pamoja na wewe, lakini hata hivyo kaa nataka kutoa maelezo kidogo.

Waheshimiwa Wabunge, nataka kutoa maelezo kidogo kwa sababu Mheshimiwa Salome amesema anachokisema Mheshimiwa Jenista siyo sahihi. Kifungu cha 46 kimetaja pale watu wenye vyeo mbalimbali na haijasema yaani Rais ndiyo amekaa kule juu, lakini kuna watu wanaompelekea hizo taarifa na ndiyo wametajwa hapa na hii sheria. Kwa hiyo hakuna kilichokosewa na alichokuwa anaeleza Mheshimiwa Jenista.

Mheshimiwa Salome uwe unasoma vizuri na ndiyo maana akakwambia endelea kusoma. Umeviona vifungu vinavyofuata hapo? Rais yeye anapata wapi hizo taarifa? *Specified authority* imekuwa *defined* umesoma? *Definition* ya *specified authority* ni *President*?

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *with due respect*, Mheshimiwa Jenista wakati anaeleza alisema kwamba wanafanya marekebisho ya Sheria ya Utumishi wa Umma sasa wanafanya...

**MWENYEKITI:** Haya hapo umeshaeleweka kaa Mheshimiwa Salome, umeshaeleweka kaa Mheshimiwa Salome, umeshaeleweka. Wewe ndiye uliyemsikia hayo unayoyasema kwa sababu ili mimi nijiridhishe kwamba ndicho alichokisema unachosema wewe mimi naangalia kile ulichotaja kuhusu kifungu, hayo maelezo aliyoyatoa mpaka niite hapa Taarifa Rasmi za Bunge ambazo sina. Kuwepo Mheshimiwa Hawa na wewe, kwa hiyo wewe ulivyokuwepo mbona umesimama kuunga mkono hoja wakati imeshapita? (*Kicheko*)

Kwa hiyo, nawaambia kila siku ubongo wa mwanadamu unachangua cha kusikiliza, kwa hiyo huwezi kunilazimisha kwamba nimesikia hayo maneno. Natoa maelezo ya yale niliyoyasikia kwamba hiki kifungu namba 46 kinataja watu wenyewe vyeo mbalimbali kulingana na yule mtumishi anayezungumziwa ndiyo ilikuwa hoja hapa. Kwa hiyo, hiki kifungu kilichowekwa hapa kinatajwa kwa mamlaka yale ambayo *Chief Secretary* au Katibu Mkuu Kiongozi ana mamlaka nayo. Kwa hiyo, hiki kifungu namba 27 kinaingia kwenye sheria inayomuhusu *Chief Secretary* na nataka kufikiri Serikali kadri inavyoangalia kwasababu ile sheria pia haitamhusu kila mtu.

Kwa hiyo, pengine hizi taasisi mbalimbali zilizotajwa hapa kwenye 46 na zenyewe zitakuwa zikitazamwa ili kama kwenye hizo sheria pia kuna mapungufu kuna haja ya Bunge kuweka mazingira yale ambayo mfanyakazi ambaye amefanyakazi ya kulichangia Taifa hili hatakosa *pension* ama *mafao* wakati anamaliza utumishi wake.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu iliptishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu iliptishwa na Kamati ya  
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 72

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 73

*(Ibara iliyotajwa hapo juu iliptishwa na Kamati ya  
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 74

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 75

*(Ibara iliyotajwa hapo juu iliptishwa na Kamati ya  
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 76

Ibara ya 77

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 78

Ibara ya 79

Ibara ya 80

Ibara ya 81

Ibara ya 82

Ibara ya 83

Ibara ya 84

Ibara ya 85

Ibara ya 86

*(Ibara zillzotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 87

Ibara ya 88

Ibara ya 89

Ibara ya 90

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima pamoja na marekebishi ya Serikali)*

Ibara ya 91

*(Ibara iliyotajwa hapo juu iliptishwa na Kamati ya  
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 92

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima pamoja na marekebishi ya Serikali)*

Ibara ya 93

Ibara ya 94

Ibara ya 95

Ibara ya 96

*(Ibara zillzotajwa hapo juu ziliptishwa na Kamati ya  
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 97

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima pamoja na marekebishi ya Serikali)*

Ibara ya 98

Ibara ya 99

*(Ibara zillzotajwa hapo juu ziliptishwa na Kamati ya  
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 100

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Catherine Ruge.

**MHE. CATHERINE N. RUGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana kabisa na mapendekezo yaliyoletwa na Serikali kwenye kifungu cha 100(b)(i), (ii) na (iii) pamoja na 100(c). Kwa muktadha huo ambao umeifanya Serikali kuleta mapendekezo haya, nilikuwa naomba marekebisho yangu yaweze kuingizwa kwenye hii sheria ambayo ningependa kiwe kifungu 100(d) na naomba nikisome kama ifuatavyo:-

*"Importation by a person, company or private sector of goods or service to be useful for the public interest".* Kama nia ni nzuri ya kuweza kukwamua miradi ya maendeleo, lakini pia *private sector* inaweza ku-import aidha *raw materials* au vifaa kwa ajili ya kusaidia jamii au *CSR activities*, kwa hiyo na wao basi wapewe msamaha wa VAT kwa hivyo vifaa ambavyo wanaingiza. Nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Catherine Ruge hebu tusomee hicho kifungu kitasomekaje ukishakiweka hapa kwa sababu kwenye marekebisho yako kinaingia kwenye 2(b)(iv), hebu tusomee kuanzia hii *opening statement* hapa.

**MHE. CATHERINE N. RUGE:** *"Importation by a person, company or private sector of goods or service..."*

**MWENYEKITI:** Ngoja, ngoja, ngoja hapa inapoongezeka maana yake usome hii (b) halafu uunganishe na haya ya kwako uliyoyaweka hapa.

**MHE. CATHERINE N. RUGE:** *"Importation by a Government entity or supply to Government entity of goods or services to be useful for implementation of project funded by:-"*

(i) *The Government...*"

**MWENYEKITI:** Nenda tu moja kwa moja ya kwako ambayo unataka nne iingie kwa hiyo, "*implementation of a project funded by...*" anza ya kwako.

**MHE. CATHERINE N. RUGE:** "*Importation by a person, company or private sector of goods or service to be useful for the public interest.*"

**MWENYEKITI:** Hapo inaweza kukaa ama imegoma?

**MHE. CATHERINE N. RUGE:** Imegoma, lakini lengo langu ni kwamba *private sector* iwe *incorporated*.

**MWENYEKITI:** Sawa.

Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali nadhani umeliajata wazo la Mheshimiwa Catherine Ruge kwamba pengine mnavyoangalia huko kwenye haya marekebisho mlivoleta muangalie pia taasisi binafsi zinazoleta kwa ajili ya shughuli za umma ama taasisi za umma yaani imelata binafsi lakini yanakwenda kufanyakazi ya umma nadhani ndiyo lengo hasa japo kuwa marekebisho yake hayawezi sasa kuingia kwa leo hapa, lakini jambo ambalo kama Mheshimiwa Waziri wa Fedha ulivyo sema kwamba mnaendelea kuyatazama ni muhimu kuyatazama kwa sababu wakati mwininge makontena yanabaki pale kwa muda mrefu kwa vitu ambavyo vinakwenda kutumika moja kwa moja kwenye shughuli ya umma na siyo kwenye shughuli binafsi. (*Makof*)

Kwa hiyo nadhani ndiyo hoja yake hasa ila marekebisho yake hayawezi kuingia hapa moja kwa moja, kwa hiyo miltazame kadri mnavyoangalia hayo marekebisho ili hata huyu ambae analeta kwa ajili ya umma basi na yeye aangaliwe hata kama siyo taasisi ya Serikali.

*(Ibara iliyo tajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

**NDG. LAWRENCE MAKIGI - KATIBU MEZANI:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge zima imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Subirini kwanza Wabunge, hebu nitoe maelezo kwanza kwenye hii 100; kulikuwa na marekebisho ya Mheshimiwa Ruge ndiyo hayo tumeyatolea maelezo Serikali iyatazame katika hizo itakazoleta baadaye. Lakini tunayo marekebisho yaliyoletwa tena na Serikali yake ya ziada ambayo yanafuta marekebisho ambayo Serikali ilikuwa imeleta awali katika kifungu cha 100. Sasa nilivoyatazama hapa, nataka kumbukumbu zile vizuri. Nilivoyatazama hapa haya marekebisho ya ziada yaliyoletwa na Serikali sijui kama wote tuko hapo. Kuna marekebisho ya ziada yaliyokuja, yako kwenye karatasi moja na yanahusu kifungu C(c) ambacho kiko ukurasa wa tano kwenye yale marekebisho ya mwanzo.

Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, tuko wote hapo? Unayo hii sio? Sasa nilivyoipitia hapa mbele Waheshimiwa Wabunge, tunavyozungumzia kupitisha hiki kifungu pamoja na marekebisho ya Serikali sio haya waliyoyleta baadaye kwa sababu haya yaliyoletwa baadaye hayaweki mtiririko mzuri wa kisheria. Kwa hiyo, haya Bunge linashauriwa kuyakataa haya. Lakini yale mliyoleta mwanzo ndiyo tunayoyakubali. Haya mliyoyleta baadaye, Mheshimiwa AG labda kama unataka kutoa maelezo.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tulileta *further schedule of amendment* yaani marekebisho ya ziada baada ya kugundua kwamba yale marekebisho ya awali tuliyoyaleta yalifanya rejea kifungu kisicho sahihi. Ukienda kwenye Ibara C(c) inarejea Kifungu cha 2(a)(i) lakini kifungu kilichokwuwa kinakusudiwa ni kifungu cha 2(b)(i) na ndiyo maana tukasema tufute tu hayo marekebisho ili tuweze kurekebisha hilo kosa. Tukiacha hivi kama ilivyo itabaki na kosa la kiuandishi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa AG tukiacha ipi itabaki na makosa ya kiuandishi, hii ambayo mliyleta kwanza? Sasa mtakuwa mmetusaidia kwa upande wa Bunge kwa sababu

pia Bunge halilazimiki kukubali marekebisho ya Serikali kwa hiyo sisi tutakachofanya ni kuyakataa marekebisho ya Serikali kwenye kifungu namba 100 ili kibaki kama kilivyokuwa, hiki ambacho mmekileta mwanzo. Nasema hiyvo kwa sababu haya marekebisho mliyoyaleta baadaye hayakamilika kiuandishi. Kwa sababu mmesema; *the schedule to the bill*. Sasa *bill* hii hatuna *schedule*, kwa hiyo, ilikuwa hii yenye ni *schedule of amendment to this bill* sasa kwa sababu hii hajakamilika, hii tunaikataa. Tukishaikataa hii sasa sisi kama Bunge tunakataa marekebisho ya Serikali yaliyoletwa kuhusu kifungu namba 100, kwa hivyo, kinabaki kama kilivyo. Nadhani tumeenda vizuri Mwanasheria Mkuu wa Serikali. (*Makofi*)

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho wa siku tutafikia lengo hilo hilo moja kwa hiyo tunapokea mwongozo wako. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Sawa. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tulivyopitisha kifungu namba 100 kwa marekebisho yale ya Serikali yaliyokuwa yameletwa kwenye kifungu 100 hayajakubaliwa. Kifungu kimepita kama kilivyo. (*Makofi*)

Katibu!

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa Taarifa kwamba Kamati ya Bunge zima imekamilisha kazi yake.

*(Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Mtoha hoja taarifa.

## TAARIFA

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 89 Fasili ya kwanza ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016, napenda kutoa Taarifa kwamba Kamati ya Bunge zima imeupitia Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria

mbalimbali Na. 6 wa Mwaka 2019 [*The Written Laws Miscellaneous Amendments No. 6, Bill 2019*] Ibara kwa Ibara na kuukubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 6 Mwaka 2019 [*The Written Laws Miscellaneous Amendments No. 6 Bill, 2019*] kama ulivyorekebishwa katika Kamati ya Bunge zima sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.  
(*Makofi*)

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Sasa nitawahoji.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)  
(*Hoja illiamuliwa na Kuafikiwa*)

**Muswada wa Sheria kwa ajili ya Kufanya Marekebisho katika Sheria Mbalimbali kwa lengo la kuondoa mapungufu ambayo yamejitokeza katika Sheria hizo wakati wa utekelezaji wa baadhi ya masharti katika Sheria hizo (*A Bill for an Act to Amend Certain Written Laws*)**

(*Kusomwa Mara ya Tatu*)

(*Muswada wa Sheria wa Serikali Ulipitishwa na Bunge*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa taratibu zetu Bunge limeshakamilisha kazi yake kwenye huu Muswada ambaao ulikuwa umeletwa kwa ajili ya marekebisho ya sheria mbalimbali. Kwa hivyo, kwa taratibu zetu Muswada huu Bunge kwa kuwa limemaliza kazi zake kwa mujibu wa Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, utapelekwa kwa Mheshimiwa Rais ili na yeze atimizie la kwake chini ya Katiba hiyo kwenye Ibara ya 97.

Kwa hiyo nichukue fursa hii kuwapongeza sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali lakini pia Wizara mbalimbali zitakazohusika na utekelezaji wa sheria hizi ambazo zimerekebishwa na Bunge. Tuwatakie utekelezaji mwema na tunaamini kwamba zile changamoto ambazo mmeziletea haya marekebiso na Bunge sasa limeshatunga sheria kwa hiyo mnazo nguvu za kuendelea kufanya hizo kazi na tunaamini kwamba kadri mnavyosikiliza mawazo ya Waheshimiwa Wabunge na mapendekezo yao mtaendelea kuleta marekebiso ya sheria mbalimbali kama ambavyo sheria hizi ambazo mmezileta safari hii, ninyi ni mashahidi Wabunge wengi walikuwa wakipongeza katika michango yao kwamba Serikali imesikiliza mawazo ya Waheshimiwa Wabunge na imechukua hatua. (*Makofii*)

Kwa hiyo ni jambo jema na hata haya mengine ambayo Wabunge wanaendelea kuchangia basi muendelee kuyachukua na kuyafanya kazi na tunaamini kwamba sote tutaweza kusonga pamoja na kulifanya Taifa letu lisonge mbele zaidi.

Kwa hiyo, ninawapongeza sana na wataalam wenu na ninaamini mtaendelea kuyafanya kazi hata yale ambayo safari hii hatukufanikiwa na hata yale ambayo Wabunge wamependekeza kuboresha katika haya tuliyoyarekebisha naamini mtaendelea kuyatilia maanani na kuchukua hatua ili Waheshimiwa Wabunge kama wawakilishi wa wananchi basi waone mambo ya wananchi yanasonga mbele.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 12.50 Jioni Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Ijumaa,  
Tarehe 13 Septemba, 2019, Saa Tatu Asubuhi)*